

**PAULO, MJUMBE WA MUNGU
(MWALIMU)**



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

Mwaka wa Kwanza

Kitabu cha Tatu

PAULO, MJUMBE WA MUNGU

VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

(MWALIMU)

Mwaka wa Kwanza

Kitabu cha Tatu

Africa Coordinated Curriculum for Bible Study

J1 - 3Ts

With permission of International Publications Services



**Published and Printed by
Baptist Publications House
Thika Road, Ruaraka
Box 30370, Nairobi**

© Copyright . 1988

Baptist Publications House

All Rights Reserved

Wewe pia unaweza kukua na kupata imani zaidi kwa kujifunza mafunzo haya.

(Unapofunga darasa kwa maombi, kumbuka kuwaombea wanafunzi wako pamoja nawe ili maweza kutambua hitaji la kushi maisha mema kwa ajili ya Kristo kama Paulo alivyofanya.)

VIFUNGU VYA KUKUMBUKA:

Tabuni basi, mrefee, ili dhambi zenu zifuwe. Matendo 3:19a

Mwenende kama uliyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa, mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu. Yakobu 1:10

Nitawimbishe Bwana maadamu ninalishi; nitamsingilia Mungu wangu nikitwa hai. Zaburi 104:33

Amin, amlu, nawaambia, Yeye alisitiaye mmoja langu na kuwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa mliche; wala haligili hukumuuni, bali amepita kutoka maufini kuingia uzimani. Yohana 5:24

Kwa maana mimi, Bwana, Mungu wako, nitakushika mkono wako wa kuume, nitakwambia, Usilogope; mimi nitakusaidia. Isaya 41:13

Ninaweka Bwana mbele yangu daima, kwa kuwa yako kuumei kwangu, sitaondosha. Zaburi 16:8

Kisha nitaisikia sauti ya Bwana, akisema, Ninatume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, "Mimi baya, nitume mimi." Isaya 6:8

Maana mamepea kwa ajili ya Kristo, si kuwamini tu, ila na kutewa kwa ajili yake. Wafilipi 1:29

Hata twaathubutu kusema, Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogopa; mwanadamu atanitenda nini?

Waraka kwa Waebrania 13:6

Juoni ya kuwa yeye amrefezaye mweye dhambi hata atoke katika njia ya upolevu, ataokoa roho na njia ya upolevu, ataokoa roho na maufi, na kufunika wingi wa dhambi. Yakobo 5:20

Huku akiyua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoshidi. Warumi 4:21

Lakini nawambia ninayi mnaosikia, wapendani adui zenu, watendani mema wale ambao wawachukia ninyi. Luka 6:27

kuwa Mkristo." Sasa, katika ramani yako unaweza kuandika namba 1 kando ya mji ambao Paulo aligeuzwa kuwa Mkristo. Hadithi hii inapatikana katika Matendo 9:3-9.

"Mambo mengi ya ajabu yalinifanyikia katika safari zangu. Nilikutana na watu wengi walionitakia baraka za Bwana. Siku moja marafiki wengine walionionya nisiende mji wa Yerusalemu. Watu hawa walikuwa marafiki zangu wa mji wa Tiro. Kabla ya kuwaacha na kuendelea na safari yangu, tulipiga magoti pwani kuomba." Tafuta mji huu katika ramani yako, kisha andika namba 2 kando yake. Ukihitiaji kutafuta majibu ya maswali haya, soma Matendo 21:3-6.

"Wakati nilipokuwa katika mji wa Kaisaria ilinibidi kupeleka kesi yangu mbele ya liwali mpya. Jina la liwali huyu mpya lilitwa Festo. Nilikuwa nimekwisha kukaa gerezeni miaka miwili. Sasa wakuu wa Wayahudi walikuwa bado wakijaribu kunifanya niuawe. Kisha nilipeleka kesi yangu mbele ya mfalme, aliyeitwa Agripa. Yeye pamoja na Bernike, dada yake, walisikia maneno yangu."

Tafuta mji huu katika ramani yako na uandike namba 3 kando yake. Ukihitiaji kuhakikisha majibu yako, soma Matendo 25:13-22.

"Nilitaka rufani kwa Kaisari ili aweze kusikia kesi yangu, kwa hivyo Festo alinituma Rumi. Safari ya kwenda Rumi ilikuwa ndefu na mambo mengi ya ajabu yalinifanyikia njiani. Niliwambia nahodha wa

merikebu tukae pale katika Bandari Nzuri wakati wa baridi. Lakini yeye hakunisikitiza, basi tukaanza safari ya kwenda Foinike. Tulipokuwa njiani, dhoruba kali ilitujia. Baada ya siku nyingi, merikebu yetu iliyunijika na sisi sote tukafika salama katika kisiwa cha Melita."

Tafuta kisiwa hiki katika ramani yako halafu andika namba 4 hapo. Maelezo juu ya safari hii ya ajabu yanapatikana katika Matendo 27:8-12, 41 na Matendo 28:1.

WAKATI WA KUFUNGA

Waulize wanafunzi swali hili: "Niambi ni baadhi ya mambo ambayo tumekwisha kujifunza katika maisha ya Mtume Paulo?" (Wape wakati wa kujibu.) Utataka kuongoza wakati huu wa mazungumzo kwa kuwakumbusha wanafunzi kweli za Biblia ambazo zimekwisha kufundishwa katika masomo yote ya kitabu hiki. Kwa hivyo itakubidi kufahamu hadithi ambazo tumekwisha kujifunza na ukweli hasa muhimu wa kila hadithi.

Paulo anaweza kuwa mfano mwema kwa maisha yetu sisi kama Wakristo. Imani yake na ushujaa wake hata wakati wa shida, yanaweza kututia moyo hata sasa. (Je! mwalimu, umekwisha kujifunza nini kwa Paulo? Umekwisha kujifunza kudai ahadi za Mungu ukijua ya kwamba utazitimiza? Je! umekwisha kupata furaha ya kushiriki imani yako na wengine kama Paulo alivyoshiriki imani yake na watu aliokutana nao?

VIJANA TUIJIFUNZE BIBLIA [MWALIMU]

Mwaka wa Kwanza

Kitabu cha Tatu

YALIYO MO

Sura

Ukurasa

1. Ugeuzi Kamili	5
2. Kumpa Kristo Nafasi ya Kwanza	9
3. Kuimba Gerezani	12
4. Paulo Ahubiri Athene	16
5. Usiogope	20
6. Kumpendeza Mungu Badala ya Mwanadamu	24
7. Paul Aenda Yerusalemu	29
8. Kuteseka kwa Ajili ya Kristo	35
9. Mungu Amlinda Paulo	39
10. Kumshuhudia Kristo	44
11. Kuhakikisha Ahadi za Mungu	48
12. Jinsi ya Kuwatendea Maadui	54
13. Somo la Marudio	59

kwa Wakristo wote wa nyakati zile alipoishi.

Kwa kurudia maisha ya Paulo, ingekuwa jambo la busara kuyachukua masomo yote na kuyasoma tena. Chukua Biblia yako na kusoma maisha ya Paulo katika kitabu cha Matendo. Soma kitabu hiki chote! Wakati unapojiandaa kufundisha, fikiria tena masomo haya na mafunzo tuliyojifunza kwa kusoma habari za maisha ya Paulo.

Bila shaka utataka kuomba wakati unapojiandaa kufundisha ili Bwana ataweza kukutumia wewe kuwasaidia wanafunzi wako waweze kufahamu vyema mfano wa Paulo wa kuishi maisha mema ya Kikristo. Ingawa miaka mingi sana imekwisha kupita tangu Paulo alipofanya safari zake, bado tunaweza kufuata mfano wake wa kueneza injili. Tambua mfano huu ambao Paulo alituwekea sisi sote. Kusudi la somo hili ni kuonyesha tena ya kwamba Mungu atatugeza kuwa wafuasi wake waaminifu.

MAMBO YA KUKAZA

Somo hili la marudio linakaza mambo manne muhimu.

1. Hatua yetu ya kwanza kwa wokovu ni kuacha maisha yetu ya dhambi na kupokea maisha mapya katika Bwana.

2. Kwa kumpa Kristo nafasi ya kwanza maishani mwetu, tunaweza kumwamini kutulinda na kushiriki upendo wake na wengine.

3. Hata wakati wa mateso na udhalimu, inatupasa kuwa na nia ya kumshuhudia kila mtu nguvu za Yesu Kristo za kutuokoa.

4. Kila ahadi ya Bwana itatimizwa kama tukiwa na imani ya kutaka ahadi hizo na kufuata mapenzi ya Mungu kwa maisha yetu.

KULIFUNDISHA SOMO

Somo hili la marudio linakufanya kuwa kama maarifa ya kujifunza. Kwa kujifunza na kurudia masomo yaliyopita juu ya Paulo, wanafunzi wataabiliwa na mafunzo muhimu ya Kikristo ambayo yatastawiisha maisha yao. Wanaposoma mambo haya mafupi ya ajabu katika maisha ya Paulo wataweza kupata maana hiyo. Tumia mikazo hiyo minne iliyoandikwa hapo juu kuhusu kila somo, na uwasaidie wanafunzi kutafuta kwele za Biblia wakati wanapotenda kazi ya kufanya. Watie moyo sikuzote kwa kuwasaidia kukumbuka mambo ambayo wamekwisha kujifunza. Watakuwa na tamaa ya kutimiza kila sehemu ya kazi yao ya kufanya.

KAZI YA KUFANYA

"Nilikuwa njiani kwenda Dameski kuwatesa Wakristo. Kwa ghafla nuru kutoka mbinguni itanangaza kote kote na kunipofusha macho. Sauti ilinika kwa jina langu la Kiyahudi na kusema, 'Saul, Saul, mbona wanuudi?' Sauti hii ilikuwa ya Bwana aliyekuwa na kazi aliyotaka nifanye. Ni hapa ndipo nilipogeuka

watendeeni mema wale ambao wawachukia ninyi." Luka 6:27

Yesu ndiye aliyesema maneno haya. Aliwapenda maadui zake. Alikwenda huku na huko akiwasaidia watu ambao hawakumwamini. Anajua kwamba kulipiza kisasi si kuzuri tena hakuleti furaha, kwa hivyo ni bora kwetu kuwapenda maadui zetu.

WAKATI WA KUFUNGA

Mtu akiwa anakuchukia na kukutendea kama adui, utafanya nini? Ni jambo la kawaida kwako kumfikiria mabaya. Ni jambo la kawaida kwako kutaka kumlipiza kisasi. Labda unaweza kumwomba apatwe na jambo fulani baya, kama kupata shida shuleni au kutopendwa tena na marafiki zake wengine.

Sura ya Kumi na Tatu

SOMO LA MARUDIO

MASOMO YA BIBLIA: Maandiko yote ya masomo ya kitabu hiki

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Hili ndilo somo la mwisho juu ya Mtume Paulo. Kutokana na masomo yote ya kitabu hiki ambayo tumejifunza, tumemwona Paulo jinsi alivyokuwa kuanzia alipokuwa

Hayo ni mawazo ya kawaida, lakini ukiwa Mkristo, umekwisha kugeuka kabisa kama Paulo alivyofanya na kuacha mawazo kama hayo. Humtendei mabaya mtu anayekuchukia. Yesu amekwisha kukupa asili mpya inayotaka kufikiri na kuwaza na kutenda kama Yesu alivyofanya wakati alipokuwa hapa ulimwenguni. Yesu anaweza kukusaidia kuwapenda adui zako badala ya kuwachukia. Anaweza kukusaidia kuwa na nia ya kumwomba adui yako.

Je! utamwomba Bwana kukusaidia kumtii kwa kuwapenda na kuwa mwema kwa maadui zako? Funga kwa maombi ili wanafunzi wako watakuwa na moyo wa kusamehe na kuwapenda wote ambao wanawachukia.

kiongozi wa Kiyahudi aliyewatasa Wakristo mpaka akawa mtu wa Mungu aliyeneza injili ya Bwana katika kila mahali alipopatembelea. Labda Paulo ndiye mwandishi muhimu sana wa Agano letu Jipya. Vitabu vyake na barua (nyaraka) zake zimewapa Wakristo uongozi, siyo tu kwa wale aliowaandikia, bali pia ni

Sura ya Kwanza

UGEUZI KAMILI

Mungu anaweza kutugeuza sisi kama alivyomgeuza Sauli.

MAMBO YA KUKAZA

1. Ni muhimu kuwaonyesha wanafunzi wako ya kuwa Sauli alibadilika kabisa baada ya kupokea Kristo kama Mwokozi wake.
2. Tukimwamini Kristo, Mungu atabadilisha mawazo yetu juu ya watu wengine.
3. Mungu hubadilisha mambo tunayotaka na yale tunayotaka kufanya.

KULIFUNDISHA SOMO

Paulo ni jina la Mkristo shujaa ambaye tutajifunza habari zake. Alikuwa Myahudi na alizaliwa katika mji ulioitwa Tarso. (Waambie vijana kutafuta mji huo wa Tarso katika ramani.) Wazazi wake walikuwa watu wema, na walimwamini Mungu. Paulo (kwa wakati ule alikuwa akiitwa Sauli) alikua na kumwamini Mungu mmoja tu wa kweli. Labda wazazi wake walikuwa washonaji hema na Sauli alijifunza kwao kushona hema. Alipokuwa kijana alikwenda shuleni Yerusalemu kujifunza sheria za Wayahudi.

Hata siku moja Sauli alipokuwa Yerusalemu, alisikia habari za Kristo. Watu wengi walikuwa wakiamini ya kwamba Yesu Kristo alikuwa Mwana wa Mungu. Sauli alimpenda Mungu,

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wakati unapojiandaa kufundisha labda utapendezwa na mambo fulani kuhusu maisha ya Paulo. Alizaliwa katika mji wa Tarso. Wakati huo alikuwa akiitwa Sauli, kisha baadaye akaitwa Paulo. Alikuwa na wazazi wa Kiyahudi waliomwamini Mungu na walioshika sheria za Musa. Wazazi wake walimfundisha kumpenda Mungu na kutii sheria. Sauli alifikiria kwamba ilikuwa vema kuwatasa Wakristo. Hakuamini ya kwamba Yesu wa Nazareti alikuwa Mwokozi aliyehidiwa kuja.

Mungu alitaka kutumia Paulo kuwafundisha watu habari za Kristo. Alijua ya kwamba Paulo alikuwa na elimu nzuri na angeweza kusema na watu wa nchi nyingine. Mungu akamgeuza Sauli. Alimsamehe dhambi zake akamtumia kuwapelekea watu wa Mataifa Neno la Kristo.

Masomo juu ya safari za Paulo ni ya kupendeza. Alipatwa na mambo mengi. Mengine kati ya mambo hayo ni mazuri na mengine ni mabaya. Tunajifunza kwamba ugeuzi wa Paulo ulimletea mabadiliko kamili katika roho yake na katika maisha yake. Kusudi la somo hili ni ya kwamba

na alitaka kumpendeza. Alifikiri kwamba ilikuwa makosa kwa mtu yeye yote kusema aiti Kristo alikuwa Mwana wa Mungu. Alitwisha kujifunza sheria za Agano la Kale, na alidhania kuwa Mungu angemtaka kuwaadhibu watu waliocema Kristo alikuwa Mwana wa Mungu. Wakati wote alipowapata watu waliomwamini Kristo, alitakamata na kuwaweka gerezeni, kisha akawapiga.

Wakati ambapo Stefano alipigwa kwa mawe, Sauli alikuwapo alitazama, tena yeye ndiye aliyetunza nguo za watu wale waliomtupia Stefano mawe. (Wanafunzi wasome Matendo 7:58.) Baada ya Stefano kufa, Sauli alikwenda nyumba za Wakristo wengi, akawatoa nje na kuwafunga gerezeni.

Kuhani mkuu na watawala pia walifitiri kwamba Sauli alikuwa atienda haki kwa kuwaadhibu Wakristo. Wakati Sauli apowaomba ruhusa kwenda Damaski kuwakamata Wakristo wa huko, walifurahi sana kumruhusu kwenda.

Mji wa Damaski ulikuwa maji 130 hivi kaskazini mashariki ya mji wa Yerusalemu. (Wambie wanafunzi kutafuta Yerusalemu na Damaski katika ramani.) Kulikuwa na Wakristo wengi sana Damaski, na Paulo alitaka kuwakamata na kuwaleta wengi sana Yerusalemu kama aliyoweza, na kuwaadhibu. Aliwachukua watu pamoja naye ambao wangependa wafungwa.

Hata siku moja mchana, baada ya Sauli kusefiri siku kutoka Yerusalemu,



alitakibia mji wa Damaski. Hakutaka kupumzika wakati ule wa jua kali, bali alijibarokisha kwenda. Kwa ghafla, nuru kutoka mbinguni ilimwagaza kote kote. Yeye pamoja na watu wale alikuwa nao walianguka chini. Sauli alisikia sauti ikimwita jina. Alitazama ni nani yule aliyelitika jina lake. Bwana akamjibu, "Mimi ndimi Yesu unayenitadhi." (Matendo 9:5) Pia alimwambia Sauli kusimama na kuingia katika mji wa Damaski mpaka kwa nyumba ya mtu mmoja aliyetwa Yuda, na pale ndipo angambiwa jambo la kufanya. Paulo hakutweza kuona kwa sababu nuru ile ilipofusha macho yake. Watu wale waliokujia pamoja naye, walimshika mkono wakamwongoza mpaka kuingia mjini.

Paliuwapo Damaski Mkristo mmoja aliyetwa Anania. Mungu alisema naye katika maono

alikamatwa na kupelekwa Rumi kama mfungwa, na muda mfupi baadaye alihukumwa kufa na Nero mfalme mwovu.

Jei huu ulikuwa mwisho wenye huzuni kwa mtume Paulo? Ia, kwa sababu tunajua ya kwamba baada ya kufa kwake hapa ulimwenguni aliingia mara mbinguni na kukaa pamoja na Bwana wa ajabu.

KAZI YA KUFANYA

Mungu aliokea tena maisha ya Paulo. Wakati huu alimwoko Paulo katika bahari iliyochafuka na kuvunja merikebu waliyokuwa wakisafiria. Baada ya muda mfupi Paulo na abiria wengine wakitambua kwamba walikuwa katika kiswa cha Melita. Piga mistari chini ya majibu ya kwele ya maswali yafuatayo.

1. Hali ya hewa ilikuwaje? ya moto kidogo ya mvua na baridi
2. Wenyeji walikuwaje wakariimu kwa watu wale waliotoka melini? Waliwasha moto.

Walivachukua Paulo na wengine.

3. Ni kitu gani kilichomzonga-zonga Paulo mkononi? ndege —nyoka

4. Watu walipoona kitu hiki kilizonga-zonga mkononi mwa Paulo, Jei walifikiri Paulo alikuwa nani. mchawi —mwuaji

5. Walipoona kwamba hakuna dhara lo lote lililompata Paulo, walimfikiria kuwa nani?

mungu malaika

Paulo alishukuru sana kwa ajili ya ukarimu wa wenyeji wale. Andika majibu ya maswali yafuatayo:

1. Jei Paulo alifanya Publio, mkuu wa kiswa hiki, jambo gani? Alimponya babaye.

2. Jei Paulo alitafanyia wengine waliokuwa katika kiswa hiki jambo gani? Alitaponya wagonjwa wao.

3. Wenyeji waliwapa Paulo na wenzake vitu gani wakati walipokuwa wakiondoka. zawadi na vitu waliyohitaji

Paulo alitambua Wayahudi wa Rumi sababu iliyomfanya kuwa huko. Kata maneno yaliyo katika alama hii () ambayo Paulo hakuwaambia Wayahudi wale.

"Sikufanya neno kinyume cha watu wetu. Lakini nililewa kama (mfungwa) (tatuwa) kutoka (Bendari—Nanti) (Yerusalemu), nikaitwa katika mkono ya (Weytanti) (Warumi) Waliponiliza- uliza, hawakuona sababu yo yote kwangu kuawa, lakini kwa sababu (Weytanti) (Wayahudi) walimchukua, na kusema maneno yasiyo ya kwele juu yangu, nilitaka ruhani kwa Kaisari. Nilitwita niwaoone na kusema nanyi kwa sababu (nimefungwa kwa minyororo) (fatahebiwa—karibuni) kwa ajili ya Kristo ambaye ni tumaini la Israeli."

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Lakini nawaambia ninyi mnaosikia, wapendani adui zenu,



kukaa Rumi kwa siku tatu, aliwaita wakuu wa Wayahudi pamoja kuwaeleza sababu ya kuletwa kwake Rumi kama mfunzwa. Waulize wanafunzi wako kama wanajua sababu iliyomfanya Paulo kuletwa Rumi. Wape wakati wajaadiliane jambo hilo. Jibu ni kwamba Paulo alikuwa ametaka rufani kwa Kaisari kwa sababu wakuu wa Wayahudi mjini Yerusalemu walitaka kumfunga bure bila sababu yoyote maalum kulingana na sheria ya Kirumi. Pia Paulo alijua kwamba ilikuwa mapenzi ya Mungu kwake kwenda Rumi, na labda hii ndiyo iliyokuwa njia ambayo Mungu alikuwa akitimiza mapenzi hayo yake.

Wakuu hawa wa Wayahudi walimwambia Paulo ya kwamba hawakupata barua zo zote zenye habari zake, wala hawajasikia habari au neno lo lote baya juu yake. Walimwambia ya kwamba walitaka kusikia maoni yake kuhusu imani ya

Kikristo. Paulo aliagana nao siku ambayo wao wangukuja kumtembelea nyumbani mle alimokuwa alikaa. Siku hiyo ilipofika, walikuja kwa wingi, na kutoka asubuhi hadi usiku aliwaeleza kwa utaratibu na kuwashuhudia mambo yaliyofundishwa na Agano la Kale juu ya Kristo.

Wengine kati yao waliamini maneno ya Paulo kuwa ni ya kweli na wengine hawakuyamini. Kulikuwa na hali ya kutopatana kati yao, kisha wakaondoka, wakaenda zao. Paulo alijaribu kuwashawishi ya kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zao, na kwamba Kristo ndiye aliyekuwa Mwana wa Mungu aliyeahidiwa Wayahudi. Soma Matendo 28:28 kuona mambo ambayo Paulo aliwambia mwishowe.

Paulo alikuwa bado mfunzwa, lakini alikuwa alikaa katika nyumba aliyopanga kwa pesa zake mwenyewe. Alikuwa bado yuko chini ya ulinzi, lakini alikuwa na uhuru wa kuwakaribisha wageni wakati wote wote. Aliwakaribisha watu wote waliokuja kwake na kuwahubiria ufalme wa Mungu na kuwafundisha habari za Bwana Yesu Kristo. Hakuna mtu aliyemzuia kufundisha hayo.

Wataalamu wengi wa Biblia wanaamini kwamba aliachiliwa huru baada ya miaka hii miwili. Alikwenda katika nchi nyingine na kuhubiri tena kama mtu huru. Wataalamu wa Biblia pia wanaifikiri ya kwamba baadaye Paulo



Mkristo? (Uliza:) Alienka kwa njia zipi? Sauli alitaka sasa kufanya mambo yaliyompendeza Mungu. Hakutaka kuwatesa Wakristo tena. Kuanzia hapo alitaka kuwambia wengine habari za Kristo kama Mwokozi wake.

Masomo mengine yajayo yatahusu mahali na jinsi Sauli alivyomtumikia Kristo.

KAZI YA KUFANYA

Jaza nafasi katika sentensi hizo hapo chini kwa maneno yanayofaa.

1. Sauli aliwachukia Wakristo.
2. Sauli alifikiri kwamba alikuwa akimsaidia Mungu kwa kuwaadhibu Wakristo.
3. Sauli alipokuwa njiani kwenda Damaski alipofushwa.
4. Je! kulifanyika nini wakati Anania alipomwendea Sauli nyumbani mwa Yuda? Anania aliweka mikono yake juu ya Sauli na akapata kuona tena. Alijazwa na Roko Mtakatifu. Alibatizwa.

akamwambia kuondoka kwenda katika njia iliyoitwa Nyofu na kuingia nyumba ya Yuda na kuuliza pale kama kuna mtu aitwaye Sauli. Mungu alimwambia Anania kuweka mikono yake juu ya Sauli ili angeweza kuona tena. (Uliza:) Je! unafikiri kwamba Anania aliogopa? Ndiyo. Anania aliogopa kwa sababu alikuwa amekwisha kusikia habari za Sauli jinsi alivyowatesa Wakristo. Mungu alimwambia Anania kwenda kumwona Sauli kwa sababu alikuwa amemchagua Sauli kuwambia watu habari za Kristo. Anania aliondoka akacenda nyumbani mwa Yuda, akamweka Sauli mikono. Alimwambia Sauli ya kwamba Bwana Yesu alikuwa amemtuma kwake, amweke mikono ili apate kuona tena. Pia alimwambia Sauli ya kwamba angejazwa Roko Mtakatifu. Alipomweka Sauli mikono, Sauli aliweza kuona tena mara moja, akasimama, akabatizwa.

Kabla ya Sauli kuweza kutumiwa na Mungu ilimbidi kugeuzwa na kumpokea Kristo. (Uliza:) Je! unafikiri Sauli aligeuzwa na kuwa

5. Sauli alitaka kufanya nini baada ya kugeuzwa kuwa Mkristo? Alitaka kuwaambia watu wengine habari za Yesu.

Jibu sentensi zifuatazo kwa kuandika ferufi "K" kando ya zile ambazo ni kwele, na kuandika herufi "M" (makosa) kando ya zile ambazo si kwele.

K 1. Kwanza, Sauli aliwachukia Wakristo.

M 2. Kristo alisema na Sauli akiwa njiani kwenda Antioka.

K 3. Sauli aliancha dhambi na kumfuata Mwana wa Mungu.

M 4. Anania hakwenda kumsaidia Sauli.

K 5. Sauli alibatizwa.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Tubuni basi, mrefee, ili dhambi zenu zifutwe." Matendo 3:19a

Kama maelezo ya kifungu cha kukumbuka, unaweza kusema ya kwamba Sauli alipokuwa njiani kwenda Dameski aliacha dhambi zake na kumpokea Mwana wa Mungu. Aligeuzwa kuwa Mkristo na fikira zake pia zikabadilika. "Kugeuka" maana yake ni kuacha njia uliyokuwa ukifuta, na kupita njia nyingine. Ikiwa Kristo ndiye Mwokozi wako, basi dhambi zako zimesamehewa na kusahuliwa. Sasa unafuata njia mpya katika fikira zako

na katika matendo yako. Mungu hubadilisha mawazo yako juu ya wengine; hubadilisha mambo unayotaka (ya anasa), na yale unayofafanya ambayo si mazuri.

WAKATI WA KUFUNGA

Mwalimu, juilize wewe mwenyewe swali hili: Je! Kristo amebadilisha maisha yangu kwa njia ipi? Je! vijana ninaowafundisha wanaweza kumwona Kristo ndani yangu? Pia, uwaulize wanafunzi ambao wamekwisha kumpokea Kristo kuwa Mwokozi kama Kristo huyo amegeuzwa maisha yao. Jinsi maisha ya Paulo yaliyogeuzwa, ndivyo kila maisha yanavyoweza kugeuzwa. Robo Mtakatifu ataingia katika roho, na kila maisha yatageuzwa kuwa bora na yenye furaha zaidi. Waulize wanafunzi wako kuombeana wao wenyewe na kumwomba kila mmoja ili Kristo atakuwa mwokozi wa kila mwanafunzi.

Funga darasa kwa maombi. Waulize wanafunzi kama kuna ye yote kati yao ambaye angependa kuongoza kwa maombi. Usiwalazimisha kuomba. Wanapaswa kuomba kama wao wenyewe wanataka. Ikiwa hakuna ye yote anayetaka kuomba kwa sauti, basi unaweza kufunga kwa maombi.

Ndiyo, ni mwjiza wa Mungu. Mungu alikuwa akiminda Paulo.

Publio ambaye alikuwa mkuu wa kisiwa hiki, alikuwa na nyumba karibu na mahali pale ambapo abiria wa merikebu ile iliyovunjika walifikia nchi kavu. Publio alikuwa mkarimu sana kwa watu wote walikuwa pamoja na Paulo. Paulo alipata nafasi ya kulipiza ukarimu huo wake. Babaye Publio alikuwa mgong'wa sana. Paulo alimtembelea, akamwomba, kisha akamwekelea mikono, akamponya. Kisha wagonjwa wote wa kisiwa hiki walimjia Paulo na wote wakaponywa.

Je! wenyeji wa kisiwa hiki walionyesha jinsi gani shukrani yao kwa mambo yote ambayo Paulo aliwafanyia? Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 28:10.

Yulio na askari zake na wafungwa walika katika kisiwa hiki kwa muda wa miezi mitatu walingojea wakati mzuri wa kusafiri. Wakati huo ulipofika, walingia katika merikebu ya Iskanderia iliyokuwa ikienda Italia. Kisha walikwenda Regio na baada ya siku moja upepo wa kusini ulivuma, na siku ya pili wakawasilii Putcoli iliyokuwa bandari ya Italia.

Walika Putcoli siku saba kabla ya kwenda Rumi. Paulo aliwona ndugu Wakristo katika bandari hiyo. Alikuwa hajapata kuwona, lakini walikuwa ndugu zake kwa sababu wao pia walimpenda Bwana Yesu Kristo. Putcoli ndiyo iliyokuwa bandari kubwa na merikebu zote zilizojuia katika sehemu hii ya Italia

zilisimama hapa na kupakua ngano au bidhaa zote walizoleta. Abiria waliweza kushuka na kwenda katika sehemu zo zote za nchi hii waliotaka kwenda.

Wakati Paulo alipokuwa Putcoli, Wakristo wa Rumi walisikia habari ya kwamba alikwisha kuwasili Italia. Paulo hakuwajua Wakristo hawa, lakini alikuwa amekwisha kuwaandikia barua. Walimjua na walikwisha kusikia habari za safari zake za kuwapelekea Wayahudi na watu wa mataifa Injili ya Kristo. Wakristo wa Rumi walimthibitisha Paulo ya kwamba walikuwa na tamaa juu ya kuja kwake kwa sababu waliembea mwendo mrefu kwenda kumlaki. Wengine kati yao walimlaki katika umbali wa kilometa sitini na tano kutoka Rumi. Wengine walimlaki karibu na Rumi. Paulo alitiwa moyo kujua ya kwamba Wakristo hawa walikuwa pale.

Je! Yulio aliwafanyia wafungwa wake jambo gani wakati walipofika Rumi? Wafungwa wote isipokuwa Paulo walikabidhiwa mikononi mwa akida wa ulinzi. Paulo aliruhusiwa kutaa peke yake pamoja na askari mlinzi, lakini hakuwa huru kwenda mahali po pote alipotaka. Alifungwa na minyororo. Luka na mwezake ambao walisafiri pamoja na Paulo katika safari hii walikuwa huru kumtimizia Paulo mahitaji yake, na wageni wengine wangeweza kumwona wakati wo wote waliotaka. Paulo hakupoteza dakika hata moja akifikiri juu ya mateso au shida zilizojuia zikimkabili. Baada ya

MAMBO YA KUKAZA

1. Kabla ya ugeuzi wa Paulo, aliwachukia wale ambao hakupatana nao.
2. Paulo alionyesha upendo wa Kristo kwa wenyeji wa kisiwa cha Melita na kwa wakuu wa Wayahudi mjini Rumi, na kwa wale waliomfanya kufungwa gerezeni.

KULIFUNDISHA SOMO

Je! tulipokutana na Paulo mara ya kwanza, maadui zake walikuwa nani? Walikuwa Wakristo. Alifikiri kwamba walikuwa wakifanya kosa kwa kumwabadu Mungu kwa Yesu Kristo. Baada ya Paulo kugeuka kamili na kuwa Mkristo, alianza kuwa na maadui wengine wapya. Maadui hawa walikuwa wakuu wa Wayahudi ambao walikuwa marafiki zake kabla ya ugeuzi wake. Sasa wakuu hawa walitaka Paulo auawe. Ilionekana kwao kana kwamba Paulo alijiunga na maadui zao.

Ilimbidi Paulo sasa kujibu swali hili moyoni mwake. "Je! niwatende jinsi watu wanaonichukia?" Hili ndilo swali lililombidi Paulo kujibu. Je! ni mtu gani aliyemwekea Paulo mfano wa kufuata? Ni Kristo. Alikuwa mwema kwa wale waliomchukia na kumtesa.

Tunajua kutokana na somo lililopita kwamba Paulo na kila mmoja aliyeikuwa ndani ya merikebu walifika salama katika nchi kavu. Kisiwa kile walichofika kiliitwa Melita. Waambie wanafunzi watafute

kisiwa hiki katika ramani zao. Hali ya hewa ilikuwa baridi na mvua nyingi, na ilikuwa jambo jema sana kwa abiria wale kuona moto ule uliowashwa. Paulo na wengine walisaidia kukusanya mzigo wa kuni wa kuweka motoni.

Paulo alikuwa na ukuni mkononi mwake, na alipouweka motoni, mara nyoka ilitoka ndani yake, ikamzunga-zonga mkononi.



Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 28:4 kuona jambo ambalo watu wale walimfikiria Paulo walipoona nyoka akilewalewa mkononi mwake. Paulo alimtukusha nyoka kutoka mkononi mwake, na hakupata dhara lo lote. Je! watu walimfikiria Paulo nini sasa? Walifikiri kwamba alikuwa Mungu. Je! unafikiri ni nini kilichomzuia Paulo kuumwa na nyoka yule?

Surra ya Pili

KUMPA KRISTO NAFASI YA KWANZA

MASOMO YA BIBLIA: Matendo

9:23-31; 11:20-26; 13:1-3; 14

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Katika mafunzo haya juu ya Paulo, utasoma ya kwamba alikaa katika miji kadha kwa muda. Katika kila mji kulifanyika jambo la kupendeza. Labda wanafunzi wako watataka kutafuta miji hii katika ramani. Hakikisha kwamba umetafuta miji hii katika ramani wakati unapotayarisha somo hili ili uweze kuwasaidia wanafunzi wako.


Katika somo lililopita tulijifunza ya kwamba Paulo aligeuzwa kuwa Mkristo. Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wanafunzi kuelewa ya kwamba Paulo alionyesha ugeuzi wake kuwa ni halisi kwa kujitoa hasa kwa Kristo na kwa kuwasaidia wengine kumpokea Yesu kama Mwokozi wao.

MAMBO YA KUKAZA

1. Kazi ya Paulo ya umisheni inaanza.
2. Mateso yanaenea katika Ikonio.
3. Paulo awatembelea Wakristo wapya.

KULIFUNDISHA SOMO

Paulo, mwamini mpya, alitumia wakati wake wote katika kushiriki habari njema na wengine. Baada ya



kuhubiri kwa muda katika Dameski, viongozi fulani wa dini walipanga kumkamata. Waambie wanafunzi kusoma 2 Wakorintho 11:32-33. Paulo alifahamu mipango yao na alijua kwamba askari walikuwa wakilinda mlango wa mji. Nyakati zile miji mingi ilikuwa na kuta. Kuta nyingine zilikuwa pana zaidi bata nyumba zilijengwa juu yao. Marafiki fulani wa Paulo walimsaidia kutoroka mle mjini kwa kumweka ndani ya kapu kubwa na kumtelemsha katika dirisha la ukutani.

Kisha Paulo alikwenda Yerusalemu. Baadaye Paulo akaenda Kaisaria, mji uliokuwa katika pwani, kutoka pale alingia


merikebuni, akasafiri mpaka Tarso, mji kwa.

Katika wakati ule waamini wengine walikwenda Antiokia wakaanza kuhubiri habari za Bwana Yesu Kristo.

(Tafuta Antiokia katika ramani). Mtu mmoja aliyetwa Barnaba alikuwa mmoja wao. Alijua kwamba alhitaji mtu kumsaidia kwa kazi ya kanisa lile lililokuwa inaendelea. Alimkumbuka Paulo na jinsi aliyompenda Bwana sana. Basi aliondoka akaenda Tarso akamchukua Paulo akaja naye. Yeye na Paulo walifanya kazi Antiokia kwa muda wa mwaka mmoja.

Siku moja Robo Mtakatifu aliwaongoza viongozi wa kanisa kuwatuma Paulo na Barnaba kwenda nchi nyingine kama wamisheni, kuwahubiria watu. Mahali mojawapo ambapo Paulo na Barnaba walikwenda paliwa Ikonio. Katika mji huu, Paulo na Barnaba waliingia sinagogini kwa ushujaa, wakawahubiria watu. Wayahudi wengi na Wayunani waliamini mahubiri yao, wakampokea Kristo kama Mwana wa Mungu na Mwokozi wao. Pia kulikuwapo watu wengi ambao hawakuwaamini na waliotaka waondoke. Waambie wanafunzi kusoma Matendo 14:4-6.

Paulo na Barnaba walikwenda Lистра. Watu wa mji huu (wa Lистра) waliabudu sanamu, na waliamini kwamba waliishi chini wa ulinzi wa miungu waliocitwa Hermie. Paulo alianza kuwahubiria watu hawa, na



akamwona mtu mmoja kiwete aliyependeza sana na maneno Paulo aliyokuwa akisema. Paulo alimwona kiwete huyo kuwa ana imani, basi akamwambia kwa sauti kubwa, "Simama kwa miguu yako." Kiwete huyo alisimama, akaweza kutembea. Huu ulikuwa mwujiza ambao Paulo alifanya. Mungu alikuwa akifanya kazi yake kwa Paulo. Mtu huyu alikuwa kiwete tangu tumboni mwa mamaye, na sasa alikuwa akitembea. Watu walidhania ya kuwa Paulo na Barnaba walikuwa miungu wale wao (yaani Hermie na Zeu), na kwamba walikuwa wamechuka duniani. Walitawalea Paulo na Barnaba sadaka za kutekeleza na taji za mana. (Matendo 14:13) Paulo na Barnaba hawakupenda jambo hili kwa sababu walitaka watu kumwabudu Mungu wa kweli. Walitawambia watu hao, "Sisi nasi tu wanadamu hali moja na ninyi." Walitawambia habari za Mungu wa kweli aliye hai, ambaye alitamba

Mungu alikuwa amemwahidi Paulo ya kwamba angeifika Rumi. Mungu aliahidi kwamba abiria wote waliokuwa ndani ya merikebu wangekuwa salama. Paulo alishawishika kabisa ya kwamba Mungu angetimiza ahadi yake. Mungu hutimiza ahadi yake siku zote.

WAKATI WA KUFUNGA

Katika hadithi hii juu ya Paulo, tunajifunza tena juu ya imani thabiti

aliyokuwa nayo. Tunaona tena jinsi Paulo aliyokuwa Mkristo imara. Alikuwa na ahadi za Mungu na kuziamini. Aliendelea mbele na mipango ambayo alijua kwamba ilikuwa mapenzi ya Bwana. Ahadi za Mungu ni kwele sisi sote.

Funga kwa maombi ili wewe na wanafunzi wako mtakuwa na imani thabiti katika ahadi za Mungu.

Sura ya Kumi na Mbili

JINSI YA KUWATENDEA MAADUI

MASOMO YA BIBLIA: Matendo

28

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Somo hili juu ya Paulo linaonyesha jinsi Paulo aliyokuwa na moyo wa upendo kwa wale waliokuwa maadui zake. Itakuwa muhimu kwako kuwaongoza wanafunzi kufahamu kwamba Kristo aliwapenda watu wote hata wale ambao walimchukia. Kristo aliwaomba wale walimsultisha msalabani. Paulo alionyesha upendo kwa wale waliomfunga gereza ni na ambao hawangeweza kuamini ujumbe wake wa Kristo.

Katika ulimwengu huu wetu wa sasa, kama vijana hawa ndio watakoakuwa viongozi wa kesho, wajifunza upendo wa Kristo kwa watu wote, kisha ulimwengu wote ukawa mahali pema pa kukaa. Zungumza na wanafunzi wako juu ya kuwapenda watu wale wanaowafikiria kwamba wanawachukia. Waruhusu kujadiliana pamoja nawe shida hii.

Kusudi la somo hili ni kuongoza wanafunzi wako kukata shauri kupenda na kuwaomba wale wanaowachukia. Waambie ya kwamba Kristo aliye ndani ya roho zao anaweza kuwajaza mawazo yake ya upendo.

KAZI YA KUFANYA

Paulo alikaa kifungoni kwa muda zaidi ya miaka miwili. Sasa walisafiri kwenda Rumi kuhukumiwa na Kaisaria. Yeye pamoja na wafungwa wengine walikabidhiwa mikononi mwa Yulio aliyekuwa akida wa Kirumi. Paulo alimwambia mwenye merikebu wasisafiri.

Chora mvingo kwa picha ya nanga iliyo mbele ya sentensi ya kweli:

Mwenye merikebu alichagua kutumia wakati wa baridi katika Bandari Nzuri kama Paulo alivyomwambia kufanya.



Ingawa Paulo alionywa kwamba ingekuwa hatari kuendelea na safari, mwenye merikebu alisafiri kwenda Foinike.



Paulo alimwambia mwenye merikebu kuendelea na safari mara tu upepo wa kusini ungeanza kuvuma.

Piga mstari chini ya jibu la kweli la kila swali hapo chini.

Merikebu haikuweza kushindana na upepo. Je! mabaharia walifanya nini?

Walisafiri kwenda nchi kavu.

Waliacha kuchukuliwa na upepo.

Katika kisiwa cha Kanda walipitisha kamba chini ya merikebu ili iishikanishe pamoja. Walipunguzaje uzito wa merikebu?

Walitupa vyombo vya merikebu baharini.

Walitupa nanga nyingine baharini.

Angalia jinsi Paulo alivyoweza mfono mzuri melini. Kata maneno yote yasiyo kweli katika alama hii (): :

Paulo aliwasihi abiria kula (chakula) (~~elawe~~). Walikuwa hawajakula kitu kwa muda wa (~~siku~~ 2) (siku 14).

Paulo alitwaa (mkate) (~~keki~~) akala. Walipokwisha kula wote na kushiba, walitupa (ngano) (~~mizigo~~) baharini ili kupunguza shehena.

Chora mvingo kwa herufi "K" iliyo kando ya sentensi ya kweli na uchope mvingo kwa herufi "M" kando ya sentensi ambayo si kweli.

K M Kulipokucha walitambua nchi waliyotumainia kufika.

K M Mavimbi yalinua merikebu yakaipoleka ukingoni mwa nchi kavu.

K M Kulikuwa na watu wachache ambao hawangeweza kujifikisha nchi kavu salama.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyohidi."

Warumi 4:21

mbingu na nchi na vitu vyote vilivyomo ndani yake.

Maadui wengine wa Paulo walifika Listra kutoka Ikonio. Waliwaambia watu uwongo mwingi juu ya Paulo na Barnaba. Kisha watu wakawaamini watu hawa badala ya kumwamini Paulo na Barnaba. Walimpiga Paulo kwa mawe, wakamburuta nje ya mji, wakamwacha pale wakidhania ya kuwa alikwisha kufa. Paulo alisimama akaingia tena mle mjini, kisha yeye na Barnaba wakaondoka, wakaenda Derbe. Waambie wanafunzi kutafuta miji ya Ikonio, Listra, na Derbe katika ramani.

Katika mji wa Derbe, Paulo na Barnaba walivuta watu wengi sana kwa Kristo. Walikuwa mashujaa kwa sababu baada ya wao kuhubiri Derbe, walirejea Listra na Ikonio kuona jinsi waamini wapya huko walivyokuwa wakendelea.

Walikata shauri kurudi Antiokia, kwa hivyo walipitia mji wa Atalia uliokuwa katika Pwani, wakaabiri kwa merikebu mpaka Antiokia. Wakristo wa Antiokia, ambao waliwatuma katika safari hii ya umisheni, walifurahi kusikia mambo yote Mungu aliyoyafanya pamoja nao. Paulo na Barnaba waliwaambia mambo yote waliyoyafanya, wakitukuza Mungu kwa kuwavuta watu wengi kwa Kristo. Mwambia mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 14:27.

KAZI YA KUFANYA

Soma sentensi zifuatazo, kisha uweke alama hii (X) kando ya jibu sawa la kila sentensi.

1. Barnaba alimwuliza Paulo kuja kufanya kazi naye () Yerusalemu (X) Antiokia.
2. Paulo na Barnaba walingia wapi walipofika Ikonio? () sokoni (X) sinagogini.
3. Ni nani waliompokea Kristo kama Mwokozi wao? () Warumi (X) Wayahudi wengi na Wayunani.
4. Kiwete yule katika Listra aliponywa kwa sababu alikuwa na (X) imani () pesa.
5. Watu wa Listra walifikiri Paulo na Barnaba walikuwa (X) mungu () malaika.
6. Wakati Paulo na Barnaba waliporudi Antiokia, () walijisifu wenyewe (X) walimsifu Mungu.

Jaza nafasi katika sentensi zifuatazo:

1. Marafiki za Paulo walimweka ndani ya kapu wakamtelemba ukutani ili apate kutoroka Dameski.
2. Paulo alirudi Yerusalemu alipotoka Dameski.
3. Mjini kwao Paulo uliitwa Tarsu.
4. Paulo alitaka kushiriki neno la Kristo na wengine.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

Mwenende kama uliyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa; mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu. Wakolosa 1:10

WAKATI WA KUFUNGA

Vakristo hawachoki kuzungunza juu ya mabadiliko ambayo Kristo amekwisha kufanya maishani mwao. Mojawapo ya mabadiliko yale maishani mwa Paulo ni kwamba

Sura ya Tatu

KUIMBA GEREZANI

MASOMO YA BIBLIA: Matendo 16
KUJIANDAA KUFUNDISHA

Furaha ambayo si furaha ya kweii, daiina hutegemea mahali tulipo, watu tulio nao, au kitu tulicho nacho. Furaha ya kweii hupatikana kwa ushirika halisi na Bwana, na hutwezesha kumsifu Mungu hata wakati ambapo mambo ya kidunia yanapokuwa katika hali tusiyoenda. Mfaka mingi sana iliyopita, mtu mmoja alisema ya kwamba utii kamili kwa Bwana huleta furaha halisi. Utaona katika somo hili ya kwamba Paulo alikuwa na furaha kama hiyo.

alikuwa na mawazo mapya juu ya watu, tena alikuwa na tamaa ya kumwona Kristo atikaa maishani mwa watu. Paulo angaliweza kuwa mungu kule Litra kwa sababu Mungu alitumia yeye kumponya kiwete yule. Lakini hakutaka utukufu wa kuwa mungu kwa watu wale. Aliwataka kumjua Mungu mmoja wa kweii. Jambo hilo lilikuwa muhimu sana kwake. Sisi kama Wakristo, ni lazima tuone ya kwamba watu wanamjua Mungu na kumwamini Mwanawe kama Mwokozi wao. Funga darasa kwa maombi.

Watu wengi sana ulimwenguni ni wagonjwa, wengine ni vipofu, na wengine ni vivete. Kuna watu wasio na makao, wala hakuna mtu wa kuwafundisha. Watu wengine hawana chakula. Je! watu kama hao wanaweza kuwa na furaha? Je! furaha inaweza kuwapa kama mambo yanaenda vibaya? Paulo aliyona mambo yote kama yakiinwenda vibaya, lakini katika somo hili tunaona jinsi alivyokuwa na furaha moyoni mwake.

Kusudi la somo hili ni kuonyesha kwamba furaha ya Paulo ya kiroho

hakuna mtu hata mmoja ambaye angearamia. Paulo akaamini abadi hiyo. Alifanya mambo yote ambayo Mungu alimwonyesha kufanya ili kuokoa maisha yake mwenyewe na maisha ya wengine. Aliwazua kutoroka mababarika ambao walihitajiwa sana kuleta merikebu katika nchi kavu.

Malaika wa Bwana alikwisha kumwambia Paulo ya kwamba merikebu yao ingevunjika, na kwamba ingewabidi kuogelea au kushikilia vipande vya mbao vya merikebu yao iliyovunjika ndipo wangeweza kufika katika nchi kavu.

Abiria wale waliokuwamo ndani ya merikebu walikuwa wachafu kwa sababu hawakula wakati wa dhoruba. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 27:33-34 kuona mambo ambayo Paulo aliwambia watu wale. Aliwasili kula. Kisha aliwaa mkate, akamshukuru Mungu mbele yao wote, akaumega, akaanza kula. Ndipo wao wote waliitwa moyo, wakala chakula wenyewe. Watu wote waliokuwa ndani merikebuni walikuwa mia mbili na sabini na sita. Walipokwisha kula wote na kushiba, walipunguza uzio wa merikebu kwa kutupa ngano baharini.

Mambo yalitanyika kama malaika wa Bwana aliyomwambia Paulo. Merikebu iliyunjika na kuangamia, lakini maisha ya kila abiria yaliokolewa. Kulipopambazuka, mababarika waliona kwamba walikuwa karibu na nchi kavu. Waliona hori

yenye ufuo ambapo walipanga kuingiza merikebu yao. Walakini, walifika mahali palipokutana bahari mbili na merikebu yao ikakwana na tezi yake ikavunjiwa na mawimbi. Askari waliokuwa wakiinda wafungwa waliogopa ya kwamba pengene wafungwa wangogelea na kukimbia, kwa hivyo walipanga kuwaua. Kulingana na sheria ya Kirumi, askari ye yote aliyelinda mfungwa kama mfungwa huyo wake alikimbia, yeye ndiye angetukumiwa badala ya mfungwa huyo. Yulio, kwa sababu alitaka kumwoko Paulo aliwazua kutimiza mipango hiyo yao. Aliwaamuru wale ambao wangeweza kuogelea kujitupa baharini na kuogelea kwenda nchi kavu, na wengine kushika mbao na kuelea hadi ufuoni. Bwana alitimiza abadi yake na kila mtu alifika salama katika nchi kavu.



WATU WOTE WAKAPATA
KUFIKA NCHI KAVU SALAMA

Hakuna mtu hata mmoja mle merikebuni aliyekula kwa siku nyingi. Labda hawakuwa na tamaa ya kula kwa sababu ya mawimbi yale yaliyowarusha-rusha. Tena walishughulika sana na kuteka maji mle merikebuni na kumwaga baharini. Ndipo sasa Paulo alianza kuwaambia ya kwamba alikuwa na habari njema ya kuwaarifu. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 27:21-25 na kusema habari hiyo njema.

Paulo alitiwa moyo sana na maneno haya ya Mungu. Alitaka watu wote waliokuwa ndani ya merikebu ile kuamini ujumbe huu wa furaha. Ni kweli kwamba hapakuwapo tumaini lo lote kwao kuokoka. Basi, ingekuwa Paulo kuwaambia kufurahi na kuamini kwamba ingawa merikebu ingeangamia, maisha yao yangeokolewa?

Paulo alimjua Mungu. Alijua kwamba Mungu alipoahidi kitu, alitimiza ahadi hiyo yake hata wakati ambapo ulipodhaniwa kwamba hangeweza kuitimiza. Wakati Bwana aliposema na Paulo, upepo na mawimbi yalikuwa yamepiga-piga merikebu mpaka sasa ilikuwa katikati ya visiwa vya Kauda na Melita. Wasaidie wanafunzi wako kutafuta visiwa hivi. Viko chini ya ramani ya Italia.

Hata usiku wa kumi na nne ulipotimia tangu walipotoka Bandari Nzuri, wakiwa bado wanachukuliwa huku na huko na mawimbi baharini

na mabaharia walidhania kwamba walikuwa wakitaribia nchi kavu. Labda masikio yao yalisikia mawimbi yakipiga-piga ufunoni mwa bahari. Walipima kina cha mahali pale walipokuwapo, wakapata pima ishirini. Palionekana kuwa si mahali pa kina sana. Baadaye kidogo walipima tena na wakapata kina kumi na tano. Ilikuwa usiku na hawakujua kwamba ni kisiwa kipi kilichokuwa mbele yao. Labda merikebu yao ingechukuliwa na mawimbi na kugongwa kwenye miamba iliyokuwa ukingoni mwa bahari wakati wote. Kwa hiyo walitupa nanga baharini kuzuia merikebu isichukuliwe na mawimbi.

Mabaharia walidhania kwamba wangeokoka kama wangekwenda nchi kavu kwa mashua dogo badala ya kukaa ndani ya merikebu. Walijifanya kana kwamba walikuwa wakishusha nanga nyingine baharini, lakini kumbe walikuwa wakishusha mashua dogo ili wapate kutoroka. Hawakujali maisha ya mtu mwingine ye yote ila maisha yao wenyewe.

Paulo alipoona kwamba mabaharia wale walikwisha kushusha mashua yale, alijua kusudi lao la kufanya hivyo. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 27:31 kuona jambo ambalo Paulo alifanya, na some Matendo 27:32 kuona jambo ambalo askari walifanya.

Wakati wote walipokuwa ndani ya merikebu walingojea kupambazuka, Paulo alitumia wakati huo vizuri sana. Mungu alikuwa ameahidi ya kwamba

ilimwezesha kumsifu Bwana hata wakati wa taabu. Omba kwamba tokeo la somo hili vijana watakuwa na tamaa ya kumsifu Bwana wakati wa huzuni na wakati wa furaha.

MAMBO YA KUKAZA

1. Paulo alimtii Bwana kwa kuhubiri Ulaya.
2. Bwana alimpa Paulo uwezo wa kumtoa pepo mchafu aliyekuwa ndani ya kijakazi.
3. Ingawa Paulo na Sila walipigwa na kufungwa gerezeni kwa sababu ya utumishi wao, walimba nyimbo za kumsifu Mungu.
4. Mlinzi wa gereza na jamaa yake yote walimpokea Yesu kama Mwokozi na Bwana.

KULIFUNDISHA SOMO

Uliza: Je! mnakumbuka ni nani aliyesafiri pamoja na Paulo katika safari ya kwanza ya umisheni? (Barnaba) Uliza: Je! unaweza kukumbuka mambo fulani ya furaha ambayo yalimfanyikia Paulo? (Alisamehewa dhambi zake; alichaguliwa kuwa mmisheni wa kwanza wa Mungu kwenda nchi za kigeni; alianzisha makanisa; alifanya miujiza). (Uliza:) Je! unakumbuka mambo fulani ya huzuni ambayo yalimfanyikia Paulo? (Maadui katika Dameski walitaka kumvua; watu wa Ikonio walimchukia; katika Listra alipigwa kwa mawe akaachwa ikidhaniwa kuwa amekufa.)

Sasa tutazungumza juu ya safari ya pili ya Paulo ya umisheni. Katika safari hii Paulo alimchukua mtu mmoja aliyeitwa Sila, akaenda naye. Walianza safari kutoka Antiokia, na badala ya kusafiri kwa mashua, walitembea kwa miguu mpaka kwenye miji ambayo Paulo na Barnaba walikwisha kutembelea.

Katika miji wa Lистра kulikuwa na kijana mmoja ambaye alipendewa na kazi ya Paulo na Sila. Kijana huyu alitiwa Timotheo. Paulo na Sila walimtaja Timotheo kwenda nao na kuwasaidia. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma 2 Timotheo 3:15 katika vifungu vya Biblia. Mwambie mwingine kusoma 2 Timotheo 1:5. Tangu Timotheo alipokuwa mdogo, alikuwa akijifunza maandiko ya Agano la Kale. Nyanya yake na mama yake walimpenda Mungu, na walimfundisha kumpenda Mungu na kumtii. Wakati Timotheo alipomsikia Paulo akieleza ya kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, na Mwokozi aliyeahidiwa, alimwamini Yesu kwa moyo wake wote.


Paulo na Sila na Timotheo walikwenda katika miji mingi ambayo Paulo alikwisha kuhubiri wakati wa safari yake ya kwanza ya umisheni. Waliwatia Wakristo wapya moyo kwendelea kuishi kwa njia impendezayo Bwana.

Wamisheni hawa watatu walikwenda katika nchi ambazo Injili ilikuwa bado kuhubiriwa mbeleni. Walikwenda katika mji mmoja ulioitwa Troa ambao ulikuwa katika

pwani. Hawakujua mahali ambapo Bwana aliwatoka kwenenda baada ya kutoka Troa. Waliomba kwa ajili hiyo, na ilipofika usiku wa manane, Paulo aliona maono. Katika maono hayo alimwona mtu aliyemwambia, "Vuka uje Makedonia utasaidie." (Matendo 16:9) Wanafunzi wako watatufe miji ya Troa na Makedonia katika ramani.

Kabla ya Paulo, Sila, na Timotheo kuondoka Makedonia, msaidizi mmoja mwingine alijiunga pamoja nao, jina lake Luka (yaani Daktari Luka). Luka ndiye aliyandika kitabu cha Matendo. Wote wanne waliabiri kwa mashua mpaka Makedonia. Kisha wakatia nanga katika mji wa Neapoli. Kutoka hapo walicimbea kwa miguu mpaka Filippi ambao ulikuwa mji mkuu wa sehemu ile ya Makedonia. Watu wengi waliokaa Filippi walikuwa Warumi.

Kulikuwa na Wayahudi wachache sana waliokaa Filippi kwa hivyo hapakuwapo sinagogi ambapo wangekwenda kuabudia. Ujiza mmoja wapo wa wanafunzi wako kusoma Matendo 16:13 kuona mahali ambapo Wayahudi waliabudia siku ya sabato. Watu wote walioabudu waliuwa wanawake. Paulo aliwaambia habari za kuja kwa Mwokozi, Yesu Kristo; na wanawake walisikiliza na kuamini. Walikuwa wamekwisha kumwamini Mungu, na waliua manabii walisema ya kwamba Mwokozi angekuja siku moja. Mmoja kati ya wanawake wale alitiwa Lidia. Alimwamini Kristo akabatizwa. Pia aliwakaribisha Paulo



na wenzake kwake nyumbani kukaa naye wakati walipokuwa Filippi.

Kila siku ambapo Paulo na Sila walipokwenda katika mahali pa maombi, kijakazi mmoja alirafuata. Uliza: Je! kuna mmoja anayefahamu maana ya kijakazi? Waambie: Alikuwa amenunuliwa na watu wengine, na alivapatia watu hao faida kwa kuagua. Mambo aliyosema mara nyingi yalikuwa kwele, kwa hivyo watu walimlipa pesa ili awaaguc. Wakati alipokuwa akirafuata Paulo na kundi lake, aliendelea kupiga kelele, akisema, "Watu hawa ni watumishi wa Mungu aliye juu, wenyewe kuwahubiria njia ya wokovu." Ingawa maneno hayo yalikuwa kwele, yaliscemwa na upepo mchafu aliyekuwa ndani ya kijakazi yule. Pepo huyo alikuwa akirazuia watu kumfuata Bwana. Alirafuata Paulo na Sila sana kwa siku nyingi. Mwishowe Paulo alimwambia,

Kutoka Sidoni walisafiri katikati ya Kipro na pwani ya Foinike, kisha wakaelekea upande wa magharibi kupitia pwani ya Kilikia na Pamfilia mpaka wakafika Mira. Je! wanafunzi wanatafuta safari hii katika ramani zao? Katika Mira, Yulio aliwapandisha wafungwa wake katika merikebu iliyotoka Iskanderia kwenenda Italia. Merikebu hii ilikuwa imebeba ngano kutoka Misri. Baada ya kuondoka Mira walisafiri karibu na Nido, na kutoka Nido, merikebu ilipita bahari ya upande wa mashariki ya Krete, ikafika Badari Nzuri. Krete ilikuwa kisiwa na Bandari Nzuri ilikuwa kusini ya kisiwa hiki.

Hatujui ni kwa muda gani merikebu ilikaa katika Bandari Nzuri, lakini "Wakati mwingi" ulikwisha kupita tangu Yulio na wafungwa wake kuondoka Kaisaria. Wakati huu ulikuwa wakati wa hatari sana wa mwaka kwa merikebu ndogo ya mbao kusafiri baharini.

Paulo alikuwa mfungwa wa ajabu. Fikiria mfungwa kuwaonya manahodha wa merikebu ya kwamba ingekuwa hatari kwao kuendelea na safari. Paulo alifanya hivyo. Mwanbie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 27:10. Nahodha wa merikebu hakukubaliana na Paulo. Labda Bwana alikuwa amezungumza na Paulo na kumwonya. Nahodha alijua kwamba Bandari Nzuri hapakuwa mahali pazuri pa kukaa wakati wa baridi. Alitaka kwenenda Foinike. Walikata shauri kwamba

kama wangesafiri karibu na pwani hawangepata shida, tena safari haingewachukua muda mrefu.

Muda mfuji baada ya kuondoka katika Bandari Nzuri, dhoriuba kali ilianza na kupiga-piga merikebu ile ndogo. Ilikuwa vigumu sana kwa mshika usikani kuongoza merikebu. Jambo aliofanya ni kuacha merikebu iendeshe na upepo. Kisiwa cha Kauda ni kama Kilometa 32 kusini magharibi ya Bandari Nzuri. Ni kisiwa kidogo. Waambie wanafunzi watatufe kisiwa hiki katika ramani zao. Kwa kusafiri kandokando ya pwani, merikebu ile iliepuka upepo. Mawimbi yalikuwa juu sana na Merikebu ikaanza kurushwa huku na huku, hata wakaanza kutupa shehena baharini. Siku ya tatu walitupa vyombo vya meli.

Mawingu meusi yalitunika uso wa jua mchana na kufunika nyota usiku na kutanya safari kuwa ya hatari sana. Siku hizi manahodha wana vifaa vya kuwaonyesha mahali hasa walipo baharini. Katika siku zile za Paulo, na kwa miaka mingi sana baadaye, mabaharia walitegemea jua na nyota kuwaongoza. Wakati jua na nyota zilipofunika na mawingu, labda walisafiri katika mahali pa hatari pwani bila kujua mpaka waliposhindwa.

Baada ya kusafiri siku nyingi katika mawimbi makubwa, na bila jua wala nyota, walikata tamaa yao ya kuokoka. Hawakuwa na ufahamu hata kidogo wa mahali pale walipokuwa.

angetimiza ahadi zake kwake bila kujali hatari zilizomkabili na kuchelewa.

MAMBO YA KUKAZA

1. Mungu alitimiza ahadi yake ya kumtuma Paulo Rumi.
2. Malaika wa Bwana alimhakikishia Paulo ya kwamba hakuna mtu hata mmoja ambaye angeangamia baharini.
3. Alifuata ahadi ya Mungu, Paulo aliwasaidia abiria wenzake kujitayarisha kuondoka merikebuni.
4. Ingawa merikebu ilivunjika na kuangamia, watu walisalimika kama Mungu alivyoahidi.

KULIFUNDISHA SOMO


Wengi wetu hutembea wakiwa na fikira za picha zao wenyewe. Picha hizo ni za mambo tunayofikiria kuwa tunafanana nayo sasa, na picha za mambo tunayotumaini kuwa tutafanana nayo wakati tutakapokuwa wakubwa. Je! unajifikiria kuwa katika kazi fulani ya ajabu? Je! umepata kufikiria jinsi ya Mkristo unayotamani kuwa siku fulani?

Jiulize mwenyewe swali hili: "Nawezaje kuwa kama Mungu anavyonitaka?"

Mtume Paulo alikuwa na fikira ya picha yake ambayo haikutegemezwa kwa ahadi ya Mungu mwenyewe. Alikuwa akisafiri kwenda Rumi, mji uliokuwa makao makuu ya ulimwengu wa ustaarabu. Paulo aliendelea kuwa

"Nakuamuru kwa jina la Yesu Kristo, mtoke huyu. Akamtoka saa ile ile." (Matendo 16:18)

Mabwana za kijakazi yule hawangeweza kuwa na tumaini la kupata faida kwake baada ya p-p-o kumtoka. Jambo hili liliwakasirisha sana. Waliwakamata Paulo na Sila wakawapeleka sokoni ambako watawala walikuwako. Waliwaambia watawala hawa ya kwamba Paulo na Sila walikuwa wakichafua sana mji wao kwa kuhubiri dini mpya. "Makutano wote wakaondoka wakawaendea, makadhi wakawavua nguo zao kwa nguvu, wakatoa amri wapigwe kwa bakora." (Matendo 16:23) Baada ya Paulo na Sila kupigwa walifungwa miguu kwa mikatale, wakatupwa gereza katika chumba cha ndani. Mikatale ni vipande vizito vya miti vilivyo na mashimo ya kuingiza miguu.



na taabu. Inaonekana kwamba mambo mengi yalijaribu kumzuia kupeleka ujumbe wa Kristo Rumi. Lakini yeye alimwamini Mungu. Mungu alikuwa amemwambia kwenda Rumi. Kwa hivyo Paulo alishawishika kabisa kwamba angeweza kutimiza ahadi hiyo ambayo Mungu alikuwa ameahidi.

Tunaanza safari ya kwenda Rumi. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 27:1. Kwa kifungu hiki, tunaona ya kwamba Paulo alikuwa bado mfungwa, na akida aliyewasimamia wafungwa alitwa Yulio. Tunadhani kwamba Luka pia alikuwapo katika safari hii kwa sababu neno "tuabiri" limetumiwa. Luka ndiye aliyeandika kitabu cha Matendo, na inawezekana kwamba alikuwapo pamoja na Paulo wakati wa kuhukumiwa na katika safari hii.

Biblia yetu inatwambia kwamba siku ya pili yake, merikebu ilisimama Sidoni. Yulio alionyesha fadhili zake kwa Paulo kwa kumruhusu kwenda kwa marafiki zake.

Paulo na Sila walikuwa wamekuja Filipi kwa sababu Mungu ndiye aliyewaita huko, lakini sasa walikuwa gereza. Ilipofika usiku wa manane, Paulo na Sila walianza kuomba na kumwambia Mungu nyimbo za sifa. Wafungwa wengine waliwasikia wakimba, wakashangaa kwa nini walikuwa na furaha. Walikuwa wanekwisha kupigwa, wakatupwa gereza, na sasa walikuwa wakiimba.

Kulitokea kwa ghafla mtetemeko wa nchi na misingi ya gereza ikatishika zaidi mno hata milango ikafunguka na vifungu vilivyokuwa mikononi na miguuni mwa wafungwa viligezwa. Minzi wa gereza alipoona milango ya gereza ikiwa wazi, alidhania ya kuwa wafungwa wote walikimbia, akataka kujua mwenyewe. Nyakati zile, sheria ya Rumi iliamuru kwamba mfungwa akikimbia, basi minzi wa gereza atauawa kwa ajili yake. Paulo alimwona minzi yule akitaka kujua, akapaaza sauti yake kwa nguvu. Mwambia mwanafunzi mmoja kusoma maneno ambayo Paulo alimwambia minzi yule wa gereza katika Matendo 16:28.

Minzi yule wa gereza alingia ndani ya gereza katika chumba kile ambacho Paulo na Sila walikuwamo, akawaangukia. Alisema, "Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?" Uliza: Paulo alimjibuje? Mwambia mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 16:31. Walimweleza minzi yule wa gereza maana ya kumwamini Bwana Yesu Kristo. Minzi na jamaa yake na

wote waliokuwamo nyumbani mwake, walisikia ujumbe wa Kristo, wakamini wote, wakabatizwa.

Minzi yule wa gereza alionyesha shukrani yake kwa kuosha mapigo ya Paulo na Sila. Pia aliwaandalia chakula, akawapa, wakala. Mbele, hakujali wanafunzi hawa kwamba waliunizwa na kwamba walikuwa na njaa, lakini sasa Kristo akawa moyoni mwake, aliwajalia na kuwatunza.

KAZI YA KUFANYA

Andika herufi hii "X" katika kila mstari ulio kando ya maneno ya kwele.

1. Barnaba alifuatana na Paulo katika safari yake ya pili ya unisheni.

X 2. Timotheo alikuwa kijana aliyemwamini Mungu.

3. Paulo hakumchukua Timotheo.

X 4. Sila alifuatana na Paulo katika safari yake ya pili ya unisheni.

5. Paulo na Sila waliabiri kwa mashua kwenda kwa miji ambayo alikuwa bado hajapata kutembelea.

Piga mstari chini ya neno au maneno ya kwele katika sentensi zifuatazo:

1. (Siku moja) (Usiku) Paulo aliona maono, na katika maono hayo alimwona mtu aliyemwambia avuke aende Makedonia.

2. Watu (walatu) (wanne) walikwenda pamoja na Paulo Makedonia.

3. (Petro) (Mabibu Luka) alikwenda pamoja na Paulo.

4. Wayahudi wa Filipi waliabudu

(ndani ya sinagogi) (kando ya mto).

5. (Lidia) (Marianu) alikuwa mmojawapo wa wanawake wale waliobudu kando ya mto.

6. (Watawala) (Minzi wa gereza) alimwamini Bwana Yesu akawa Mkristo.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Nitamwambia Bwana madamu alinalishi; nitamshangilia Mungu wangu alikiwa hai." Zaburi 104:33

Tutaisihi mara moja tu hapa duniani, na tunapishi, inatupasa daima kumwambia Mungu nyimbo za sifa.

WAKATI WA KUFUNGA

Jei kwa nini Paulo na Sila walikuwa na furaha halisi? (Waruhusu wanafunzi kujadiliana jambo hili.)

Jei sisi pia tunaweza kuwa na furaha kama ile Paulo aliyokuwa nayo? Furaha halisi haitegemei mambo ya kidunia. Ni furaha inayopatikana kwa kujua Mungu na kujua kwamba anatwala maisha yetu. Hebu turudie kusema kifungu chetu cha kukumbuka. Tukumbuke kumsifu Mungu kila siku.

Wambie wanafunzi kufikiri kuma na kukata shauri kama wanastahili kuwa na furaha hiyo halisi inayopatikana kwa kujua Mungu wao binafsi, kama wanamruhusu Mungu kutwala maisha yao, kama wana tamaa ya kufanya jambo lo lote ambalo Mungu anawaambia kufanya. Funga kwa maombi.

kwa kujua kwamba dhambi zao zilisamehewa.

Hebu tusome pamoja kifungu chetu cha kukumbuka, Yakobo 5:20. Paulo alifanya nini ili kujaribu kuokoa roho katika mauti? Aliwasihi watu kumwamini Kristo. Alionyesha kwa matendo yake kwamba aliwajali.

Tutatumia dakika chache katika maombi ya kufikiri. Bila shaka utawajua watu wengi ambao hawajampokea Kristo kuwa Mwokozi wao. Fikiria mmojawapo wa watu hao. Labda ni rafiki yako. Jei

Surra ya Kumi na Moja

KUHAKIKISHA AHADI ZA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Matendo

27

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Kila mwanafunzi darasani mwako anaweza kuwa mtoto wa Mungu mara tu anapomwamini Yesu kuwa Mwokozi wake. Kufanya hivyo humpa nafasi na haki ya kushiriki katika jamaa ya Mungu. Ushirika ambao wanafunzi wako wanao na Baba yao aliye mbinguni huongezeka wakati wanapomfuata Mungu ambaye ni Baba wa upendo, wa kutoa riziki, wa kuongoza, wa kusahihisha, na wa kutia moyo.

unajali ya kwamba rafiki huyu wako ni mwenye dhambi mbele za Mungu kwa sababu hajamtegemea Kristo kumsamehe dhambi zake? Ni kwa jinsi gani unaweza kuwa mwaminifu katika kuwasaidia marafiki zako kujua Kristo? Ni kwa jinsi gani unaweza kuonyesha marafiki zako ya kwamba unawajali?

Waulize wanafunzi kadha kama wangependa kuomba. Wape wakati wa kutosha, kisha ufunge maombi hayo wewe mwenyewe.

Katika hali ya kila siku wanafunzi wako huonyesha kwamba wanamtambua Mungu kama Baba wakati wanapotii Neno lake na kutaka ahadi zake. Kila mwanafunzi anaweza kuona katika maisha yake ya kila siku kwamba ahadi zinaweza kuaminiwa na tena ni za kwele. Omba ili somo hili juu ya kuhakikisha ahadi za Mungu limsaidie kila mwanafunzi kuendelea kumtegemea Baba yake aliye mbinguni ambaye hutunza ahadi zake.

Fanya kusudi la somo hili kuwa la kuonyesha jinsi Paulo alivyoendelea kuwa na matumaini kwa Mungu

SHERIA YA KIRUMI

Hakuna mshitakiwa ye yote ahukumiwaye kabla ya kukutana na washtaki wake uso kwa uso na kupewa nafasi ya kujitefa kuhusu mashtaka aliyofanyiwa.

Piga mstari chini ya sababu ya Festo kumtaka Agripa kumsikia Paulo.

1. Festo alitaka kumhukumu Paulo kufa.
2. Festo alitaka kujua jambo la kumwandikia Kaisari.
3. Festo alitaka kusikia habari za Yesu Kristo.

Tazama picha hiyo hapo chini. Watu hao waliopo pichani walikuwa watu muhimu sana wakati ule wa Paulo.



Je! unafikiri Paulo alifurahi kupata nafasi ya kuzungumza nao? _____

Kwa nini, au kwa nini hakufurahi?

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Jueni ya kuwa yeye amrejezaye mwenye dhambi hata atoke katika njia ya upotevu, ataokoa roho na mauti, na kufunika wingi wa dhambi." Yakobo 5:20

Mwenye dhambi akitubu dhambi zake kwa Mungu kwa njia ya Kristo, roho yake itaokolewa na atakuwa na uzima wa milele kama Kristo aliyoahidi. Dhambi zote, hata kama ni ngapi, zitasamehewa.

WAKATI WA KUFUNGA

Festo na Mfalme Agripa waliridhika kukaa bila kumjua Kristo, wakamdhihaki Paulo kwa tamaa yake ya kuzungumza habari za Bwana. Je! ni kwa nini Paulo alihusika na watu hawa? (Wape wanafunzi wakati wajadiliane jambo hili.)

Hebu tusome pamoja Yohana 3:36. Maana ya kifungu hiki ni kwamba mtu anayemwamini Kristo kweli kama Mwokozi wake ana uzima wa milele. Mtu asiyemwamini Kristo hawezi kuwa na uzima wa milele, bali hasira ya Mungu inamkalia.

Kwa sababu Paulo alijua ya kwamba watu waliomwamini Kristo hawana uzima wa milele, mara kwa mara alitaka kuwasaidia. Alihusika nao hasa. Aliwataka kuwa na furaha

Sura ya Nne

PAULO AHUBIRI ATHENE

MASOMO YA BIBLIA: Matendo 17:16-34

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wanafunzi darasani mwako hujiunza kujifikiria mambo mengi, lakini wanahitaji kuongozwa na mtu mkubwa ili waweze kuwa na fikira na mawazo mema. Somo hili linatueleza habari jinsi Paulo alivyowafundisha watu wa Athene Injili ya Kristo. Wasaidie wanafunzi kuona mawazo mabaya ya watu wa Athene, na pia kuona jinsi Paulo alivyowaambia ukweli wa Mungu. Wasaidie wanafunzi kukata shauri kushiriki injili na wengine, na kuacha matokeo ya kushiriki kwao mikononi mwa Mungu.

Kusudi la somo hili ni kuonyesha ya kwamba kuwa watu wa dini pekee yake hakutoshi. Ni lazima kumkiri Yesu Kristo kama Mwokozi wako.

MAMBO YA KUKAZA

1. Paulo aliwaona watu wa Athene kuwa wenye dini, lakini hawakumjua Mungu wa kweli aliye hai.
2. Watu wenye ujuzi walimpeleka Paulo Areopago kusikiliza mafundisho yake.
3. Katika kusema na watu hawa, Paulo alijaribu kuwaonyesha kwamba wazo lao la kuabudu miungu wengi lilikuwa kosa, na kwamba ilikuwa

lazima wamwamini Mungu wa kweli aliye hai ili wanguweza kupata wokovu.

4. Ni watu wachache tu kati ya wale waliomsikia Paulo ndio waliomwamini Yesu.

KULIFUNDISHA SOMO

Waulize wanafunzi wako swali hili: Je! nitafanya nini watu wakikataa kusikiliza nikiwaambia habari za Kristo?

(Labda wewe kama mwalimu, umekwisha kujaribu kushiriki imani yako na mtu mwingine ambaye alikataa kusikiliza. Ikiwa umekwisha kuona jambo hili, uwaambie wanafunzi wako juu yake. Labda wao pia watakwambia jambo hili.)

Tunakumbuka ya kwamba Paulo, mmisheni wetu, alikuwa amekwisha kutembelea miji mingi kushiriki Habari Njema ya Mungu. Katika mahali pengi, ni watu wachache tu ndio waliomsikiliza alipowaambia habari za Kristo, na wengine wakaamini. Tunajua ya kwamba watu wengine hawakumsikiliza, na kwamba Wayahudi wengine waliokasirika, waliwakamata Paulo na Sila na kuwaweka gerezani Filipi. Baada ya Paulo na Sila kufunguliwa gerezani, Timotheo alijunga nao. Wote watatu walikwenda Thesalonike na Beroia. Waambie wanafunzi kutafuta miji hii miwili katika ramani.

Watu wengi katika miji hii walisitiliza injili ya Kristo, wakamwamini kama Mwokozi. Pia kuikuwapo watu wengine ambao hawakutaka kusitiliza injili, watu hawa walimfanya Paulo kuondoka Beroia. Timotheo na Sila wakabaki Beroia.

Paulo alikwenda Athene, mji mkuu wa Uyunani. Wasaidie wanafunzi kupata mji huu katika ramani. Mwanbia mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 17:15-16. Hebu tujifanye kama kwamba tuko Athene pamoja na Paulo, na kwamba tunatembea naye mji. Po pote tuendapo tunaona madhabu na sanamu ambazo Wayunani wanatumia katika ibada yao. Majengo mazuri kuliko mengine yote miji ni mahkalu ya mungu. Tunasimama na kuangalia mungu hao waliotengenezwa kwa dhahabu, kwa fedha, na kwa jiwu. Mungu hawa hawana uhai. Tunaweza kuwagusa. Hawawezi kujongea kwa maana wao ni sanamu tu zilizotengenezwa na wanadamu. Zinaka ndani ya hekulu zilizojengwa.

Tunaposema na watu hawa wa Athene tunaona kwamba wanaamini ya kuwa mungu hawa wanatawala sehemu mbalimbali za ulimwengu. Wanatawambia ya kwamba "Neptune" anatawala bahari, maziwa na miti, "Jupiter" anatawala mbingu, na "Athene, mungu wa kike" anatawala mji wa Athene.

Kisha tunaona madhabu iliyoandikwa, "KWA MUNGU

ASIVEULIKANA." Watu wa Athene wanaogopa ya kuwa pengene hawamwabudu Mungu wa kwele, kwa hivyo wamejenga madhabu hii kwa mungu wasijemua.

Paul anakasirika, watu hawa hawamui Mungu wa kwele aliyebai. Paulo alikata shauri ya kwamba ni lazima kuwambia watu hawa habari za Mungu na Kristo. Waambi wanafunzi kusoma Matendo 17:17 wapate kuona jambo ambalo Paulo alifanya. Tutamfata Paulo mpaka sokoni. Huko sokoni watu hawawadi kwa shughuli ya kuza na kumama bidhaa peke yake, wanakwenda pia kuzungunza juu ya shughuli zilizote kama sasa na ya dini. Paulo anasema na watu hawa. Wamekati yao ni watu wenyewe ujuzi. Wana tamaa kusikia mawazo mabaya, kwa hivyo wanayamaza kinywa kumwambia Paulo. Mwanbia mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 17:18, ili wawazi wote wapate kuona jinsi watu hawa walivyomfikiria Paulo na wote wake.

Watu wengine waliposikia habari za Yesu na ufufuo wake, walifikiri kwamba Paulo alijua habari za Mungu fulani mgani kwake, na walitaka kusikia mengi kutoka kwake. Walimpeleka Paulo mpaka Areopago, na wao walakaji juu ya mawe yaliyokuwa hapo. Paulo alitaka kuwawezesha kwamba wawazi na kosa kuibudu mungu hawa na sanamu zilizojengwa. Pia alitaka kuwasikia kumjua Mungu wa kwele na kusamehewa dhambi zao.

kuelekea nuru na kuwafanya waache nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu.

Paulo alitii mwito wa Mwokozi katika maono. Kwanza, aliwahubiria watu wake kisha akawahubiria watu wa Mataifa.

Paulo alisema ya kwamba hakusema jambo lo lote tofauti isipokuwa yale yaliyonenwa na manabii. Je! ni ukweli upi muhimu ambao Paulo aliwambia watu wote? Mwanbia mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 26:23.

Kwa sababu Festo alikuwa Mrumi, hakuweza kuelewa mengi ambayo Paulo aliyasema. Je! Festo alifikiri nini wakati Paulo alipokuwa akiitoa ushahidi wake? Soma Matendo 26:24. Festo liwali alifikiri Paulo alikuwa na wazimu wakati Paulo aliposema juu ya ufufuo wa Kristo katika wafu. Alifikiri ya kwamba Paulo alikuwa anasoma sana.

Ingawa Festo hakujua habari za manabii, Mfalme Agripa alikuwa anajua. Alikwisha kusikia unabii wa Kristo maishani mwake mwote. Paulo alimwiliiza kama aliwaamini manabii. Kisha Paulo alijibu swali hilo yeye mwenyewe kwa kusema, "Najua ya kuwa wawaamini." Mfalme Agripa alimwambia Paulo, "Kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo?" Paulo alimjibu, "Namwomba Mungu kwamba, ikiwa kwa machache au ikiwa kwa mengi, si wewe tu ila na hao wote wanaonisia leo wawe kama mimi, isipokuwa vifungo hivi." (Matendo 26:29)

Wakati Paulo alipomaliza kusema, mfalme, liwali, Bernike na wakuu wengine, wote walitoka nje kusemezana juu ya kesi ile. Walikubaliana ya kwamba Paulo hakutenda neno lo lote lililostahili kifo wala kufungwa. Ingawa hakuwa na hatia, ile rufani aliyotaka kwa Kaisari haingeweza kubadilishwa.

Maombi ya Paulo yalikuwa yakijiibiwa na bwana. Alikuwa akienda Rumi, na alijua ya kwamba ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kwake kwenda Rumi.

KAZI YA KUFANYA

Mfalme Agripa na Bernike, dada yake, walikujia Kaisaria ambako mtume Paulo alikuwa mfungwa. Chora mwingo kwa herufi "K" iliyo kado ya sentensi iliyo ya kwele, na uchope mwingo kwa herufi "M" iliyo kando ya sentensi ambayo si kwele.

K. M Mfalme Agripa na Bernike walikujia kumkaribisha Festo.


K. M Festo liwali alimwambia mfalme ya kwamba Paulo alikuwa na hatia.

K. M Viongozi wa Kiyahudi walitaka Paulo ahukumiwe.

Festo alimkumbusha Agripa sheria ya Kirumi. Kamlisha mambo aliyomwambia Agripa katika sentensi ifuatayo hapo chini:

siyo hatia. Nilimwuliza Paulo kama alitaka kwenda Yerusalemu kuhukumiwa huko, lakini yeye alitaka rufani kwa mfalme Kaisari Augusto."

Baada ya Agripa kumsikiliza Festo akimsimulia maneno juu ya Paulo, alimwambia Festo ya kwamba alitaka kumsikia Paulo yeye mwenyewe. Festo alimwahidi kwamba angemsikia Paulo keshowe. Festo alimtaka sana Agripa kusikia maneno ya Paulo. Hakuna na jambo lo lote kanuni la kumwandikia mfalme juu ya Paulo mfungwa wake. Halikuwa jambo la busara kumpeleka mfungwa kwa mfalme bila kumwandikia hatia yake. Festo liwali alitumaini ya kwamba kwa kumwuliza-uliza Paulo maswali, angepata jambo la kumwandikia mfalme.



Keshowe, Paulo aliletwa mbele ya wakuu waheshimiwa - yaani, mbele ya mfalme, malkia liwali, wakuu wa vita, na watu wengine muhimu. Waulize vijana kama wanafikiri ya kwamba Paulo alifurahi kuzungumza na watu


hawa muhimu. Ngojca ili wanafunzi watoe jibu.

Paulo alianza maneno yake kwa kumwambia Agripa ya kwamba alikuwa na furaha kujitetea yeye mwenyewe mbele ya mtu (yaani mbele ya mfalme Agripa mwenyewe) ambaye alijua desturi za Kiyahudi. Paulo alikuwa amekwisha kuwasimulia Feliki na Festo maneno hayo yake, lakini wao walikuwa Warumi na hawakufahamu vizuri dini ya Wayahudi. Mfalme Agripa alikuwa Myahudi kama yeye, tena alijua vyema sheria za Kiyahudi na desturi zao.

Paulo alieleza jinsi alipokuwa kijana aliwachukia Wakristo. Alieleza jinsi alivyofikiri kwamba alikuwa akifanya kazi njema kwa kuwatesa Wakristo na kujaribu kuwalazimisha kumlaani Kristo. Alifikiri kwa hakika ya kwamba kadiri angezidi kuwatesa waamini wa Yesu, ndiyo angezidi kupendeza Mungu, lakini fikira hii yake ilikuwa upuzi tu.

Paulo alimwambia Mfalme Agripa juu ya ugeuzi wake alipokuwa njiani kwenda Dameski. Waulize wanafunzi wakueleze habari za ugeuzi wa Paulo. Habari hizo zilikuwa katika somo la kwanza juu ya Paulo. Jaribu kuona jinsi wanavyoweza kuzikumbuka vyema.

Pia Paulo alimwandikia Mfalme Agripa ya kwamba Bwana alimwambia kufumbua macho ya Wayahudi na watu wa Mataifa waliokuwa vipofu katika macho ya kiroho, kuwageuza waiache giza



Paulo alianzaje mahubiri yake? Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 17:22-23. Paulo alianza mahubiri yake kwa kuwasifu watu hawa. Alisema, "Katika mambo yote naona ya kuwa ninyi ni watu wa kutafakari sana mambo ya dini." (Matendo 17:22b) Uliza: Kwa nini unafikiri Paulo alimtaja mungu asiyejulikana? (Tumia wakati katika kuzungumza.)

Ingawa watu wa Athene waliabudu miungu wengi, hawakumjua Mungu pekee wa kweli, Mungu aliyewaumba na kuwatumia Mwanawe kuwaokoa katika dhambi zao. Paulo aliwambia hakuja kuwaeleza habari za mungu mgeni, kama alivyotumainia, bali alikuja kuwambia habari za Mungu ambaye walikuwa waktjaribu kumwabudu bila kumjua. Aliwambia ya kwamba Mungu ambaye yeye alimwabudu ndiye Bwana wa mbingu

na nchi, na ndiye Mtawala wa vitu vyote.

Paulo aliwambia watu hawa ya kwamba Mungu wa kweli na aliye hai hakai ndani ya mahekalu yaliyojengwa kwa mikono ya wanadamu, bali anakaa ndani ya roho ya kila mmoja wetu. Alisema Mungu "hawi mbali na kila mmoja wetu." (Matendo 17:27.) Waambie wanafunzi wako kufungua Biblia zao katika Warumi 10:9-15.)

Uliza: Je! tunawajua watu wengine katika nchi hii wanaohitaji kumjua Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao?

Je! unaelewa ni kiasi gani unahitaji kumjua Yesu kama Bwana na Mwokozi wako?

KAZI YA KUFANYA

Soma sentensi zifuatazo kisha uweke alama hii (X) katika kila mstari ulio kando ya sentensi ya kweli.


 X 1. Paulo aliudhika alipoona mji wote wa Athene ukijaa sanamu au miungu wa uongo.

 X 2. Paulo alizungumza na Wayahudi ndani ya jengo la sinagogi ambalo Wayahudi walijenga kama mahali pao pa kuabudia.

 X 3. Kila siku Paulo alizunguza habari za Yesu sokoni na wale aliokutana nao.

Je! ni maneno yapi mageni ambayo Paulo aliona madhabahu iliyokuwa pale mji? Andika

maneno hayo chini ya picha ya madhabahu.



KWA MUNGU ASIYE- JULIKANA

Soma katika Matendo 17:24-26 mambo ambayo Paulo aliwaambia watu wa Athene juu ya Mungu. Sasa chora msitari kutoka kwa kila sentensi hapo chini hadi kwa neno linaloikamilisha.

Mungu aliumba
M u n g u n i nchi
Bwana wa mbingu ulimwengu na
Mungu hakai watu wote
ndani ya mikono ya
M u n g u wanadamu
hatumikiwi kwa h e k a l u
Kutoa kwa mtu
mmoja Mungu
alifanya taifa la

Soma matendo 17:32-34 uone jinsi watu mbalimbali walivyofikiria ujumbe wa Paulo. Chini ya kila picha andika namba ya kifungu cha Biblia kinacleza habari yake.



Kifungu cha 32:



Kifungu cha 34:



Kifungu cha 32:

Surra ya Kumi

KUMSHUHUDIA KRISTO

MASOMO YA BIBLIA: Matendo 25:13-27, Matendo 26:1-32

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Katika somo hili utataka vijana wako kuona mambo ambayo Paulo aliyaoona na kuwaza mambo Paulo aliwaza. Wakifanya hivyo ndipo watakuwa na tamaa ile kuu ya Paulo ya kuwataka wengine kujitunga na jamaa ya Mungu. Waongoze wanafunzi wako kuona ya kwamba Paulo alitumia kila nafasi kumshuhudia Kristo. Kusudi la somo hili ni kutia wanafunzi wako moyo kuwasaidia wengine kumpokea Kristo kama Mwokozi wao. Paulo, kwa uaminifu mkuu alitumia kila nafasi kushuhudia mambo ambayo Bwana Yesu aliyefufuka katika wafu alimfanyia, na kuwasihii wengine kumpokea Yesu kama Mwokozi wao. Paulo aliwashuhudia watu wote watu wa kawaida na wengine yeye. Katika somo hili tunajifunza jinsi aliyowashuhudia watu muhimu.

MAMBO YA KUKAZA

1. Paulo hakujitetea tu mbele ya Mfalme Agripa na wengine, bali alivakaribisha pia kuwa Wakristo.
2. Inatupasa kushirikiana na Paulo ya kuwahubiria wengine wokovu wa Kristo.
3. Mungu alikuwa akimtararishia Paulo njia ya kwenda Rumi.

KULIFUNDISHA SOMO

Katika kuendelea na somo letu lililopita, tutakumbuka ya kwamba Paulo alikuwa mfungwa bado katika Kaisaria. Alitaka rufani kwa Kaisari mjini Rumi kuhukumu kesi yake.

Festo liwali alikuwa na mgeni msheshimiwa. Je! ni nani aliyekuja Kaisaria kumtembelea Festo? Mwanafunzi anaweza kusoma Matendo 25:13 na kutupa jibu hili. Ndiyo, walikuwa Agripa mfalme wa Kiyahudi na Bernike dayeye. Kama mfalme katika Uyahudi (Palestina), Agripa alikuwa na mamlaa katika serikali ya Warumi kama Festo liwali alivyokuwa. Ilikuwa jambo la kawaida kwa watawala hawa wawili kuzungumza habari za serikali ya Warumi na shida zao.

Je! ni kesi ipi hasa ambayo Festo alimwambia mfalme Agripa? Ndiyo, alimwambia kesi ya Paulo aliyekuwa mfungwa wake. Je! Festo alimkumbusha Agripa jambo gani kuhusu sheria ya Warumi? Mwanambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 25:16.

Hapa kuna maneno ambayo Festo alimsimulia Agripa. "Muda mfupi baada ya mimi kuwa liwali, makuhani wakuu na wakuu wa Wayahudi waliniomba kumhukumu Paulo kufa. Na wakati wa hukumu nilistajabu kuwasikia Wayahudi wakimshtaki Paulo kwa tofauti za kidini tu wala

1. Jemadari aligopa kwamba Paulo angefanywaje? Angeraruliwa.

2. Wakati Paulo alipokuwa ngomeni ni nani aliyemtia moyo usiku? Bwana.

3. Wayahudi wale arobaini wenye hasira walipanga kufanya nini? Kumwua Paulo.

4. Ni nani aliyesikia mpango huo wao na kwenda kumwona Paulo? Mtoto wa dada ya Paulo.

5. Jemadari aliamua kumpeleka Paulo, Kaisaria. Je! alimpeleka kwa nani? Feliki liwali.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Hata twathubutu kusema, Bwana ndiye anisaidiye, sitaogopa; mwanadamu atanitenda nini?" Waraka kwa Waebrania 13:6

Katika hadithi ya Marie Monsen na ya Paulo, tunajifunza kwamba watu hawa walikuwa na imani kuu katika Bwana, na katika kuwasaidia na kuwalinda. Ikiwa wanafunzi wako wanaweza kuwa na imani hii katika Bwana, watakuwa na maisha ya furaha bila wasiwasi. Lakini hii si kusema kwamba havatakuwa na shida. Maana yake hasa ni kwamba Mungu atawaongoza katika njia yo yote watakayomhitaji.

WAKATI WA KUFUNGA

Kama mwanafunzi akiuliza swali hili, "Je! naweza kuwa na hakika kwamba Mungu atakuwa karibu nami

wakati nitakapomhitaji?" Wewe utamjibuje? Somo hili juu ya Paulo ni swali zuri sana. Watie wanafunzi wako moyo kuomba kuwa na imani thabiti katika Mungu. Wakiwa na imani thabiti watajua kwamba Mungu yuko karibu nao daima. Waulize wanafunzi wako swali hili: Je! mnaweza kuwa na hakika kwamba Mungu atakuwa karibu nanyi wakati mtakapomhitaji? (Wape muda wa kujibu.)

Funga kwa maombi ili kila mmoja wao watakuwa na imani thabiti.

Klaudio Lisia kwa liwali mtukufu Feliki, Salamu! Mtu huyu alikamatwa na Wayahudi wakawa karibu kumwua, ndipo nikaenda pamoja na kikosi cha askari nikamwkoa, nilipopata habari ya kuwa yeye ni Mrumi. Nami nikitaka kulijua life neno waliomshitakia, nikamtelemsha nikamweka mbele ya baraza; nikaona kwamba ameshitakiwa kwa ajili ya maswali ya sheria yao, wala hakushitakiwa neno lo lote la kustahili kuuawa wala kufungwa. Hata nilipopewa habari kwamba patakuwa na yitimvi juu ya mtu huyu, mara nikampeleka kwako, nikawaagiza wale waliomshitaki, wanene habari zake mbele yako. Wasalamu. Matendo 23:26-30

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Amin, amin, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa millele; wala haingii hukumuni bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani." Yohana 5:24

Katika kuwaeleza wanafunzi wako kifungu cha kukumbuka, unaweza kusema ya kwamba Yesu ndiye aliyewaambia watu maneno haya ya upendo wa Mungu. Aliwaambia ya kwamba kama wangepapokea maneno haya miyoni mwao, na kumwamini Mungu, wangerithi uzima wa millele.

Sura ya Tano

USIOGOPE

MASOMO YA BIBLIA: Matendo

18:1-22

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Je! umepata kuogopa? Unafikiri wanafunzi walioko darasani mwako wanaogopa? Ndiyo, wanaogopa. Pengine wanaogopa giza au kuzungumza mbele ya darasa, au pengine wanaogopa ugonjwa au mauti. Vijana wengi wa rika lenu hawataki kusema kwamba wanaogopa kitu cho chote. Walikuwa katika umri huu, wanaogopa mambo mengi.

Kwa kujifunza somo hili, utaona ya kwamba Paulo alikuwa na sababu ya kuogopa. Siku moja usiku katika maono, Bwana alisema na Paulo akamwambia asiogope kwa sababu angekuwa pamoja naye.

Kabla ya kufundisha somo hili, zungumza na wanafunzi wako juu ya woga. Ni jambo la muhimu sana kwa wanafunzi wako kujua ya kwamba Mungu yupo pamoja nao. Atawapa ushujaa wa kufanya mambo ambayo wanaogopa kufanya. Ni lazima wazungumze na Mungu juu ya woga

WAKATI WA KUFUNGA

Tumejifunza katika somo hili ya kwamba Paulo aliwaambia watu waioabudu miungu mingi habari za Mungu mmoja wa kweli. Wengine kati ya watu hao walianza kumwamini Mungu, wakajifunza kumpenda Kristo kama Mwokozi wao. Pengine baadhi ya wanafunzi wako hawamjui Yesu Kristo kuwa ndiye Mwokozi wao. Pengine hawaelewi jinsi ilivyo muhimu kufanya hivyo. Funga kwa maombi ili kwamba wanafunzi wako wote watamjua Kristo kuwa ndiye Bwana na Mwokozi wao.

wao na kumwomba kuwasaidia. Wakimwomba hivyo, atawasaidia. Labda wewe kama mwalimu, unaweza kujua woga wao. Ni lazima wajifunze kwamba hawapaswi kuishi kwa woga, bali wawe na ushujaa. Mungu atawapa ushujaa wanaotaka. Sisi sote tunapaswa kumwamini Bwana kutusaidia kushinda woga wetu. Wanafunzi wakitaka kuzungumza juu ya woga wao, uwaruhusu kutanya hivyo na uwasikilize. Pengine unaweza kuwasidia kuwa na nia ya kushinda woga wao kwa kumwamini Bwana. Kusudi letu leo ni kuonyesha kwamba Mungu atatusaidia wakati tunapogopa.

MAMBO YA KUKAZA

1. Paulo alihubiri nyumbani mwa Yusto baada ya Wayahudi wasioamini waliokuwa sinagogini kukataa Injili.
2. Bwana alimwamuru Paulo katika maono kushuhudia kwa ushujaa, akaahidi kuwa pamoja naye.
3. Paulo alipoendelea kuhubiri katika Korintho, Wayahudi walimkamata na kumpeleka mbele ya liwali wa Kirumi kuhukumiwa.
4. Mungu alichagua kumlinda Paulo kudhuriwa.

KULIFUNDISHA SOMO


Katika somo lililopita tulimwacha Paulo Athene. Katika somo hili tutajifunza juu ya wakati wa Paulo kuwako katika Korintho. Wakati tunapojifunza somo hili, hebu

tufikirie nyakati ambazo Paulo angekuwa na sababu za kuogopa. Kisha tutatafuta jibu la swali hili: Naweza je kushinda woga wangu?

Jei Paulo alipata marafiki Korintho? Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 18:2. Akila na Prisila, mkewe, walikuwa wakika Rumi. Iliwabidi kuondoka huko kwa sababu Wayahudi wote waiamriwa kutoka Rumi. Kwa hivyo walikuja kukaa Korintho.

Wakati Paulo alipokwenda Korintho walikwenda nyumbani mwa marafiki zake wawili kukaa pamoja nao. Walikuwa na kazi kama ya Paulo. Jei kazi hiyo ilikuwa nini? Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 18:3.

Kila kijana wa Kiyahudi aliyetoka katika jamaa maskini au tajiri, alifundishwa kazi. Paulo alifundishwa ushonaji hema. Walishona hema kwa ngozi ya mbizi.



waliokuwa na hasira nyingi. Walimrudisha Paulo ngomeni.

Siku ya pili yake, Bwana alisimama karibu na Paulo. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma mambo ambayo Bwana alimwambia Paulo katika Matendo 23:11. Bwana alikuwa akimtia Paulo moyo kwa sababu pengine alijua kwamba Paulo alikuwa na wasiwasi juu ya mambo ambayo yangempata.

Kulipopambazuka, Wayahudi walifanya mapatano, wakajifunga kwa kiapo kwamba hawangekula kitu cho chote wala kunywa mpaka wamwue Paulo. Wayahudi hao waliopiana walikuwa arobaini. Walikwenda kwa waku na makuhani na wazee, wakawapasha habari juu ya kujifunga kwao kwa kiapo. Waliwaomba waku hao wa makuhani na wazee kuwasaidia katika mpango huu wao kwa kumwambia jemadari amlete tena Paulo mbele ya baraza. Walisema wangemwua Paulo kabla hajakaribia baraza.

Mtoto wa dada ya Paulo alisikia habari juu ya mpango huu akaenda ngomeni kumwarifu Paulo. Halafu Paulo alimwita askari mmoja akamwambia kumchukua mtoto yule kwa jemadari ili kumwarifu juu ya mpango ule wa Wayahudi arobaini. Baada ya mtoto yule kumwarifu jemadari juu ya mpango ule, jemadari alimwagiza asimwambie mtu ye yote kwamba alimwarifu juu ya mpango ule.

Jemadari aliona kwamba haikuwa salama kwa mfungwa wake (Paulo)

kubaki Yerusalemu. Alikata shauri kumpeleka Kaisaria kwa liwali Feliki. Alikata shauri kumwondoa Paulo usiku ule ule. Kwa ajili ya ulinzi na usalama, aliwaamuru askari mia mbili, na askari wapanda farasi sabini, na wenye mikuki mia mbili kumchukua Paulo na kumpeleka Kaisaria. Jemadari hakutaka jambo lo lote baya kumpata mfungwa huyu Paulo ambaye alikuwa raia wa Rumi. Pia, aliandika barua kwa liwali Feliki. Barua hii imeandikwa katika Matendo 23:25-30. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma.

Askari wa miguu walimchukua Paulo mpaka kwa Antipatri usiku ule. Siku ya pili yake asubuhi walirudi zao ngomeni, na askari wale wapanda farasi wakamchukua Paulo na kumpeleka Kaisaria. Walimpa liwali barua ile walipopewa na jemadari, wakamweta Paulo mbele yake. Liwali alimwambia Paulo ya kwamba angesika kesi yake wakati washaki wangewasili kutoka Yerusalemu.

KAZI YA KUFANYA

Katika baraza kulikuwa na makundi mawili, Mafarisayo na Masadukayo. Makundi haya yalitofautiana katika imani yao. Paulo alikuwa Farisayo. Baada ya muda usio mrefu, makundi haya mawili walingia katika mabishano makali juu ya Paulo. Mafarisayo walisema, "Hatuoni uovu wo wote katika mtu huyu." Jaza nafasi zilizoachwa katika sentensi zifuatazo:

Katika somo hili tutajifunza kwamba Paulo aliamini ahadi za kumlinda. Hakumwogopa mwanadamu.

Jemadari hakujiunza sababu iliyowafanya Wayahudi wale wenye hasira kutaka Paulo auawe. Siku ya pili yake alimpeleka Paulo mbele ya baraza. Watu sabini wa baraza hilo walikuwa wazee ambao ndio waliokuwa wakuu wa Israeli. Baraza hili lilikuwa kama mahakama zetu za sasa. Lilikutana kuhukumu wale waliodanganya watu au wale waliofundisha mambo kinyume cha sheria ya Kiyahudi. Katika wakati ule wa Paulo, kuhani mkuu ndiye aliyetawala baraza la Kiyahudi kama vile majaji wanavyotawala mahakama zetu za sasa.

Je! ni jambo lipi la kwanza ambalo Paulo aliliambia baraza? Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 23:1. Baada ya Paulo kusema maneno haya, kuhani mkuu alimwamuru mtu aliyekuwa akisimama karibu naye kumpiga mdomo. Labda kuhani mkuu alikuwa amekasirika sana na Paulo kwa sababu alijiona kuwa na hatia kwa sababu maisha yake hayakuwa mema na hakutubu dhambi zake kwa Mungu. Kisha Paulo alikasirika sana. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 23:3. Paulo alijua kwamba hakufanya lo lote baya la kumfanya kuadhibiwa.

Paulo alijua wazi kwamba hangehukumiwa na baraza lile kulingana na sheria. Alifikiria njia

nyingine ya kumfanya kushinda kesi yake. Aliona njia ambayo kwayo angeweza kuwafanya Mafarisayo kuwa upande wake. Baraza lile lilikuwa la Mafarisayo na Masadukayo, na makundi haya mawili hawakupatana sikuzote. Paulo alijivunia kuwa Farisayo kabla ya kukutana na Kristo. Alikata shauri kuleta mashindano kati ya Mafarisayo hawa na Masadukayo juu ya ufufuo wa wafu. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 23:8. Mafarisayo walisimama upande wa Paulo wakati alipoliambia baraza kwamba alikamatwa na kufungwa gerezeni kwa sababu ya kuamini kwake kwamba kuna ufufuo wa wafu.

Wakati Paulo aliposema ya kwamba aliamini ufufuo wa watu, alikuwa na maana kwamba alikamatwa na kufungwa gerezeni kwa sababu ya kuwa Mkristo. Mojawapo ya kweli za maana ambazo Mkristo anaamini ni kwamba Kristo alifuka katika wafu na sasa ankaa mbinguni. Sisi Wakristo tunajua ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu anayetupa uzima wa milele kwa maana yu hai.

Baada ya Paulo kusema kwamba aliamini ufufuo wa wafu, je! Mafarisayo walisema nini? Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 23:9. Kisha palitokea ugomvi mkubwa na jemadari akaamuru askari kushuka na kumwondoa Paulo. Yeye ndiye aliyekuwa na mamlaka juu ya Paulo na alilogopa ya kwamba pengine Paulo angeraruliwa na watu

Je! unaweza kustajabu kwa nini Paulo alitumia wakati katika kushona hema na hali kazi yake muhimu ilikuwa kuhubiri Injili? Paulo alikuwa na nia ya kujitegemea mwenyewe badala ya kutegemea makanisa. Tunaweza kuwa na hakika ya kwamba wakati Paulo alipokuwa akifanya kazi ya kushona hema, alitumia kila nafasi aliyokuwa nayo kuwaambia washonaji wenzake na wanunzi habari za Mwokozi wake.

Siku ya sabato ilipofika, Wayahudi wengi walikwenda sinagogini kumwabudu Mungu. Paulo pia alikwenda. Alitaka kuwaambia watu ya kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zao. Yeye mwenyewe alikuwa Myahudi na alitaka sana Wayahudi hawa wenzake kuokolewa. Paulo alikutana na Wayahudi hawa kila siku ya sabato, akiwafundisha maandiko ya Agano la Kale juu ya Mwokozi ambaye Mungu aliahidi kuwatumia. Aliwaeleza ya kwamba Yesu wa Nazareti ndiye aliyekuwa Mwokozi.

Je! ni marafiki gani wa Paulo waliojiunga naye wakati alipokuwa Korintho? Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 18:5.

Wayahudi hawa wa Korintho hawakupokea ujumbe wa Paulo kuwa wa kweli. Ingawa Sila na Timotheo walisema ujumbe huo ulikuwa wa kweli, ni Wayahudi wachache tu walioamini. Wale wengine walikuwa wajeuji sana kwa Paulo. Paulo aliwaambia ya kwamba ataachana nao. Alikwisha kujaribu

kuwaonyesha njia ya wokovu lakini hawakumwamini. Alisema angewepelekea watu wa Mataifa ujumbe wa Kristo.

Je! Paulo alifanya mikutano yake wapi wakati alipoondoka sinagogini? Alikwenda kwa nyumba iliyokuwa imepakana na sinagogi hiyo na ilikuwa nyumba ya mtu mmoja aliyeitwa Yusto. Yusto alikuwa Myunani na alikuwa mwamini. Hata sasa Wayahudi wangeweza kusikia habari za Bwana Yesu kama wangetaka, kwa kuhudhuria mikutano ya Paulo nyumbani mwa Yusto.

Paulo alipoendelea kuhubiri Injili, Krispo, ambaye alikuwa alikuwa mkuu wa sinagogi, pamoja na nyumba yake yote, walimwamini Kristo na kumpokea kuwa Mwokozi wao. Wakorintho wengine wengi pia waliamini na kubatizwa.

Bwana alijua kwamba Paulo angehitaji ushujaa katika hatari ambazo zingemkabili wakati wa kuhubiri Injili. Paulo alikuwa mmojawapo wa mitume mashujaa zaidi kuliko wengine wote, lakini ingawa alikuwa shujaa, alikuwa na sababu nzuri ya kuogopa chuki na pingamizi ya Wayahudi hawa wenye hasira.

Usiku mmoja Bwana alisema na Paulo katika maono. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma ujumbe wa Mungu katika Matendo 18:9-10. Paulo alipata ushujaa mwingi katika maono yale ya Bwana hata akakaa Korintho akifundisha Neno la Mungu

kati ya watu kwa muda wa mwaka mmoja na nusu.

Katika mwaka huo mmoja na nusu ambao Paulo alika Korintho, Wayahudi walimkasirika sana hata wakamkamata na kumpeleka mbele ya liwali wa Kirumi wa Yunani. Walidai ya kwamba Paulo aliwawita watu kumwabudu Mungu kinyumbe cha sheria yao. Liwali alisema kama Paulo angalivunja sheria ya Kirumi angakubaliana nao na kusitiliza kesi hiyo, lakini kwa mambo ya sheria ya Kiyahuditu, hatakubali kusitiliza kesi.

Hatimaye baada ya hayo, Paulo aliondoka Korintho akaabiri mpaka Efeso, na watu waliokuwa pamoja naye walikuwa Akila na Prisia, marafiki zake wa kushona hema. Paulo alihubiri sinagogini, Efeso kama ilivyokuwa desturi yake. Aliwaambia watu wa Efeso habari za Kristo.

Paulo aliwaacha marafiki zake wale (Akila na Prisia), akaendelea na safari yake mpaka Kaisaria, na baadaye Yerusalemu ambapo alikwenda kwa kanisa la kwanza. Mwishowe alireja Antiokia.

KAZI YA KUFANYA

Chora mstari chini ya jibu sawa la kila swali.

1. Je! Paulo alikaa pamoja na mume na mke yupi katika Korintho?

Anania na Safira

Akila na Prisia

2. Je! walifanya kazi gani?

Kushona hema

Kuvua samaki

Kulima

3. Paulo alikuwa amefundishwa kazi. Je! kazi hiyo ilikuwa nini?

Kulima

Kufuga kondoo

Kushona hema

4. Je! Paulo alihubiri wapi siku ya Sabato?

Sokoni Sinagogini Njiani

5. Aliwahubiria watu gani.

Warumi

Watu wa Athene

Wayahudi

Kata maneno ambayo si kweli katika sentensi zifuatazo.

1. Wayahudi hawakunani Injili ya Kristo, kwa hivyo, Paulo aliwaambia ya kuwa angekwenda kuwahubiria (~~Warumi~~) (Mataifa).

2. Paulo aliingia katika nyumba ya mtu mmoja aliyeitwa (Yusto) (~~Akila~~). Mtu huyu alikuwa wa Mataifa na alimwabudu Mungu. Nyumba yake ilipakana na (~~seke~~) (sinagogi).

3. Krispo, (~~kutenti~~) (mtu) wa sinagogi, pamoja na jamaa yake (~~hewekwewamini~~) (walimwamini) Kristo.

4. Watu wengine (wengi) (~~wetetehe~~) katika Korintho pia walimwamini Kristo.

Alikei katika chumba chake mle melini akingoja kuona jinsi Mungu angemimiza ahadi hizo zake. Mlango wa chumba hicho chake ulifunguka, kisha haramia mmoja akangia ndani. Marie aliwaza kama kwamba Shetani mwenyewe ndiye aliyekuwa akisimama pale na kumkazia macho.

Haramia yule alimwita Marie kwa ukali kumpatia saa yake ya mkono. Marie alimweleza kwamba hakuwa desturi yake kutoa zawadi zenye thamani kama hiyo kwa watu asiowajua. Haramia alijibu kumhonga kwa kumwambia ya kwamba angemlinda kama angempa ile saa yake ya mkono. Lakini mpaka sasa Marie alikataa.

Kwa ghafla haramia yule aliruka juu akiwa ameshika bastola yake mkononi na kumwekeza Marie kichwa na kupiga kelele akisema, "Nitakupiga risasi." Marie alimjibu kwa utulivu, "Hakuna silaha yo yote iliyotengenezwa na binadamu itakayofaa. Hii ni ahadi ya Bwana kwa watumishi wake."

Haramia yule, kwa mara ya pili tena alitisha kumpiga Marie risasi, na tena Marie akarudia kusema ahadi ile. Kwa ghafla pakaja haramia wa pili aliingia ndani akamtoa nje haramia yule wa kwanza. Haramia huyu wa pili hakutaka kumdhuru Marie.

Huu ulikuwa mwanzo wa kuona Mungu akifanya miujiza kwake. Marie alikata shauri kukaa mle chumbani mwake. Kwa siku tisa

alikuwa tu matunda, na biskuti na chokoleti ambazo alikuwa nazo. Wale maharamia waliitaka kumpa chakula walichokuwa wameiba. Lakini yeye aliwaambia, "La. Siwezi kula chakula mlichotiba."

"Basi utakufa," maharamia walimwambia.

"Ndiyo, naweza kufa," aliwajibu, "lakini Baba yangu anaweza kunifanya kuwa hai."

Siku ya kumi kabla ya kupambazuka, alisikia mtu akigonga mlango. Mtu huyu alikuwa afisa wa pili na alikuwa na mai na mikate ya Kichina ambayo alimlelea. Na baadaye, alimlelea mayai kila siku asubuhi na mapema.

Marie alianza kushawishi moyo ya maharamia wale wakati. Walikuja mlangoi pake kila siku na alisema nao akiwaambia habari za Bwana wake wa ajabu. Bwana aliendelea kumpa amani.

Wale maharamia waliambiana wao kwa wao. "Je! msichana huyu ana amani ya aina gani hi? Unaweza kuiona usoni pake. Waangalie abiria wengine. Waonekana kuwa na wasiwasi na wadhaifu kila siku."

Bada ya siku ishirini na nne wale maharamia waliacha meli ile. Walimwacha mmishe Marie bila kumdhuru. Marie alijiunza ukweli wa ahadi ile ya Mungu isemayo, "Bwana ndiye msaidizi wangu; sitaogopa cho chote mwanadamu atachonifanya."

MUNGU AMLINDA PAULO

MASOMO YA BIBLIA: Matendo

22:30; Matendo 23:1-35

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Kuna wakati ambapo sisi huwaza miyoni mwetu kuwa tuko mbali sana na Mungu, au wakati ambapo tunawaza ya kwamba Mungu yuko mbali sana nasi. Wakati kama huo tumepoteza tumaini letu katika ulinzi wa Bwana kwetu. Tunajua sikuzote ya kwamba Mungu yuko karibu sana nasi tukimtafuta. Wazo hili la kuwa mbali na Mungu, kwa kawaida ni la muda tu, na kwa kuzungumza na Mungu hata kama ni kwa dakika chache tu tunapata tena mawazo yetu ya kawaida ya kwamba Mungu yuko karibu nasi daima. Katika kufundisha somo hili juu ya Paulo, omba ili wanafunzi wako watakuwa na matumaini mapya katika ulinzi wa Bwana, kwa kumwamini na kumtii.

Somo hili linafuatana na lile lililopita. Paulo alikuwa na nia ya kuteseka kwa ajili ya Kristo kwa sababu alimpenda Bwana wake. Kwa sababu Paulo alijua ya kwamba Bwana alikuwa karibu naye, hakuogopa watu. Waonyeshe wanafunzi ya kwamba Paulo hakuogopa mambo ambayo watu wangemfanyia kwa sababu alimwamini Mungu kuwa msaidizi wake. Kusudi la somo hili ni kuonyesha kwamba Mungu atatulinda ikiwa tutamkiri.

MAMBO YA KUKAZA

1. Paulo alikuwa na akili katika kushughulika na watu waliomshaki kwa baraza la Kiyahudi.
2. Bwana alimtia Paulo moyo.
3. Bwana atakuwa msaidizi wetu kama maisha yetu yataonyesha kwamba kumpendeza yeye ni kuzuri zaidi kuliko kuwapendeza watu.

KULIFUNDISHA SOMO

Kabla ya kusimulia hadithi ya Paulo, wasimulie wanafunzi hadithi hii ya kweli ya Mwamerika mmoja mmisheni wa China.

Abiria waliokuwa na woga walinong'onezana wao kwa wao, "Meli yetu imetekwa nyara na maharamia Wachina." Ilikuwa yapata siku nyingi tangu meli yao kuanza safari. Abiria hawa walidhanja kwamba wangepatwa na jambo baya sana.

Marie Monsen, mmisheni huko China, pia aliogopa kwanza. Kisha alikumbuka ahadi fulani za Mungu zinazosema: "Usiogope maana niko pamoja nawe; usifadhaikie maana mimi ndimi Mungu wako; nitakushika kwa mkono wangu wa kume wa wema wangu." "Bwana ndiye msaidizi wangu; sitaogopa choote mwanadamu atakachonifanyia."

5. Mungu alisema na Paulo katika maono ~~(akamwambia—alikuwa hatarini—kwa—hiyo—ilimpesa kuondoka)~~ (akamwambia akae na kuwahubiria watu, wala asigope).

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Kwa maana mimi, Bwana, Mungu wako, nitakushika mkono wako wa kuume, nikikuambia, Usiogope; mimi nitakusaidia." Isaya 41:13

Mungu alitoa ahadi hii yake siku za nabii Isaya, na anatoa ahadi hii siku hizi. Tukimwamini yeye, atatusaidia. Tuna shukrani kubwa kwa kujua ya kwamba Mungu aliye hai ndiye Mungu wetu

Funga kwa maombi.

Sura ya Sita

KUMPENDEZA MUNGU BADALA YA MWANADAMU

MASOMO YA BIBLIA: Matendo

19:23-41

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Mara nyingi vijana hukabiliwa na shida ya kufanya jambo ambalo ni kosa, na wasipofanya, huchukiwa na marafiki zao. Tunapendeza kukua, tunatambua ya kwamba urafiki wa namna hii hautupasi kutaka. Katika

WAKATI WA KUFUNGA

Maisha ya Paulo yalikuwa hatarini kwa sababu Wayahudi ambao hawakumwamini Kristo walikasirika naye sana. Kama Paulo hangaliamini ahadi ya Mungu ambayo Mungu alimwahidi kumsaidia, angaliondoka Korintho. Paulo alimwamini Mungu na Mungu akamsaidia. Waulize wanafunzi wako kama wanafikiri kwamba ahadi ya Mungu inawahusu wao pia. Ndiyo, ahadi hiyo ni kwetu sisi sote tunaamini. Hebu tuseme tena kifungu cha kukumbuka. Ahadi ya Biblia kama hiyo ya kifungu cha kukumbuka hutusaidia kushinda woga. Hebu tumshukuru Bwana kwa ahadi yake kwamba atatusaidia. Tukate shauri kumwendea haraka wakati tunapojaribiwa kuwa woga.

somo hili letu juu ya Paulo, Paulo anatambua jinsi anavyowafanya watu wengi kupoteza faida katika shughuli zao kwa sababu ya mahubiri yake. Anajua ya kwamba wafanya biashara hawa hawampendi, lakini anaona ni heri kumpendeza Kristo kuliko kuwapendeza watu hawa.

Ni muhimu sana wanafunzi kujifunza kwamba ni bora

kumpendeza Kristo kuliko kuwapendeza watu, kama mambo ambayo watu hao wanataka wafanye si mazuri. Kwa hivyo, mara kwa mara vijana wanamtaka kila mtu kuwapenda, lakini si vizuri kama kupendwa huko kwao kutaweka kaika hali ya kutenda kosa. Kusudi la somo la leo ni kuonyesha kwamba ni vizuri kutenda kama Kristo angaliyaka tufanye hata kama kufanya hivyo kutatufanya kuwa na maadui wengi. Omba ili wanafunzi wako wawe na tamaa halisi ya kumpendeza Kristo bila kujali mawazo ya wengine.

MAMBO YA KUKAZA


1. Tokeo moja la kazi ya Paulo kaika Efeso lilikuwa kwamba uraji vilekalo vya sanamu ulipungua.
2. Wafanya biashara (yaani, wafua fedha) waliwataharukisha watu mjini kote.
3. Inawapasa Wakristo wakati mwingine kuchagua kama wanataka upendeleo wa nani - wa wanadamu au wa Kristo.

KULIFUNDISHA SOMO

Wakristo wengi wana tamaa mbalimbali. Hutafuta kumtumikia Kristo na wakati huo huo wanatafuta mambo ya kidunia. Mtume Paulo alijizua kuwa na tamaa mbalimbali kama hizo. Alijioa sana sana kwa Kristo hata akajichukua mwenyewe kama mtumwa wa Kristo. Alikaata kupokea mapenzi ya wanadamu

kushindana na kusudi lake la kupata kibali cha Kristo.

Paulo alisimama Efeso alipokuwa njiani kwenda nyumbani wakati wa safari yake ya pili ya umisheni. Alikuwa amewaacha Priscila na Akila, marafiki zake wa kutengeneza hema katika mji huo. Na wakati aliporudi Efeso katika safari yake ya tatu ya umisheni, alika kwa miaka miwili akifanya kazi nao na kushuhudia Bwana. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 19:8-9. Tunaona ya kwamba Paulo alilingia tena sinagogini kama alivyofanya Korintho. Alilingia katika darasa la mtu mmoja aliyeitwa Tirano. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 19:10-11. Mungu alifanya miujiza mingi sana kuwa huduma ya Paulo. Watu waliokuwa wakifanya uganga walieta vitabu vyao pamoja na kuvichoma. Vitabu hivi vilikuwa na thamani ya fedha hamsini elfu, lakini waganga hao walijua kwamba Kristo hakupenda mambo hayo ya kuagua.



tutajifunza mambo ambayo Paulo aliwaambia viongozi wale.

KAZI YA KUFANYA

Paulo aliingia hekaluni Yerusalemu. Alitaka kuwaonyesha Wayahudi kwamba alishika sheria za Mungu. Wakati Wayahudi wengine wasioamini walipomwona Paulo ndani ya hekalu, waliamua kuwataharukisha watu juu yake. Weka herufi hii "X" kando ya mambo ambayo Wayahudi walishitaki Paulo kufanya.

X Kufundisha mambo kinyume cha watu.

Kufundisha mambo yanayo-pinga dhambi.

X Kufundisha mambo kinyume cha sheria.

X Kufundisha mambo kinyume cha hekalu.

X Kunwingiza Myunani ndani ya hekalu lao takatifu.

Jaza nafasi zilizochwa katika sentensi zifuatazo kwa majibu ya kweli.

1. Paulo aliongea lugha gani na jemadari? Kiyunani

2. Paulo aliongea lugha gani na Wayahudi? Kiebrania

3. Ni jina lipi Paulo aliotaja ambalo liliwakasirisha sana Wayahudi? Watu wa mataifa

Chora mwingi kwa maneno ya kweli katika sentensi zifuatazo.

1. Jemadari aliwaamuru askari wake

kumlisha kupigana kumpiga Paulo.

2. Paulo alisema ya kwamba yeye alikuwa Mwafrika

mtu mwema raia wa Rumi.

3. Paulo hakupigwa lakini aliwekwa gerezeni alipewa kianda laini aliambiwa kusoma sheria.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Maana mmepelewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, ila na kuteswa kwa ajili yake." Wafilipi 1:29

Katika kifungu hiki Paulo anawaambia Wafilipi ya kwamba wanapaswa kuteseka kwa ajili ya Kristo. Paulo aliteseka bila huzuni kwa ajili ya Kristo. Inatupasa sisi kuwa tayari kuteseka kwa Kristo ikiwa ni lazima.

WAKATI WA KUFUNGA

Paulo hakunung'unika juu ya mateso yaliyomjia maishani mwake kwa sababu alikuwa mtifu kwa Kristo. Alijua kwamba kwa kutokuwa mtifu kwa Yesu ambaye alikufa kwa ajili yake kungemdhuru zaidi mno.

Wakati mwingine tunaweza kuwa na nafasi za kuthibitisha utii wetu kwa Kristo. Yatupasa kuwa kama Paulo, na kuwa na nia ya kuteseka kwa ajili ya Bwana na Mwokozi wetu.

wote wa mji kukasirika naye. Alimwekea Paulo ulinzi mkali asipate kutoroka. Kisha jemadari aliwauliza watu ya kuwa Paulo alikuwa nani na alifanya nini. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma jibu ambalo jemadari alijihiwa na watu wale katika Matendo 21:34. Ilikuwa vigumu kwa jemadari kupata jibu la kweli kutoka kwa watu, kwa hivyo aliwaamuru askari kumkamata Paulo na kumfunga kwa minyororo na kumpeleka ngomeni ambako angekaa salama. Walipofika katika daraja kuingia ngomeni, iliwabidi askari kumbeba Paulo kwa sababu ya umati ule mkubwa wa watu wenye hasira waliopiga kelele wakisema, "Mwondoe huyu." Maana yake hasa ni kwamba walitaka askari kumwua Paulo.

Walipofika tayari kuingia ngomeni, Paulo alisema na jemadari kwa lugha ya Kiyunani. Jemadari alifikiri ya kwamba Paulo alikuwa Mmisiri yule ambaye kabla ya siku zile aliwafitinisha watu. Paulo alimwambia ya kwamba yeye alikuwa Myahudi kutoka Tarso. Kisha alimwomba jemadari kumruhusu kusema na watu wale. Jemadari alipokubali, Paulo alisimama madarajani kisha akasema na watu wale kwa lugha ya Kiebrania. Walinyamaza na kumsikiliza Paulo akiwaambia habari kuhusu ugeuzi wake. Waliyasikiliza maneno ambayo alikuwa akisema na kupendelewa nao mpaka wakati aliposema kwamba Mungu alimtuma kuwahubiria watu wa Mataifa. Neno hili lilikwasirisha

sana wakaanza kupaza sauti zao wakisema auawe. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma jinsi watu wale walivyoonyesha hasira zao katika Matendo 22:23. Jemadari ambaye hakuelewa maneno ambayo Paulo aliyasema kwa lugha ya Kiebrania, alidhania kwamba Paulo alifanya kosa kubwa sana kwa maana watu walimkasirikia sana. Alikata shauri kuamuru Paulo kupigwa ili ajue sababu. Wakati askari walipokuwa wakimfunga Paulo na kumweka tayari kupigwa, Paulo alimwuliza jemadari swali. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma kifungu cha 25 cha Matendo 22. Kulingana na sheria za kirumi, hakuna raia ye yote wa Rumi ambaye angeweza kufungwa wala kuadhibiwa kwa njia ya yote mpaka anapohukumiwa na kupatikana na hatia. Jemadari alimfikiria Paulo kuwa ni Myahudi tu na hakudhania kwamba angeweza kuwa raia wa Rumi.

Paulo aliepuka kupigwa, lakini alikuwa bado mfungwa. Jemadari alikuwa hajajua sababu ya Wayahudi kumtaka Paulo kuawa. Hangeveza kumfungua mpaka wakati ambapo angefanya uchunguzi na kujua habari zake. Pia alifikiri kwamba Paulo alikuwa salama sana gerezani kuliko vile angalikuwa nje ambako Wayahudi wangemfikia na pengine kumwua.

Siku ya Pili yake, jemadari aliwaita viongozi wote wa dini ya Kiyahudi, akampa Paulo nafasi ya kujitetea mbele yao. Katika somo litakalofuata

Mji wa Efeso ndipo palipokuwa makao ya mungu mke Artemi. Watu kutoka nchi nyingi walikuja kumwabadu. Sanamu ya Artemi haikuwa nzuri kama sanamu nyingine za Wayunani; lakini watu waliamini kwamba sanamu hiyo ya jiwe ilianguka kutoka mbinguni. Waliweka ndani ya hekalu zuri lililojengwa kwa mawe meupe. Karibu kila mtu aliyetembelea mji wa Efeso alinunua sanamu ndogo ya Artemi au vihekalu vyake. Sanamu hizi ambazo zilitengenezwa kwa udongo, kwa miti, au kwa vyuma, watu walizichukua na kusafiri nazo kama hirizi ya kuwaletwa bahati njema. Hata nyingine ziliwekwa nyumbani kama miungu wa nyumbani.

Mafundi waliotengeneza sanamu hizi na kuziua, pamoja na vihekalu, walipata faida nyingi. Paulo aliona moyoni mwake ya kwamba kama alihubiri kweli Neno la Mungu kwa uaminifu, ilimpasa kuwaambia watu ya kwamba ilikuwa kosa kumwabadu Artemi. Bila shaka alijua kwamba jambo hilo lingelea shida baina yake na mafundi wale waliotengeneza sanamu hizo za Artemi na kuziua. Kwanza ilimpasa (yeye Paulo) kujibu swali hili moyoni mwake: "Je! niwapendeze nani, wanadamu au Kristo?" Alijua ya kwamba watu kama wangejifunza kumpenda Kristo na kumwabadu, wangekoma kununua sanamu za Artemi. Paulo alijibu swali lake? Alikusudia kumpendeza Kristo hata kama angekuwa na uadui na mafundi wake waliotengeneza sanamu.

Mungu alibariki mahubiri ya Paulo. Watu wengi waliacha imani yao ya uwongo na kumwamini Mungu wa kweli aliye hai. Wakristo hawa, kwa kweli walimpenda Paulo, wakawa marafiki zake.

Paulo alikata shauri kukaa Efeso mpaka baada ya karamu ya Pentekoste kwisha. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma 1 Wakorintho 16:8-9. Siku hii ilitokea katika mwisho wa mwezi wa Mei. Na huu ndio mwezi ambao watu wengi walikuja Efeso kumwabadu Artemi. Watu walifika kutoka kila sehemu za jimbo hilo kufurahia mchezo na sherehe iliyofanywa kwa heshima ya mungu mke wao. Bila shaka, Paulo alikuwa akitazamia wakati huu wa sherehe kwa sababu aliwaambia watu hawa habari za Mwokozi aliyekufa ili kuwaokoa katika dhambi zao.

Je! watu wale waliompokea Bwana Yesu kama Mwokozi wao wangeendelea kumwabadu Artemi? La, hawangeendelea kwa maana sasa wangekuwa na mwokozi aliye hai maishani mwao na hawangekuwa na hitaji lo lote la hirizi ya bahati njema. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 19:26.

Mtu mmoja aliyeitwa Demetrio alikuwa mmojawapo wa mafundi wale waliotengeneza sanamu za kuwauzia watu. Aliona ya kwamba watu walikuwa hawanunui sanamu kama zamani. Hakuwa akipata faida nyingi kama zamani. Mafundisho ya Paulo yalikuwa yakiangusha biashara

ya mafundi wote waliotengeneza sanamu katika Efeso.

Demetrio aliita mkutano wa mafundi wote wa sanamu. Aliwakumbusha kwamba waliitajirika sana kutokana na biashara ile ya kutengeneza sanamu na kuziiza. Pia aliwarifu ya kuwa mafundisho ya Paulo yalikuwa yakiwazua watu kununua sanamu katika Efeso na katika Asia yote. Alisema ya kwamba hawakuwa katika hatari ya kupoteza biashara yao peke yake, bali hata hekalu la Artemi lilikuwa katika hatari ya kuhesabiwa si kitu. Heshima ya mungu mke wao aliye mkuu ilikuwa hatari. Demetrio aliwafanya watu hao wengine kukasirika sana juu ya jambo hilo. Walianza kupiga kelele, wakisema, "Artemi wa Efeso ni mkuu."

Watu wengi hukusanyika mara moja wakati lisilo la kawaida linapofanyika. Baada ya muda mfupi watu huzidi kuongezeka. Jambo kama hili ndilo lililofanyika Efeso. Baada ya muda mfupi, Waefeso wote walikuwa wakipiga kelele pamoja na mafundi wale wa kutua fedha, na kusema, "Artemi wa Efeso ni mkuu." Hata baadhi ya watu waliokiri upendo wao kwa Kristo walijiunga na watu wale.

Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 19:29 kuona ni shida ipi iliyokuwa ikioka. Je! Paulo aliyekuwa chanzo cha shida hiyo alikuwa wapi? Mara tu aliposikia kelele hizo alitaka kwenda

katika mahali pale pa mchezo ambapo waliwapeleka marafiki zake wawili. Lakini wanafunzi pamoja na baadhi ya wakuu wa Asia walimsihi asiende. Walijua kama Paulo angekwenda pale, basi ghasia zingezidi kuendelea.

Mkutano ule ulikuwa umechafuka sana hata wengine hawakujua sababu ya kukusanyika kwao pale. Juhudi zilifanywa kuwatuliza watu lakini waliendelea tu kupiga kelele, "Artemi wa Efeso ni mkuu." Mwishowe, karani wa mji aliwatuliza watu.

Karani huyu wa mji alianza kusema na watu kwa ujia ya werveu ambayo wangependa kuelewa. Aliwaambia ya kwamba kila mtu alijua Waefeso walimwabudu Artemi mungu mke aliye mkuu, kwa hivyo hapakuwa na sababu ya kuwa na wasiwasi. Aliwaambia kwamba Paulo na wenzake hawakufanya kosa lo lote. Hawakuiba vitu vya hekalu wala kumtukana mungu mke wao, Artemi. Aliongeza kusema kwamba ikiwa Demetrio alikuwa na neno juu ya mtu ye yote, neno hili lilipaswa kupelekwa barazani kuhukumiwa. Aliwaambia watu kuondoka na kwenda zao kwa amani kama siyo wangepigia taabuni kwa kuanzisha ghasia.

Paulo alichagua kumpendeza Kristo kuliko kumpendeza mwanadamu. Mungu alimsaidia katika hali hii. Baada ya ghasia kwisha, Paulo aliwaita wanafunzi wake, akazungumza nao, kisha akaondoka kwenda Makedonia.

imani katika Kristo kama Mwokozi. Wayahudi wale walikuwa wamezifanya sheria hizo kutawala maisha yao kwa miaka mingi sana na ilikuwa vigumu sana kwao kubadili fikira zao.

Ilikuwa muhimu kwa Wakristo Wayahudi Yerusalemu kumwamini Paulo kwa hivyo wazee walimtolea pendekezo juu ya jambo la kufanya. Walimwambia Paulo kwamba palikuwapo watu wanne ambao waliofungwa nadhiri kumtumikia Bwana. Watu hawa walipanga kuingia hekaluni na kuoga humo na kunyoa vichwa vyao kama ishara ya utakaso wao. Wazee wale walimdokeza Paulo akaingia pamoja na watu wale wanne na kujitakasa. Jambo hili lingewapendeza Wakristo Wayahudi ya kwamba Paulo alikuwa akiti sheria ya Musa. Paulo alifanya kama walivyodokeza kwa sababu alitii kweli sheria za Musa sikuzote. Ilikuwa muhimu kwa Paulo kuwa hekaluni kwa siku saba kuondoa nadhiri ile ambayo yeye na watu wale wanne Wayahudi waliweka. Kabla ya siku hizi saba kumalizika, Wayahudi wengine wasioamini kutoka Asia walimwona Paulo hekaluni. Walijua ya kwamba Paulo alimleta mtu mmoja wa Mataifa Yerusalemu kutoka Efeso kwa sababu walikwisha kuwaona pamoja mjini mle. Ilikuwa uwongo, lakini wao walisema kwamba Paulo alimwingiza mtu huyu wa Mataifa hekaluni.

Wayahudi walikuwa na sheria kali sana iliyowakataza mtu ye yote wa Mataifa kuingia katika mahali pao pa

ibada. Walifikiri wao ndio waliokuwa watule pekee wa Mungu, na kwamba mahali pao pa ibada palipaswa kutumiwa na wao wenyewe.

Wayahudi wale kutoka Asia walijua kwamba wangepachagua watu kwa kuwaambia ya kwamba Paulo alimwingiza mtu wa Mataifa hekaluni. Wayahudi wale walisema ai Paulo alikuwa akifundisha kinyume cha sheria ya Wayahudi na ya hekalu. Pia walisema ai Paulo aliita hekalu unajisi kwa kumwingiza mtu wa Mataifa ndani.

Je! habari hii ilikuwa kweli? La. Lakini watu hawa hawakujali kungoja na kupata ukweli ndani yake. Walianini tu mambo ambayo Wayahudi wale kutoka Asia walisema, kwa hivyo walimkamata Paulo, wakamburuta, wakamtoa ndani ya hekalu, kisha wakafunga miango. Walikuwa na nia ya kumwua Paulo na hawakutaka kutia hekalu lao unajisi kwa kumwua akiwa ndani ya hekalu.

Mmoja wa askari walinzai alimpasha jemadari habari ya kwamba mji wote ulikuwa umechafuka. Jemadari aliwachukua askari haraka wakenda mjini ambalo kulikuwa ghasia. Watu walipowaona jemadari na askari wake wakitwaja mbio, waliacha kumpiga Paulo. Baada ya jemadari kumwoko Paulo, aliamuru afungwe kwa minyororo. Jemadari hakujua kwamba Paulo hakua na hatia. Alidhania kuwa Paulo alitenda kosa kubwa sana ambalo lililofanya watu

KUTESEKA KWA AJILI YA KRISTO

MASOMO YA BIBLIA: Matendo

21:18-22:29

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wokovu kwa imani katika Yesu Kristo unatolewa bure kwa wenye dhambi, lakini kuwa Mkristo mwanafunzi tunahitaji kwamba tuwe na nia ya kuacha mambo yote kuhusu hali yetu na vitu vyote tuliyo navyo. Paulo alitangaza nia yake ya kuteseka kwa ajili ya Yesu. Katika somo hili tunamwona akijaribiwa. Ilimbidi kufanya uchaguo mgumu sana. Je! angeweza kuwa mwaminifu kwa Yesu bila kujali mambo aliyotendewa na wengine? Kusudi la somo hili ni kuonyesha kwamba ni lazima kuwa mwaminifu kwa Yesu kila siku na kila saa.

Paulo alipokea maonyo ya haraka ya kumzuia kwenda Yerusalemu, lakini maonyo hayo hayakumzuia kwenda. Alipofika Yerusalemu alikwenda nyumbani mwa Yakobo akatoa habari njema kuhusu kazi ambayo Mungu alifanya katika Mataifa kwa huduma yake. Viongozi na Wakristo wa Yerusalemu walifurahi kujua kwamba Mungu alimpatia Paulo ushindi mkuu katika kazi yake ya umisheni.

Tutaona katika somo hili kwamba iliwalazimisha viongozi kumpasha Paulo habari ya kuhuzunisha.

MAMBO YA KUKAZA

1. Paulo alikwenda hekaluni kuwaonyesha Wayahudi kwamba aliamini kutii sheria za Mungu.
2. Paulo alitaka Wakristo Wayahudi kutambua ya kwamba watu wa Mataifa pia walikuwa watu wa Mungu na walipaswa kujua habari za Kristo.
3. Paulo hakunung'unika juu ya mateso yake, bali aliendelea kumshuhudia Kristo.

KULIFUNDISHA SOMO

Viongozi Wakristo ambao walikwisha kumsikia Paulo akieleza habari kuhusu kazi yake ya umisheni, walitaka Wakristo wengine Wayahudi kuelewa maneno ya Paulo na kumwamini. Iliwabidi kumwambia Paulo habari ya kuhuzunisha kwamba Wakristo wengi Wayahudi katika Yerusalemu hawakumwamini. Wakristo hao Wayahudi walikuwa wakimshtaki Paulo kwa kuwafundisha Wayahudi katika nchi nyingine kutotii sheria za Musa. Lakini Paulo hakuwa akiwafundisha Wayahudi wale kutotii sheria za Musa, bali alikuwa akifundisha kwamba imani katika Kristo ndilo lililokuwa jambo muhimu. Baadhi ya sheria ambazo Wayahudi walifikiria kuwa nzuri, Paulo aliwaambia kwamba hazikuwa nzuri kwa sababu hazikuhusiana na

KAZI YA KUFANYA

Jaza nafasi zilizoachwa katika sentensi zifuatazo.

1. Katika somo hili tunamwona Paulo katika mji wa Efeso.
2. Kwanza Paulo alihubiri katika sinagogi.

3. Paulo aliondoka sinagogini akahubiri katika darasa la Tirano.

4. Demetrio aliyekuwa mfua fedha maarufu katika Efeso alitengeneza sanamu za Artemi na vihekalu na kujipatia faida pesa nyingi.

Picha hiyo hapo chini inaonyesha hekalu, pesa, na mikono. Chora mstari kutoka kwa kila swali hadi kwa mojawapo ya vitu hivyo pichani ambacho ndicho jibu la swali hilo.



1. Je, Ni kitu kipi katika picha kinachoonyesha kwamba wafua fedha walipata kwa kufanya sanamu?

2. Je! Paulo alisema kwamba Mungu hawezi kufanywa kwa nini?

3. Je! watu wa Efeso wangehesabu nini kuwa si kitu kama wangeendelea kumsikiliza Paulo?

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Nimemweka Bwana mbele yangu daima, kwa kuwa yako kuumeni kwangu, sitaondoshwa." Zaburi 16:8

Mwandishi wa Zaburi aliyeandika kifungu hiki cha kukumbuka, alisema

kwamba alimweka Bwana mbele yake daima. Kwa kuwa na Bwana karibu hangeweza kuwa na wasiwasi wakati alipoazimu kufanya jambo ambalo lilimfanya kutopendwa na watu

WAKATI WA KUFUNGA

Katika kufunga itakuwa vizuri kueleza juu ya Roho Mtakatifu aliye ndani yetu sisi kama Wakristo. Mungu alituma Mwanawe ulimwenguni kuwa Mwokozi wetu. Mwanawe Yesu Kristo, aliwafundisha watu upendo wake. Kristo alipojua ya kwamba wakati wake wa kuondoka ulifika, aliwaambia watu kwamba hangewaacha peke yao; bali angewatumia Roho Mtakatifu kukaa nao daima. Roho Mtakatifu alimpa Paulo nguvu na hekima ya kufanya mambo yaliyompendeza Mungu wala siyo ya kumpendeza mwanadamu.

Waulize wanafunzi: Je! mnaweza kufikiria wakati ambapo unatubidi kuchagua kumpendeza Kristo au kuwapendelea watu? Wasaidie wanafunzi kutambua kwamba wanapopatana na watu vizuri, wakati huo karibu wote wanampendelea Kristo. Wakati mwingine inatubidi kutojali kupendwa na watu ili tuweze kuwa watifu kwa Kristo. Wakati kama huo unapotufikia, Mkristo wa k'eli anaweza kumtegemea Roho Mtakatifu kumtia nguvu ili aonyeshe utii wake wa kwanza kwa mwokozi wake.

Funga kwa maombi ya kwamba mtaweza kuwa waaminifu kwa Kristo wakati wote.

PAUL AENDA YERUSALEMU

MASOMO YA BIBLIA: Matendo
20:13-38, 21:1-19

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Katika sehemu zote za ulimwengu, daima kuna watu ambao hujiaribu kutuzaia kufanya jambo tunalifikiria kuwa haki. Tukijua ya kwamba jambo tunalofanya ni la haki, tuendelea kufanya katika njia hiyo hata kama wengine wanajaribu kutongoza kufanya katika njia nyingine.

Katika somo hili tunamwona Paulo akiwa na nia ya kwenda Yerusalemu, lakini marafiki zake wanaona hatari itakayompata akienda huko. Wanajaribu kumshawishi asiende. Marafiki hawa wanafanya mambo wanayofikiri kuwa haki kwa Paulo, na inampa Paulo ugonu wa kukataa mashauri yao; ingawa anajua kwamba anafanya jambo la haki.

Wakati unapojiandaa kufundisha, fikiri wanafunzi wako na jinsi somo hili juu ya Paulo linaweza kuwa na mvuto kwa maisha yao. Wako katika umri ambao wanaweza kuwa chini ya mvuto mbaya na pia mzuri.

Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wanafunzi wako kuwa imara kutenda haki hata kama wakiambiwa kufanya jambo lingine.

Waonyeshe wanafunzi ya kwamba Paulo alikataa kuacha mambo

aliyoamini kuwa ndiyo mapenzi ya Bwana kwake.

MAMBO YA KUKAZA

1. Paulo alikataa mawazo yake mwenyewe yaliyomshawishi kutofuata mapenzi ya Mungu.
2. Paulo alikataa kushawishiwa na marafiki zake kutofuata mapenzi ya Mungu.
3. Sisi pia inatupasa kuwa na nia ya kwenda kumshuhudia Bwana mahali po pote.

KULIFUNDISHA SOMO

Tunekuwa tukisafiri na Paulo katika safari yake ya tatu ya umisheni. Sasa anafanya mipango ya kurudi Yerusalemu.

Baada ya ghasia iliyotokea Efeso, Paulo alipita Makedonia na kutembelea makanisa pale. Kisha aliendelea na safari mpaka Uyunani. Waambie wanafunzi kutafuta Efeso katika ramani, na kufuata njia itokayo Efeso kwenda Makedonia na Uyunani. Labda aliabiri kutoka Efeso mpaka Makedonia. Kisha aliembea kwa miguu kupita nchi hiyo ya Makedonia mpaka Uyunani. Paulo alikaa Uyunani kwa miezi mitatu. Alipanga kuabiri kwenda Troa, kisha kutembea kupitia mji alipotaka kutembelea na kwenda Yerusalemu. Mwambie mwanafunzi



KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Kisha nikaisikia sauti ya Bwana, akisema, Nintume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nintume mimi." Isaya 6:8

Kifungu hiki cha kukumbuka kinajieleza chenyewe. Yatupasa sisi sote kumsikiliza Bwana na kumtii. Labda anataka wewe au mwanafunzi wako ye yote kuwapelekea wengine neno lake. Wakati huu sasa ambapo unajifunza kufundisha darasa lako, unamtii Mungu na unawapelekea wanafunzi wako neno lake.

WAKATI WA KUFUNGA

Waulize wanafunzi wako maswali haya: Je! basikeli ingekuwa na msaada gani kama ingetumiwa kwa muda tu na kuharibika? Saa (ya mkono) ingekuwa na msaada gani kama mtu anayeivaa hawezi kuiigemea? Askari angekuwa na usiadizi gani kama hawezi kumtii afisa wake wakati wote? Je! Paulo angalikuwa na msaada gani kama angalimtii Bwana kwa wakati fulani tu?

Funga kwa maombi.

angekabiliwa na hatari ya kufungwa gerezeni. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma majibu ya Paulo katika Matendo 21:13. Hata mwishowe marafiki hawa waliona kwamba hawakuwa na jambo la kusema wala kufanya ili kubadili nia ya Paulo. Waliacha kumsihii asiende wakamwombea wakisema, "Mapenzi ya Bwana yatendeke."

Paulo alifunga safari kwenda Yerusalemu bila kujali maonyo yale, akijua wazi kwamba alikabiliwa na mateso na taabu. Ingawa marafiki zake hawakumtaka kwenda, walikwenda pamoja naye. Hii ilikuwa mara ya tano Paulo kutembelea Yerusalemu tangu alipokuwa Mkristo. Katika mji huu, Wakristo wengine waaminifu walipenda sana Paulo kuwatembelea. Wakati alipowasili huko walimpokea na furaha.

Siku ya pili baada ya Paulo kuwasili Yerusalemu, yeye na marafiki zake walikwenda kumwona Yakobo ambaye alikuwa kiongozi wa kanisa la Yerusalemu. Viongozi na wazee walikuja kusikia habari kuhusu huduma ya Paulo. Paulo aliwaambia mambo yote kuhusu kazi ambayo Bwana alitenda katika Mataifa kwa huduma yake. Alivaeleza miji yote ambayo alitembelea na makanisa mapya waliyoanzishwa.

Tangu Paulo kuwa Mkristo, alimtii Bwana wakati wote. Aliwaza moyoni kwamba Bwana alimtaka kurejea

Yerusalemu, na ingawa marafiki zake waliompenda walijaribu kumzuia kuingia hatarini, Paulo alikuwa akimsikiza Mungu badala ya kuwasikiliza wao.

KAZI YA KUFANYA

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kuandika majibu ya kweli katika nafasi zilizoacha.

1. Paulo alikuwa amepanga kwenda Uyuni. Alibadilisha nia yake kwa sababu Wayahudi walipanga kumwua.
2. Waamini wa Tiro walimwonya Paulo ya kwamba asiende Yerusalemu.
3. Wakati wa Paulo kuondoka Tiro ulipofika, Wakristo wote walim-sindikiza mpaka pwani.
4. Kabla Paulo kuondoka Tiro, walipiga magoti pwani wakaomba.
5. Katika Kaisaria, Paulo na marafiki zake walikaa nyumbani mwa Filipo.

Katika Kaisaria, marafiki za Paulo walimsihii asiende Yerusalemu. Lakini Paulo aliwaambia kwamba alikuwa tayari kuawa kwa ajili ya Bwana. Marafiki zake hawakuweza kumbadili nia. Andika maneno ambayo walimwambia.

mmoja kusoma Matendo 20:3 mpate kuona sababu iliyomfanya Paulo kubadili mipango yake ya kuabiri. Alitembea kwa miguu kupitia Makedonia tena mpaka Filipo ambako aliingia mashua na kuabiri hadi Troa.

Paulo na marafiki zake, Luka na Timotheo, walikaa Troa kwa muda wa siku saba. Alikuwa na haraka kurudi Yerusalemu kuadhimisha Karamu ya Pentekoste kwa hivyo hakuwa na wakati wa kwenda Efeso tena. Aliwauliza wazee wa kanisa la Efeso kukutana naye Milato. Wasaidie wanafunzi kutafuta miji ya Efeso na Milato katika ramani wapate kuona jinsi miji hii miwili ilivyo karibu.

Katika Milato ndipo Paulo alipowapa wazee wale maneno ya mwisho. Aliwaambia pengine hawangeweza kumwona uso tena. Aliwaambia ya kwamba sasa uongozi wa makanisa ungekuwa chini yao. Pia aliwaambia kwamba alikwisha kuonywa asirejee Yerusalemu, na kwamba akirejee angekabiliwa na mateso na taabu. Pia aliyajibuje maonyo haya? Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 20:24. Paulo alikusudia kurejea Yerusalemu kwa sababu aliwaza moyoni mwake ya kwamba Bwana ndiye aliyemtaka kurejea huko.

Baada ya Paulo kuwaaga wazee wale wa Efeso, merikebu ambayo yeye pamoja na marafiki zake walisafiria ilikwenda hadi kisiwa cha Kosi. Siku ya pili yake walifika Rodo.


Kutoka Rodo waliendelea na safari mpaka Patara. Kutoka Patara walisafiri mpaka Foinike karibu na pwani ya Kipro, kisha wakashuka Tiro. Waambie wanafunzi kufuata safari hii katika ramani yao.

Merikebu waliyokuwa nayo ndani ilishusha shehena yake hapa Tiro na ikakaa kwa muda wa siku saba. Paulo aliwakuta Wakristo marafiki katika mji huu. Marafiki hawa walipoambiwa na Paulo ya kwamba alikuwa safarini kwenda Yerusalemu, walimwonya asiende. Walimwambia angekabiliwa na hatari kama akienda huko. Lakini Paulo aliwaambia hana budi kwenda kwa maana aliona ni Bwana ndiye aliyemtaka aende Yerusalemu. Marafiki hao walimsindikiza hadi pwani, kisha wote wakapiga magoti wakaomba.



Kutoka Tiro, Paulo na marafiki zake walisafiri mpaka Kaisaria na wakakaa nyumbani mwa Filipo kwa siku chache. Hapa tena Paulo alionywa asiende Yerusalemu kwa maana

Ulimwengu katika
Siku za Paulo



PAULO, MJUMBE WA MUNGU

VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

(MWALIMU)

Mwaka wa Kwanza

Kitabu cha Tatu

Africa Coordinated Curriculum for Bible Study

J1 - 3Ts

With permission of International Publications Services



Published and Printed by
Baptist Publications House
Thika Road, Ruaraka
Box 30370, Nairobi

Wewe pia unaweza kukua na kupata imani zaidi kwa kujifunza mafunzo haya.

(Unapofunga darasa kwa maombi, kumbuka kuwaomba wanafunzi wako pamoja nawe ili mtaweza kutambua hitaji la kuishi maisha mema kwa ajili ya Kristo kama Paulo alivyofanya.)

VIFUNGU VYA KUKUMBUKA:

Tabuni basi, murejee, ili dhambi zenu zifuwe. Matendo 3:19a

Mwenende kama uliyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa, mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu. Wakolosal 1:10

Nitawimbia Bwana maadamu ninaishi; nitamshangilia Mungu wangu nikiwa hai. Zaburi 104:33

Amin, amin, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haiingii hukumu, bali amepita kutoka mavini kuingia uzimani. Yohana 5:24

Kwa maana mimi, Bwana, Mungu wako, nitakushika mkono wako wa kuume, nikikuambia, Usiogope; mimi nitakusaidia. Isaya 41:13

Nimemwaka Bwana mbele yangu dalma, kwa kuwa yako kuumei kwangu, sitaondosha. Zaburi 16:8

Kisha nikaisikia sauti ya Bwana, akisema, Nintume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, "Mimi hapa, nitume mimi." Isaya 6:8

Maana mamepea kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, ila na kutewa kwa ajili yake. Wafilipi 1:29

Hata twaithubutu kusema, Bwana ndiye anisaidiye, sitaogopa; mwanadamu atanitenda nini?

Waraka kwa Waheberania 13:6

Juani ya kuwa yeye amrejaye mwenye dhambi hata atoke katika njia ya upolevu, ataokoa roho na njia ya upolevu, ataokoa roho na mauti, na kufunika wingi wa dhambi. Yakobo 5:20

Huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi. Warumi 4:21

Lakini nawambia ninii mnaosikia, wapendani adui zenu, wataendani mema wale ambao wawachukia ninyi. Luka 6:27

kuwa Mkristo." Sasa, katika ramani yako unaweza kuandika namba 1 kando ya mji ambao Paulo aligeuzwa kuwa Mkristo. Hadithi hii inapatikana katika Matendo 9:3-9.

"Mambo mengi ya ajabu yalinifanyikia katika safari zangu. Nilikutana na watu wengi walionitakia baraka za Bwana. Siku moja marafiki wengine waliononya nisingi mji wa Yerusalemu. Watu hawa walikuwa marafiki zangu wa mji wa Tiro. Kabla ya kuwaacha na kuendelea na safari yangu, tulipiga magoti pwani kuomba." Tafuta mji huu katika ramani yako, kisha andika namba 2 kando yake. Ukihitiaji kutafuta majibu ya maswali haya, soma Matendo 21:3-6.

"Wakati nilipokuwa katika mji wa Kaisaria ilinibidi kupeleka kesi yangu mbele ya liwali mpya. Jina la liwali huyu mpya lilitwa Festo. Nilikuwa nimekwisha kukaa gerezani miaka miwili. Sasa wakuu wa Wayahudi walikuwa bado wakijaribu kunifanya niuawe. Kisha nilipeleka kesi yangu mbele ya mfalme, aliyetwa Agripa. Yeye pamoja na Bernike, dada yake, walisikia maneno yangu."

Tafuta mji huu katika ramani yako na uandike namba 3 kando yake. Ukihitiaji kuhakikisha majibu yako, soma Matendo 25:13-22.

"Nilitaka rufani kwa Kaisari ili aweze kusikia kesi yangu, kwa hivyo Festo alinituma Rumi. Safari ya kwenda Rumi ilikuwa ndefu na mambo mengi ya ajabu yalinifanyikia njiani. Nilimwambia nahodha wa

merikebu tukae pale katika Bandari Nzuri wakati wa baridi. Lakini yeye hakunisikiliza, basi tukaanza safari ya kwenda Foinike. Tulipokuwa njiani, dhoruba kali ilitujia. Baada ya siku nyingi, merikebu yetu iliyunijika na sisi sote tukafika salama katika kisiwa cha Melita."

Tafuta kisiwa hiki katika ramani yako halafu andika namba 4 hapo. Maelezo juu ya safari hii ya ajabu yanapatikana katika Matendo 27:8-12, 41 na Matendo 28:1.

WAKATI WA KUFUNGA

Waulize wanafunzi swali hili: "Niambi eni baadhi ya mambo ambayo tumekwisha kujifunza katika maisha ya Mtume Paulo?" (Wape wakati wa kujibu.) Utataka kuongoza wakati huu wa mazungumzo kwa kuwakumbusha wanafunzi kweli za Biblia ambazo zimekwisha kufundishwa katika masomo yote ya kitabu hiki. Kwa hivyo itakubidi kufahamu hadithi ambazo tumekwisha kujifunza na ukweli hasa muhimu wa kila hadithi.

Paulo anaweza kuwa mfano mwema kwa maisha yetu sisi kama Wakristo. Imani yake na ushujaa wake hata wakati wa shida, yanaweza kututia moyo hata sasa. (Je! mwalimu, umekwisha kujifunza nini kwa Paulo? Umekwisha kujifunza kudai ahadi za Mungu ukijua ya kwamba utazitimiza? Je! umekwisha kupata furaha ya kushiriki imani yako na wengine kama Paulo alivyoshiriki imani yake na watu aliokutana nao?

VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA [MWALIMU]

Mwaka wa Kwanza

Kitabu cha Tatu

YALIYOMO

Sura

Ukurasa

1. Ugeuzi Kamili 5
2. Kumpa Kristo Nafasi ya Kwanza 9
3. Kuimba Gerezani 12
4. Paulo Ahubiri Athene 16
5. Usiogope 20
6. Kumpendeza Mungu Badala ya Mwanadamu 24
7. Paul Acenda Yerusalemu 29
8. Kuteseka kwa Ajili ya Kristo 35
9. Mungu Amlinda Paulo 39
10. Kumshuhudia Kristo 44
11. Kuhakikisha Ahadi za Mungu 48
12. Jinsi ya Kuwatendea Maadui 54
13. Somo la Marudio 59

kwa Wakristo wote wa nyakati zile alipoishi.

Kwa kurudia maisha ya Paulo, ingekuwa jambo la busara kuyachukua masomo yote na kuyasoma tena. Chukua Biblia yako na kusoma maisha ya Paulo katika kitabu cha Matendo. Soma kitabu hiki chote! Wakati unapojiandaa kufundisha, fikiria tena masomo haya na mafunzo tuiyojifunza kwa kusoma habari za maisha ya Paulo.

Bila shaka utataka kuomba wakati unapojiandaa kufundisha ili Bwana ataweza kukutumia wewe kuwasaidia wanafunzi wako waweze kufahamu vyema mfano wa Paulo wa kuishi maisha mema ya Kikristo. Ingawa miaka mingi sana imekwisha kupita tangu Paulo alipofanya safari zake, bado tunaweza kufuata mfano wake wa kueneza injili. Tambua mfano huu ambao Paulo alitwekea sisi sote. Kusudi la somo hili ni kuonyesha tena ya kwamba Mungu atatugeza kuwa wafuasi wake waaminifu.

MAMBO YA KUKAZA

Somo hili la marudio linakaza mambo manne muhimu.

1. Hatua yetu ya kwanza kwa wokovu ni kuacha maisha yetu ya dhambi na kupokea maisha mapya katika Bwana.

2. Kwa kumpa Kristo nafasi ya kwanza maishani mwetu, tunaweza kumwamini kutulinda na kushiriki upendo wake na wengine.

3. Hata wakati wa mateso na udhalimu, inatupasa kuwa na nia ya kumshuhudia kila mtu nguvu za Yesu Kristo za kutuokoa.

4. Kila ahadi ya Bwana itatimizwa kama tukiwa na imani ya kutaka ahadi hizo na kufuata mapenzi ya Mungu kwa maisha yetu.

KULIFUNDISHA SOMO

Somo hili la marudio limefanywa kuwa kama maarifa ya kujifunza. Kwa kujifunza na kurudia masomo yaliyopita juu ya Paulo, wanafunzi watakabiliwa na mafunzo muhimu ya Kikristo ambayo yatastawisha maisha yao. Wanaposoma mambo haya mafupi ya ajabu katika maisha ya Paulo wataweza kupata maana hiyo. Tumia mikazo hiyo minne iliyoandikwa hapo juu kuhusu kila somo, na uwasaidie wanafunzi kutafuta kweli za Biblia wakati wanapotenda kazi ya kufanya. Watie moyo sikuzote kwa kuwasaidia kukumbuka mambo ambayo wamekwisha kujifunza. Watakuwa na tamaa ya kutimiza kila sehemu ya kazi yao ya kufanya.

KAZI YA KUFANYA

"Nilikuwa njiani kwenda Dameski kuwatessa Wakristo. Kwa ghafla nuru kutoka mbinguni ikaniangaza kote kote na kumtofusha macho. Sauti ilinika kwa jina langu la Kiyahudi na kusema, 'Sauli, Sauli, mbona wanituhii?' Sauti hii ilikuwa ya Bwana aliyekuwa na kazi aliyotaka nifanye. Ni hapa ndipo nilipogeuka

watendeeni mema wale ambao wawachukia ninyi." Luka 6:27

Yesu ndiye aliyesema maneno haya. Aliwapenda maadui zake. Alikwenda huku na huko akiwasaidia watu ambao hawakumwamini. Anajua kwamba kulipiza kisasi si kuzuri tena hakuleti furaha, kwa hivyo ni bora kwetu kuwapenda maadui zetu.

WAKATI WA KUFUNGA

Mtu akiwa anakuchukia na kukutendea kama adui, utafanya nini? Ni jambo la kawaida kwako kumfikiria mabaya. Ni jambo la kawaida kwako kutaka kumlipiza kisasi. Labda unaweza kumwombea apatwe na jambo fulani baya, kama kupata shida shuleni au kutopendwa tena na marafiki zake wengine.

Sura ya Kumi na Tatu

SOMO LA MARUDIO

MASOMO YA BIBLIA: Maandiko yote ya masomo ya kitabu hiki

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Hili ndilo somo la mwisho juu ya Mtume Paulo. Kutokana na masomo yote ya kitabu hiki ambayo tumejifunza, tumemwona Paulo jinsi alivyokuwa kuanzia alipokuwa

Hayo ni mawazo ya kawaida, lakini ukiwa Mkristo, umekwisha kugeuka kabisa kama Paulo alivyofanya na kuacha mawazo kama hayo. Humtendei mabaya mtu anayekuchukia. Yesu amekwisha kukupa asili mpya inayotaka kufikiri na kuwaza na kutenda kama Yesu alivyofanya wakati alipokuwa hapa ulimwenguni. Yesu anaweza kukusaidia kuwapenda adui zako badala ya kuwachukia. Anaweza kukusaidia kuwa na nia ya kumwombea adui yako.

Je! utamwomba Bwana kukusaidia kumtii kwa kuwapenda na kuwa mwema kwa maadui zako? Funga kwa maombi ili wanafunzi wako watakuwa na moyo wa kusamehe na kuwapenda wote ambao wanawachukia.

Mungu alitaka kutumia Paulo kuwafundisha watu habari za Kristo. Alijua ya kwamba Paulo alikuwa na elimu nzuri na angeweza kusema na watu wa nchi nyingine. Mungu akamgeuza Sauli. Alimsamehe dhambi zake akamtumia kuwapelekea watu wa Mataifa Neno la Kristo.

Masomo juu ya safari za Paulo ni ya kupendeza. Alipatwa na mambo mengi. Mengine kati ya mambo hayo ni mazuri na mengine ni mabaya. Tunajifunza kwamba ugeuzi wa Paulo ulimletea mabadiliko kamili katika roho yake na katika maisha yake. Kusudi la somo hili ni ya kwamba

Sura ya Kwanza

UGEUZI KAMILI

Mungu anaweza kutugeuza sisi kama alivyomgeuza Sauli.

MAMBO YA KUKAZA

1. Ni muhimu kuwaonyesha wanafunzi wako ya kuwa Sauli alibadilika kabisa baada ya kupokea Kristo kama Mwokozi wake.

2. Tukimwamini Kristo, Mungu atabadilisha mawazo yetu juu ya watu wengine.

3. Mungu hubadilisha mambo tunayotaka na yale tunayotaka kufanya.

KULIFUNDISHA SOMO

Paulo ni jina la Mkristo shujaa ambaye tutajifunza habari zake. Alikuwa Myahudi na alizaliwa katika mji ulioitwa Tarso. (Waambie vijana kutafuta mji huo wa Tarso katika ramani.) Wazazi wake walikuwa watu wema, na walimwamini Mungu. Paulo (kwa wakati ule alikuwa akiitwa Sauli) alikua na kumwamini Mungu mmoja tu wa kweli. Labda wazazi wake walikuwa washonaji hema na Sauli alijifunza kwao kushona hema. Alipokuwa kijana alikwenda shuleni Yerusalemu kujifunza sheria za Wayahudi.

Hata siku moja Sauli alipokuwa Yerusalemu, alisikia habari za Kristo. Watu wengi walikuwa wakiamini ya kwamba Yesu Kristo alikuwa Mwana wa Mungu. Sauli alimpenda Mungu,

na alitaka kumpendeza. Alifikiri kwamba ilikuwa makosa kwa mtu yeye kusema ati Kristo alikuwa Mwana wa Mungu. Alikwisha kujifunza sheria za Agano la Kale, na alidhanja kuwa Mungu angemtaka kuwadhhibu watu waliosema Kristo alikuwa Mwana wa Mungu. Wakati wote wote alipowapata watu waliomwamini Kristo, aliwakamata na kuwaweka gerezeni, kisha akawapiga.

Wakati ambapo Stefano alipigwa kwa mawe, Sauli alikuwapo alitazama, tena yeye ndiye aliyetunza nguo za watu wale waliomtupia Stefano mawe. (Wanafunzi wasome Matendo 7:58.) Baada ya Stefano kufa, Sauli alikwenda nyumba za Wakristo wengi, akawatoa nje na kuwafunga gerezeni.

Kuhani mkuu na watawala pia walifikiri kwamba Sauli alikuwa akitenda haki kwa kuwadhhibu Wakristo. Wakati Sauli apowaomba rubusa kwenda Damaski kuwakamata Wakristo wa huko, walitirahi sana kumruhusu kwenda.

Mji wa Damaski ulikuwa maili 130 hivi kaskazini mashariki ya mji wa Yerusalemu. (Waanibie wanafunzi kutafuta Yerusalemu na Damaski katika ramani.) Kulikuwa na Wakristo wengi sana Damaski, na Paulo alitaka kuwakamata na kuwaleta wengi sana Yerusalemu kama aliyoweza, na kuwadhhibu. Aliwachukua watu pamoja naye ambao wangependelea wafungwa.

Hata siku moja mchana, baada ya Sauli kusafiri siku kutoka Yerusalemu,



alitakaribia mji wa Damaski. Hakutaka kupumzika wakati ule wa jua kali, bali alijiharakisha kwenda. Kwa ghafla, nuru kutoka mbinguni ilimwagaza kote kote. Yeye pamoja na watu wale aliokuwa nao walianguka chini. Sauli alisikia sauti ikimwita jina. Alituliza ni nani yule aliyelitika jina lake. Bwana akamjiibu, "Mimi ndimi Yesu unayenitidhi." (Matendo 9:5) Pia alimwambia Sauli kusimama na kuingia katika mji wa Damaski mpaka kwa nyumba ya mtu mmoja aliyetwa Yuda, na pale ndipo angecambiwa jambo la kufanya. Paulo hakuweza kuona kwa sababu nuru ile ilipofusha macho yake. Watu wale waliokuja pamoja naye, walimsika mkono wakamwongoza mpaka kuingia mjini.

Pauluwapo Damaski Mkristo mmoja aliyetwa Anania. Mungu alisema naye katika maono

alikamatwa na kupelekwa Rumi kama mfungwa, na muda mfupi baadaye alihukumiwa kufa na Nero mfalme mwovu.

Jei huu ulikuwa mwisho wenye huzuni kwa mtume Paulo? La, kwa sababu tunajua ya kwamba baada ya kufa kwake hapa ulimwenguni alingia mara mbinguni na kukaa pamoja na Bwana wa ajabu.

KAZI YA KUFANYA

Mungu aliokea tena maisha ya Paulo. Wakati huu alimwoko Paulo katika bahari iliyochafuka na kuvunja merikebu walioyokuwa wakisafira. Baada ya muda mfupi Paulo na abiria wengine walitambua kwamba walikuwa katika kisiwa cha Melita. Piga mistari chini ya majibu ya kwele ya maswali yafuatayo.

1. Hali ya hewa ilikuwaje? ya moto kidogo ya nywa na baridi
2. Wenyaji walikuwaje wakarimu kwa watu wale waliotoka melini? Walivashia moto.
3. Ni kitu gani kilicho-mzonga-zonga Paulo mkononi? ndege nyoka
4. Watu walipoona kitu hiki kilizonga-zonga mkononi mwa Paulo, Je! walifikiri Paulo alikuwa nani. mchawi mwajaji
5. Walipoona kwamba hakuna dhara lo lote lililompata Paulo, walimfikiri kuwa nani? mwajaji

mungu malaika

Paulo alishukuru sana kwa ajili ya ukarimu wa wenyaji wale. Andika majibu ya maswali yafuatayo:

1. Je! Paulo alifanya Publio, mkuu wa kisiwa hiki, jambo gani? Alimponya babaye.

2. Je! Paulo aliwafanya wengine waliokuwa katika kisiwa hiki jambo gani? Aliwaponya wagoniwa wao.

3. Wenyaji waliwapa Paulo na wenzake vitu gani wakati walipokuwa wakiondoka. zawadi na vitu waliyohitaji

Paulo aliwaambia Wayahudi wa Rumi sababu iliyomfanya kuwa huko. Kata maneno yaliyo katika alama hii () ambayo Paulo hakuwaambia Wayahudi wale.

"Sikuifanya neno kinyume cha watu wetu. Lakini nilielewa kama (mfungwa) ~~(mtume)~~ kutoka (~~Bendari~~ ~~Mstari~~) (Yerusalemu), nikatiwa katika mikono ya (~~Weywanti~~) (Warumi) Waliponiuliza- uliza, hawakuona sababu yo yote kwangu kuuawa, lakini kwa sababu (~~Weywanti~~) (Wayahudi) walimchukua, na kusema maneno yasiyo ya kwele juu yangu, nilitaka rufani kwa Kaisari. Niliwaita niwazone na kusema nanyi kwa sababu (nimefungwa kwa minyororo) (~~taitechithwa~~ ~~kertenti~~) kwa ajili ya Kristo ambaye ni tumaini la Israeli."

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Lakini nawaambia ninyi mnaosikia, wapendani adui zenu,



kukaa Rumi kwa siku tatu, aliwaita wakuu wa Wayahudi pamoja kuwaeleza sababu ya kuletwa kwake Rumi kama mfungwa. Waulizwa wanafunzi wako kama wanajua sababu iliyomfanya Paulo kuletwa Rumi. Wape wakati wajaflhane jambo hilo. Jibu ni kwamba Paulo alikuwa ametaka rufani kwa Kaisari kwa sababu wakuu wa Wayahudi mjini Yerusalemu walitaka kumfunga bure bila sababu yote maalum kulingana na sheria ya Kirumi. Pia Paulo alijua kwamba ilikuwa mapenzi ya Mungu kwake kwenda Rumi, na labda hii ndiyo iliyokuwa njia ambayo Mungu alikuwa akitimiza mapenzi hayo yake.

Wakuu hawa wa Wayahudi walimwambia Paulo ya kwamba hawakupata barua zo zote zenye habari zake, wala hawajasikia habari au neno lo lote baya juu yake. Walimwambia ya kwamba walitaka kusikia maoni yake kuhusu imani ya

Kikristo. Paulo aliagana nao siku ambayo wao wangekuja kumtembelea nyumbani mle alimokuwa akikaa. Siku hiyo ilipofika, walikuja kwa wingi, na kutoka asubuhi hadi usiku aliwaeleza kwa utaratibu na kuwashuhudia mambo yaliyofundishwa na Agano la Kale juu ya Kristo.

Wengine kati yao waliamini maneno ya Paulo kuwa ni ya kweli na wengine hawakuyaamini. Kulikuwa na hali ya kutopatana kati yao, kisha wakaoondoka, wakaenda zao. Paulo alijaribu kuwashawishi ya kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zao, na kwamba Kristo ndiye aliyeikuwa Mwana wa Mungu aliyeabidiwa Wayahudi. Soma Matendo 28:28 kuona mambo ambayo Paulo aliwambia mwishowe.

Paulo alikuwa bado mfungwa, lakini alikuwa akikaa katika nyumba aliyopanga kwa pesa zake mwenyewe. Alikuwa bado yuko chini ya ulinzi, lakini alikuwa na uhuru wa kuwakaribisha wageni wakati wote. Aliwakaribisha watu wote waliokuja kwake na kuwahubiria ufalme wa Mungu na kuwafundisha habari za Bwana Yesu Kristo. Hakuna mtu aliyenzuia kufundisha hayo.

Wataalamu wengi wa Biblia wanaamini kwamba aliachiliwa huru baada ya miaka hii miwili. Alikwenda katika nchi nyingine na kuhubiri tena kama mtu huru. Wataalamu wa Biblia pia wanafikiri ya kwamba baadaye Paulo

akamwambia kuondoka kwenda katika njia iliyoitwa Nyofu na kuingia nyumba ya Yuda na kuuliza pale kama kuna mtu aitwaye Sauli. Mungu alimwambia Anania kuwaka mikono yake juu ya Sauli ili angeweza kuona tena. (Uliza:) Je! unafikiri kwamba Anania aliogopa? Ndiyo. Anania aliogopa kwa sababu alikuwa amekwisha kusikia habari za Sauli jinsi alivyowatesa Wakristo. Mungu alimwambia Anania kwenda kumwona Sauli kwa sababu alikuwa amemchagua Sauli kuwambia watu habari za Kristo. Anania aliondoka akaenda nyumbani mwa Yuda, akamwekea Sauli mikono. Alimwambia Sauli ya kwamba Bwana Yesu alikuwa amentuma kwake, amwekee mikono ili apate kuona tena. Pia alimwambia Sauli ya kwamba angejazwa Robo Mtakatifu. Alipomwekea Sauli mikono, Sauli aliweza kuona tena mara moja, akasimama, akabatizwa.

Kabla ya Sauli kuweza kutumiwa na Mungu ilimbidi kugeuzwa na kumpokea Kristo. (Uliza:) Je! unafikiri Sauli aligeuzwa na kuwa

Mkristo? (Uliza:) Aligeuka kwa njia zipi? Sauli alitaka sasa kufanya mambo yaliyompendeza Mungu. Hakutaka kuwatesa Wakristo tena. Kuanzia hapo alitaka kuwambia wengine habari za Kristo kama Mwokozi wake.

Masomo mengine yajayo yatahusu mahali na jinsi Sauli alivyomtumikia Kristo.

KAZI YA KUFANYA

Jaza nafasi katika sentensi hizo hapo chini kwa maneno yanayofaa.

1. Sauli aliwachukia Wakristo.
2. Sauli alifikiri kwamba alikuwa akimsaidia Mungu kwa kuwaaadhibu Wakristo.
3. Sauli alipokuwa njiani kwenda Dameski alipofushwa.
4. Je! kulifanyika nini wakati Anania alipomwenda Sauli nyumbani mwa Yuda? Anania aliwaka mikono yake juu ya Sauli na akapata kuona tena. Alijazwa na Robo Mtakatifu. Alibatizwa.



5. Sauli alitaka kufanya nini baada ya kugeuzwa kuwa Mkristo? Alitaka kuwaambia watu wengine habari za Yesu.

Jibu sentensi zifuatazo kwa kuandika ferufi "K" kando ya zile ambazo ni kweli, na kuandika herufi "M" (makosa) kando ya zile ambazo si kweli.

K 1. Kwanza, Sauli aliwachukia Wakristo.

M 2. Kristo alisema na Sauli akiwa njiani kwenda Antiokia.

K 3. Sauli aliancha dhambi na kumfuata Mwana wa Mungu.

M 4. Anania hakwenda kumsaidia Sauli.

K 5. Sauli alibatizwa.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Tubuni basi, mrefee, ili dhambi zenu zifuuwe." Matendo 3:19a

Kama maelezo ya kifungu cha kukumbuka, unaweza kusema ya kwamba Sauli alipokuwa njiani kwenda Dameski aliacha dhambi zake na kumpokea Mwana wa Mungu. Aligeuzwa kuwa Mkristo na fikira zake pia zikabadilika. "Kugenkwa" maana yake ni kuacha njia uliyokuwa ukifuta, na kupitia njia nyingine. Ikiwa Kristo ndiye Mwokozi wako, basi dhambi zako zimesamehewa na kusahuliwa. Sasa unafuata njia mpya katika fikira zako

na katika matendo yako. Mungu hubadilisha mawazo yako juu ya wengine; hubadilisha mambo unayotaka (ya anasa), na yale unayofanya ambayo si mazuri.

WAKATI WA KUFUNGA

Mwalimu, jilize wewe mwenyewe swali hili: Je! Kristo amebadilisha maisha yangu kwa njia ipi? Je! vijana ninaowafundisha wanaweza kumwona Kristo ndani yangu? Pia, uwalize wanafunzi ambao wamekwisha kumpokea Kristo kuwa Mwokozi kama Kristo huyo amegeuza maisha yao. Jinsi maisha ya Paulo yaliyogeuzwa, ndiyo kila maisha yanavyoweza kugeuzwa. Roho Mtakatifu ataingia katika roho, na kila maisha yatageuzwa kuwa bora na yenye furaha zaidi. Uwalize wanafunzi wako kuombeana wao wenyewe na kumwomba kila mmoja ili Kristo atakuwa mwokozi wa kila mwanafunzi.

Funga darasa kwa maombi. Uwalize wanafunzi kama kuna ye yote kati yao ambaye angependa kuongoza kwa maombi. Usiwalazimisha kuomba. Wanapaswa kuomba kama wao wenyewe wanataka. Ikiwa hakuna ye yote anayetaka kuomba kwa sauti, basi unaweza kufunga kwa maombi.

Ndiyo, ni mwujiza wa Mungu. Mungu alikuwa akimlinda Paulo.

Publio ambaye alikuwa mkuu wa kisiwa hiki, alikuwa na nyumba karibu na mahali pale ambapo abiria wa merikebu ile iliyovunjika walifika nchi kavu. Publio alikuwa mkarimu sana kwa watu wote waliokuwa pamoja na Paulo. Paulo alipata nafasi ya kulipiza ukarimu huo wake. Babaye Publio alikuwa mgong'wa sana. Paulo alimtembelea, akamwomba, kisha akamwekelea mikono, akamponya. Kisha wagonjwa wote wa kisiwa hiki walimjia Paulo na wote wakaponywa.

Je! wenyeji wa kisiwa hiki walionyesha jinsi gani shukrani yao kwa mambo yote ambayo Paulo aliwafanyia? Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 28:10.

Yulio na askari zake na walingwa walika katika kisiwa hiki kwa muda wa miezi mitatu wakingoja wakati mzuri wa kusafiri. Wakati huo ulipofika, walingia katika merikebu ya Iskanderia iliyokuwa ikienda Italia. Kisha walikwenda Regio na baada ya siku moja upepo wa kusini ulivuma, na siku ya pili wakawasili Puteoli iliyokuwa bandari ya Italia.

Walika Puteoli siku saba kabla ya kwenda Rumi. Paulo aliwona ndugu Wakristo katika bandari hiyo. Alikuwa hajapata kuwona, lakini walikuwa ndugu zake kwa sababu wao pia walimpenda Bwana Yesu Kristo. Puteoli ndiyo iliyokuwa bandari kubwa na merikebu zote zilizokuja katika sehemu hii ya Italia

zilisimama hapa na kupakua ngano au bidhaa zote walizolea. Abiria waliweza kushuka na kwenda katika sehemu zo zote za nchi hii waliotaka kwenda.

Wakati Paulo alipokuwa Puteoli, Wakristo wa Rumi walisikia habari ya kwamba alikwisha kuwasili Italia. Paulo hakuwajua Wakristo hawa, lakini alikuwa amekwisha kuwaandikia barua. Walingua na walikwisha kusikia habari za safari zake za kuwapelekea Wayahudi na watu wa mataifa Injili ya Kristo. Wakristo wa Rumi walimthibitisha Paulo ya kwamba walikuwa na tamaa juu ya kuja kwake kwa sababu waliembea mwendo mrefu kwenda kumtaka. Wengine kati yao walimlaka katika umbali wa kilometa sitini na tano kutoka Rumi. Wengine walimlaka karibu na Rumi. Paulo alitiwa moyo kujua ya kwamba Wakristo hawa walikuwa pale.

Je! Yulio aliwafanyia walingwa wake jambo gani wakati walipofika Rumi? Walingwa wote isipokuwa Paulo walikabidhiwa mikononi mwa akida wa ulinzi. Paulo aliruhusiwa kukaa peke yake pamoja na askari mlinzi, lakini hakuwa huru kwenda mahali po pote alipotaka. Alifunga na minyororo. Luka na mwezake ambao walisafiri pamoja na Paulo katika safari hii walikuwa huru kumtimizia Paulo mahitaji yake, na wageni wengine wangeweza kumwona wakati wo wote waliotaka. Paulo hakupoteza dakika hata moja akifikiri juu ya mateso au shida zilizokuwa zikimkabili. Baada ya

MAMBO YA KUKAZA

1. Kabla ya ugeuzi wa Paulo, alivachukia wale ambao hakupatana nao.
2. Paulo alionyesha upendo wa Kristo kwa wenyeji wa kisiwa cha Melita na kwa wakuu wa Wayahudi mjini Rumi, na kwa wale waliomfanya kufungwa gerezeni.

KULIFUNDISHA SOMO

Je! tulipokutana na Paulo mara ya kwanza, maadui zake walikuwa nani? Walikuwa Wakristo. Alifikiri kwamba walikuwa wakifanya kosa kwa kumwabadu Mungu kwa Yesu Kristo. Baada ya Paulo kugeuka kamili na kuwa Mkristo, alianza kuwa na maadui wengine wapya. Maadui hawa walikuwa wakuu wa Wayahudi ambao walikuwa marafiki zake kabla ya ugeuzi wake. Sasa wakuu hawa walitaka Paulo auawe. Ilionekana kwao kana kwamba Paulo alijiunga na maadui zao.

Ilimbidi Paulo sasa kujibu swali hili moyoni mwake. "Je! niwatende jinsi watu wanaonichukia?" Hili ndilo swali lililombidi Paulo kujibu. Je! ni mtu gani aliyemwekea Paulo mfano wa kufuata? Ni Kristo. Alikuwa mwema kwa wale waliomchukia na kumtesa.

Tunajua kutokana na somo lililopita kwamba Paulo na kila mmoja aliyeikuwa ndani ya merikebu walifika salama katika nchi kavu. Kisiwa kile walichofika kilitwa Melita. Waambie wanafunzi watafute

kisiwa hiki katika ramani zao. Hali ya hewa ilikuwa baridi na mvua nyingi, na ilikuwa jambo jema sana kwa abiria wale kuona moto ule uliowashwa. Paulo na wengine walisaidia kukusanya mzigo wa kuni wa kuweka motoni.

Paulo alikuwa na ukuni mkononi mwake, na alipouweka motoni, mara nyoka ilitoka ndani yake, ikamzonga-zonga mkononi.



Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 28:4 kuona jambo ambalo watu wale walimfikiria Paulo walipoona nyoka akilewalewa mkononi mwake. Paulo alimtukusha nyoka kutoka mkononi mwake, na hakupata dhara lo lote. Je! watu walimfikiria Paulo nini sasa? Walifikiri kwamba alikuwa Mungu. Je! unafikiri ni nini kilichomzuia Paulo kuumwa na nyoka yule?

Sura ya Pili

KUMPA KRISTO NAFASI YA KWANZA

MASOMO YA BIBLIA: Matendo

9:23-31; 11:20-26; 13:1-3; 14

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Katika mafunzo haya juu ya Paulo, utasoma ya kwamba alikaa katika miji kadha kwa muda. Katika kila mji kulifanyika jambo la kupendeza. Labda wanafunzi wako watataka kutafuta miji hii katika ramani. Hakikisha kwamba umetafuta miji hii katika ramani wakati unapotayarisha somo hili ili uweze kuwasaidia wanafunzi wako.


Katika somo lililopita tulijifunza ya kwamba Paulo aligeuzwa kuwa Mkristo. Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wanafunzi kuelewa ya kwamba Paulo alionyesha ugeuzi wake kuwa ni halisi kwa kujitoa hasa kwa Kristo na kwa kuwasaidia wengine kumpokea Yesu kama Mwokozi wao.

MAMBO YA KUKAZA

1. Kazi ya Paulo ya umisheni inaanza.
2. Mateso yanaenea katika Ikonio.
3. Paulo awatembelea Wakristo wapya.

KULIFUNDISHA SOMO

Paulo, mwamini mpya, alitumia wakati wake wote katika kushiriki habari njema na wengine. Baada ya



kuhubiri kwa muda katika Dameski, viongozi fulani wa dini walipanga kumkamata. Waambie wanafunzi kusoma 2 Wakorintho 11:32-33. Paulo alifahamu mipango yao na alijua kwamba askari walikuwa wakilinda mlango wa mji. Nyakati zile miji mingi ilikuwa na kuta. Kuta nyingine zilikuwa pana zaidi hata nyumba zilizengwa juu yao. Marafiki fulani wa Paulo walimsaidia kutoroka mle mjini kwa kumweka ndani ya kapu kubwa na kumtelemsha katika dirisha la ukutani.

Kisha Paulo alikwenda Yerusalemu. Baadaye Paulo akaenda Kaisaria, mji uliokuwa katika pwani, kutoka pale alingia


merikebuni, akasafiri mpaka Tarso, mjiimi kwao.

Katika wakati ule waamini wengine walikwenda Antiokia wakaanza kuhubiri habari za Bwana Yesu Kristo.

(Tafuta Antiokia katika ramani). Mtu mmoja aliyeitwa Barnaba alikuwa mmoja wao. Alijua kwamba alihitaji mtu kumsaidia kwa kazi ya kanisa ilie lililokuwa linaendelea. Alimkumbuka Paulo na jinsi alivyompenda Bwana sana. Basi aliondoka akaenda Tarso akamchukua Paulo akaja naye. Yeye na Paulo walifanya kazi Antiokia kwa muda wa mwaka mmoja.

Siku moja Roho Mtakatifu aliwaongoza viongozi wa kanisa kuwatuma Paulo na Barnaba kwenda nchi nyingine kama wamisheni, kuwahubiria watu. Mahali mojawapo ambapo Paulo na Barnaba walikwenda paliitwa Ikonio. Katika mji huu, Paulo na Barnaba waliingia sinagogini kwa ushujaa, wakawahubiria watu. Wayahudi wengi na Wayunani waliamini mahubiri yao, wakampokea Kristo kama Mwana wa Mungu na Mwokozi wao. Pia kulikuwapo watu wengi ambao hawakuwaamini na waliotaka waondoke. Waambie wanafunzi kusoma Matendo 14:4-6.

Paulo na Barnaba walikwenda Lистра. Watu wa mji huu (wa Lистра) waliabudu sanamu, na waliamini kwamba walishi chini wa ulinzi wa mungu waliitwa Hermie. Paulo alianza kuwahubiria watu hawa, na



akamwona mtu mmoja kiwete aliyependeza sana na maneno Paulo aliyokuwa akisema. Paulo alimwona kiwete huyo kuwa ana imani, basi akamwambia kwa sauti kubwa, "Simama kwa miguu yako." Kiwete huyo alisimama, akaweza kutembea. Huu ulikuwa mwujiza ambao Paulo alifanya. Mungu alikuwa akifanya kazi yake kwa Paulo. Mtu huyu alikuwa kiwete tangu tumboni mwa mamaye, na sasa alikuwa akitembea. Watu walidhania ya kuwa Paulo na Barnaba walikuwa mungu wale wao (Yaani Hermie na Zeu), na kwamba walikuwa wameshuka duniani. Walitawala Paulo na Barnaba sadaka za kuteketeza na taji za maua. (Matendo 14:13) Paulo na Barnaba hawakupenda jambo hili kwa sababu walitaka watu kumwabudu Mungu wa kweli. Walitawambia watu hao, "Sisi nasi tu wanadamu hali moja na ninyi." Walitawambia habari za Mungu wa kweli aliye hai, ambaye alitamba

Mungu alikuwa amemwahidi Paulo ya kwamba angefika Rumi. Mungu aliahidi kwamba abiria wote waliokuwa ndani ya merikebu wangekuwa salama. Paulo alishawishika kabisa ya kwamba Mungu angetimiza ahadi yake. Mungu hutimiza ahadi yake siku zote.

WAKATI WA KUFUNGA

Katika hadithi hii juu ya Paulo, tunajifunza tena juu ya imani thabiti

aliyokuwa nayo. Tunaona tena jinsi Paulo alivyokuwa Mkristo imara. Alikuwa na ahadi za Mungu na kuziamini. Aliendelea mbele na mipango ambayo alijua kwamba ilikuwa mapenzi ya Bwana. Ahadi za Mungu ni kwetu sisi sote.

Funga kwa maombi ili wewe na wanafunzi wako mtakuwa na imani thabiti katika ahadi za Mungu.

Sura ya Kumi na Mbili

JINSI YA KUWATENDEA MAADUI

MASOMO YA BIBLIA: Matendo 28

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Somo hili juu ya Paulo linaonyesha jinsi Paulo alivyokuwa na moyo wa upendo kwa wale waliokuwa maadui zake. Itakuwa muhimu kwako kuwaongoza wanafunzi kufahamu kwamba Kristo aliwapenda watu wote hata wale ambao walimchukia. Kristo aliwaomba wale walimsultisha msalabani. Paulo alionyesha upendo kwa wale waliomfunga gereza ni na ambao hawangeweza kuamini ujumbe wake wa Kristo.

Katika ulimwengu huu wetu wa sasa, kama vijana hawa ndio wataokuwa viongozi wa kesho, wajifunza upendo wa Kristo kwa watu wote, kisha ulimwengu wote ukawa mahali pema pa kukaa. Zungumza na wanafunzi wako juu ya kuwapenda watu wale wanaowafikiria kwamba wanawachukia. Waruhusu kujadiliana pamoja nawe shida hii.

Kusudi la somo hili ni kuongoza wanafunzi wako kukata shauri kupenda na kuwaomba wale wanawachukia. Waambie ya kwamba Kristo aliye ndani ya roho zao anaweza kuwajaza mawazo yake ya upendo.

KAZI YA KUFANYA

Paulo alikaa kifungoni kwa muda zaidi ya miaka miwili. Sasa walisafiri kwenda Rumi kuhukumiwa na Kaisaria. Yeye pamoja na wafungwa wengine walikabidhiwa mikononi mwa Yulio aliyekuwa akida wa Kirumi. Paulo alimwambia mwenye merikebu wasisafiri.

Chora miringo kwa picha ya nanga iliyo mbele ya sentensi ya kweli:

Mwenye merikebu alichagua kutumia wakati wa baridi katika Bandari Nzuri kama Paulo alivyomwambia kufanya.



Ingawa Paulo alionywa kwamba ingekuwa hatari kuendelea na safari, mwenye merikebu alisafiri kwenda Foinike.



Paulo alimwambia mwenye merikebu kuendelea na safari mara tu upepo wa kusini ungeanza kuvuma.

Piga mstari chini ya jibu la kweli la kila swali hapo chini.

Merikebu haikuweza kushindana na upepo. Je! mabaharia walifanya nini?

Walisafiri kwenda nchi kavu.

Waliacha kuchukuliwa na upepo.

Katika kisiwa cha Kanda walipitisha kamba chini ya merikebu ili iishikanishe pamoja. Walipunguzaje uzito wa merikebu?

Walitupa vyombo vya merikebu baharini.

Walitupa nanga nyingine baharini.

Angalia jinsi Paulo alivyoweza mfanano mzuri melini. Kata maneno yote yasiyo kweli katika alama hii () :

Paulo aliwasilihi abiria kula (chakula) (~~dawa~~). Walikuwa hawajakula kitu kwa muda wa (~~siku~~ 2) (siku 14).

Paulo alitwaa (mkate) (~~keli~~) akala. Walipokwisha kula wote na kushiba, walitupa (ngano) (~~mizigo~~) baharini ili kupunguza shehena.

Chora miringo kwa herufi "K" iliyo kando ya sentensi ya kweli na uchope miringo kwa herufi "M" kando ya sentensi ambayo si kweli.

K M Kulipokucha walitambua nchi waliyotumainia kufika.

K M Mavimbi yalinua merikebu yakaipeleka ukingoni mwa nchi kavu.

K M Kulikuwa na watu wachache ambao hawangeweza kujifikisha nchi kavu salama.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyohidi."

Warumi 4:21

mbingu na nchi na vitu vyote vilivyomo ndani yake.

Maadui wengine wa Paulo walifika Listra kutoka Ikonio. Waliwaambia watu uwongo mwingi juu ya Paulo na Barnaba. Kisha watu wakawaamini watu hawa badala ya kumwamini Paulo na Barnaba. Walimpiga Paulo kwa mawe, wakamburuta nje ya mji, wakamwacha pale wakidhania ya kuwa alikwisha kufa. Paulo alisimama akaingia tena mle mjini, kisha yeye na Barnaba wakaondoka, wakaenda Derbe. Waambie wanafunzi kutafuta miji ya Ikonio, Listra, na Derbe katika ramani.

Katika mji wa Derbe, Paulo na Barnaba walivuta watu wengi sana kwa Kristo. Walikuwa mashujaa kwa sababu baada ya wao kuhubiri Derbe, walirejea Listra na Ikonio kuona jinsi waamini wapya huko walivyokuwa wakiendelea.

Walikata shauri kurudi Antiokia, kwa hivyo walipitia mji wa Atalia uliokuwa katika Pwani, wakaabiri kwa merikebu mpaka Antiokia. Wakristo wa Antiokia, ambao waliwatuma katika safari hii ya umisheni, walifurahi kusikia mambo yote Mungu aliyoyafanya pamoja nao. Paulo na Barnaba waliwaambia mambo yote waliyoyafanya, wakitukuza Mungu kwa kuwavuta watu wengi kwa Kristo. Mwambia mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 14:27.

KAZI YA KUFANYA

Soma sentensi zifuatazo, kisha uweke alama hii (X) kando ya jibu sawa la kila sentensi.

1. Barnaba alimwuliza Paulo kuja kufanya kazi naye () Yerusalemu (X) Antiokia.
2. Paulo na Barnaba walingia wapi walipofika Ikonio? () sokoni (X) sinagogini.
3. Ni nani waliompokea Kristo kama Mwokozi wao? () Warumi (X) Wayahudi wengi na Wayunani.
4. Kiwete yule katika Listra aliponywa kwa sababu alikuwa na (X) imani () pesa.
5. Watu wa Listra walifikiri Paulo na Barnaba walikuwa (X) mungu () malaika.
6. Wakati Paulo na Barnaba waliporudi Antiokia, () walijisifu wenyewe (X) walimsifu Mungu.

Jaza nafasi katika sentensi zifuatazo:

1. Marafiki za Paulo walimweka ndani ya kapu wakamtelemsha ukutani ili apate kutoroka Dameski.
2. Paulo alirudi Yerusalemu alipotoka Dameski.
3. Mjini kwao Paulo uliitwa Tarso.
4. Paulo alitaka kushiriki neno la Kristo na wengine.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

Mwenende kama uliyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa; mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu. Wakolosai 1:10

WAKATI WA KUFUNGA

Vakristo hawachoki kuzungunza jua ya mabadiliko ambayo Kristo amekwisha kufanya maishani mwao. Mojawapo ya mabadiliko yale maishani mwa Paulo ni kwamba

Sura ya Tatu

KUIMBA GEREZANI

MASOMO YA BIBLIA: Matendo 16

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Furaha ambayo si furaha ya kwele, daima hutegemea mahali tulipo, watu tulio nao, au kitu tulicho nacho. Furaha ya kwele hupatikana kwa ushirika halisi na Bwana, na hutuwezesha kumsifu Mungu hata wakati ambapo mambo ya kidunia yanapokuwa katika hali tusiyopenda. Miaka mingi sana iliyopita, mtu mmoja alisema ya kwamba uti kamili kwa Bwana huleta furaha halisi. Utaona katika somo hili ya kwamba Paulo alikuwa na furaha kama hiyo.

alikuwa na mawazo mapya juu ya watu, tena alikuwa na tamaa ya kumwona Kristo akikaa maishani mwa watu. Paulo angaliweza kuwa mungu kule Listra kwa sababu Mungu alitumia yeye kumponya kiwete yule. Lakini hakutaka utukufu wa kuwa mungu kwa watu wale. Aliwataka kumjua Mungu mmoja wa kwele. Jambo hilo lilikuwa muhimu sana kwake. Sisi kama Wakristo, ni lazima tuone ya kwamba watu wanamjua Mungu na kumwamini Mwanawe kama Mwokozi wao. Funga darasa kwa maombi.

Watu wengi sana ulimwenguni ni wagonjwa, wengine ni vipofu, na wengine ni viwete. Kuna watu wasio na makao, wala hakuna mtu wa kuwatunza. Watu wengine hawana chakula. Je! watu kama hao wanaweza kuwa na furaha? Je! furaha inaweza kuwapo kama mambo yanaenda vibaya? Paulo aliyauona mambo yote kama yakimwendea vibaya, lakini katika somo hili tunaona jinsi alivyokuwa na furaha moyoni mwake.

Kusudi la somo hili ni kuonyesha kwamba furaha ya Paulo ya kiroho


hakuna mtu hata mmoja ambaye angenganiamia. Paulo akaamini ahadi hiyo. Alifanya mambo yote ambayo Mungu alimwonyesha kufanya ili kuokoa maisha yake mwenyewe na maisha ya wengine. Aliwazua kutoroka mabaharia ambao walilitajwa sana kuleta merikebu katika nchi kavu.

Malaika wa Bwana alikwisha kumwambia Paulo ya kwamba merikebu yao ingevunjika, na kwamba ingewabidi kugelea au kushikilia vipande vya mbao vya merikebu yao iliyovunjika ndipo wangeweza kufika katika nchi kavu.

Abiria wale waliokuwamo ndani ya merikebu walikuwa wachafu kwa sababu hawakula wakati wa dhorruba. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 27:33-34 kuona mambo ambayo Paulo aliwambia watu wale. Aliwasili kula. Kisha alitwaa mkate, akamshukuru Mungu mbele yao wote, akaumega, akaanza kula. Ndipo wao wote waliitwa moyo, wakala chakula wenyewe. Watu wote waliokuwa ndani merikebuni walikuwa mia mbili na sabini na sita. Walipokwisha kula wote na kushiba, walipunguza uzio wa merikebu kwa kutupa ngano baharini.

Mambo yalitanyika kama malaika wa Bwana aliyomwambia Paulo. Merikebu ilivunjika na kuangamia, lakini maisha ya kila abiria yaliokolewa. Kulipopambazuka, mabaharia waliona kwamba walikuwa karibu na nchi kavu. Waliona hori

yenye utuo ambapo walipanga kuingiza merikebu yao. Wakini, walifika mahali palipokutana bahari mbili na merikebu yao ikawama na tezi yake ikavunjika na mawimbi. Askari waliokuwa wakilinda wafungwa waliogopa ya kwamba pengine wafungwa wangeogelea na kukimbia, kwa hivyo walipanga kuwana. Kulingana na sheria ya Kirumi, askari ye yote aliyelinda mfungwa kama mfungwa huyo wake alikimbia, yeye ndiye angetukumiwa badala ya mfungwa huyo. Yulio, kwa sababu alitaka kumwokoza Paulo aliwazua kutimiza mipango hiyo yao. Aliwaamuru wale ambao wangeweza kugelea kujitupa baharini na kugelea kwenda nchi kavu, na wengine kushika mbao na kuelea hadi ufuni. Bwana alitimiza ahadi yake na kila mtu alifika salama katika nchi kavu.



WATU WOTE WAKAPATA KUFIKA NCHI KAVU SALAMA

Hakuna mtu hata mmoja mle merikebuni aliyekula kwa siku nyingi. Labda hawakuwa na tamaa ya kula kwa sababu ya mawimbi yale yaliyowarusha-rusha. Tena walishughulika sana na kuteka maji mle merikebuni na kumwaga baharini. Ndipo sasa Paulo alianza kuwaambia ya kwamba alikuwa na habari njema ya kuwaarifu. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 27:21-25 na kusema habari hiyo njema.

Paulo alitiwa moyo sana na maneno haya ya Mungu. Alitaka watu wote waliokuwa ndani ya merikebu ile kuamini ujumbe huu wa furaha. Ni kweli kwamba hapakuwapo tumaini lo lote kwao kuokoka. Basi, ingekuwa Paulo kuwaambia kufurahi na kuamini kwamba ingawa merikebu ingeangamia, maisha yao yangeokolewa?

Paulo alimjua Mungu. Alijua kwamba Mungu alipoahidi kitu, alitimiza ahadi hiyo yake hata wakati ambapo ulipodhaniwa kwamba hangeweza kuitimiza. Wakati Bwana aliposema na Paulo, upepo na mawimbi yalikuwa yamepiga-piga merikebu mpaka sasa ilikuwa katikati ya visiwa vya Kauda na Melita. Wasaidie wanafunzi wako kutafuta visiwa hivi. Viko chini ya ramani ya Italia.

Hata usiku wa kumi na nne ulipotimia tangu walipotoka Bandari Nzuri, wakiwa bado wanachukuliwa huku na huko na mawimbi baharini

na mabaharia walidhanja kwamba walikuwa wakikaribia nchi kavu. Labda masikio yao yalisikia mawimbi yakipiga-piga ufuni mwa bahari. Walipima kina cha mahali pale walipokuwapo, wakapata pima ishirini. Palionekana kuwa si mahali pa kina sana. Baadaye kidogo walipima tena na wakapata kina kumi na tano. Ilikuwa usiku na hawakujua kwamba ni kisiwa kipi kilichokuwa mbele yao. Labda merikebu yao ingechukuliwa na mawimbi na kugongwa kwenye miamba iliyokuwa ukingoni mwa bahari wakati wote. Kwa hiyo walitupa nanga baharini kuzuia merikebu isichukuliwe na mawimbi.

Mabaharia walidhanja kwamba wangeokoka kama wangekwenda nchi kavu kwa mashua dogo badala ya kukaa ndani ya merikebu. Walijifanya kana kwamba walikuwa wakishusha nanga nyingine baharini, lakini kumbe walikuwa wakishusha mashua dogo ili wapate kutoroka. Hawakujali maisha ya mtu mwingine ye yote ila maisha yao wenyewe.

Paulo alipoona kwamba mabaharia wale walikwisha kushusha mashua yale, alijua kusudi lao la kufanya hivyo. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 27:31 kuona jambo ambalo Paulo alifanya, na some Matendo 27:32 kuona jambo ambalo askari walifanya.

Wakati wote walipokuwa ndani ya merikebu walingojea kupambazuka, Paulo alitumia wakati huo vizuri sana. Mungu alikuwa ameahidi ya kwamba

ilimwezesha kumsifu Bwana hata wakati wa taabu. Omba kwamba tokeo la somo hili vijana watakuwa na tamaa ya kumsifu Bwana wakati wa huzuni na wakati wa furaha.

MAMBO YA KUKAZA

1. Paulo alimtii Bwana kwa kuhubiri Ulaya.
2. Bwana alimpa Paulo uwezo wa kumtoa pepo mchafu aliyekuwa ndani ya kijakazi.
3. Ingawa Paulo na Sila walipigwa na kufungwa gerezeni kwa sababu ya utumishi wao, waliimba nyimbo za kumsifu Mungu.
4. Mlinzi wa gereza na jamaa yake yote walimpokea Yesu kama Mwokozi na Bwana.

KULIFUNDISHA SOMO

Uliza: Je! mnakumbuka ni nani aliyesafiri pamoja na Paulo katika safari ya kwanza ya umisheni? (Barnaba) Uliza: Je! unaweza kukumbuka mambo fulani ya furaha ambayo yalimfanyikia Paulo? (Alisamehewa dhambi zake; alichaguliwa kuwa mmisheni wa kwanza wa Mungu kwenda nchi za kigeni; alianzisha makanisa; alifanya miujiza). (Uliza:) Je! unakumbuka mambo fulani ya huzuni ambayo yalimfanyikia Paulo? (Maadui katika Dameski walitaka kumwua; watu wa Ikonio walimchukia; katika Listra alipigwa kwa mawe akaachwa ikidhaniwa kuwa amekufa.)

Sasa tutazungumza juu ya safari ya pili ya Paulo ya umisheni. Katika safari hii Paulo alimchukua mtu mmoja aliyeitwa Sila, akaenda naye. Walianza safari kutoka Antiokia, na badala ya kusafiri kwa mashua, walitembea kwa miguu mpaka kwenye miji ambayo Paulo na Barnaba walikwisha kutembelea.

Katika miji wa Listra kulikuwa na kijana mmoja ambaye alipendewa na kazi ya Paulo na Sila. Kijana huyu aliitwa Timotheo. Paulo na Sila walimtaja Timotheo kwenda nao na kuwasaidia. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma 2 Timotheo 3:15 katika vifungu vya Biblia. Mwambie mwingine kusoma 2 Timotheo 1:5. Tangu Timotheo alipokuwa mdogo, alikuwa akijifunza maandiko ya Agano la Kale. Nyanya yake na mama yake walimpenda Mungu, na walimfundisha kumpenda Mungu na kumtii. Wakati Timotheo alipomsikia Paulo akieleza ya kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, na Mwokozi aliyeahidiwa, alimwamini Yesu kwa moyo wake wote.


Paulo na Sila na Timotheo walikwenda katika miji mingi ambayo Paulo alikwisha kuhubiri wakati wa safari yake ya kwanza ya umisheni. Waliwatia Wakristo wapya moyo kwendelea kuishi kwa njia impendezayo Bwana.

Wamisheni hawa watatu walikwenda katika nchi ambazo Injili ilikuwa bado kuhubiriwa mbeleni. Walikwenda katika miji mmoja ulioitwa Troa ambao ulikuwa katika

pwani. Hawakujua mahali ambapo Bwana aliwataka kwenda baada ya kutoka Troa. Waliomba kwa ajili hiyo, na ilipofika usiku wa manane, Paulo aliona maono. Katika maono hayo alimwona mtu aliyemwambia, "Vuka uje Makedonia utusaidie." (Matendo 16:9) Wanafunzi wako watatufe miji ya Troa na Makedonia katika ramani.

Kabla ya Paulo, Sila, na Timotheo kuondoka Makedonia, msaidizi mmoja mwingine alijiunga pamoja nao, jina lake Luka (yaani Daktari Luka). Luka ndiye aliyandika kitabu cha Matendo. Wote wanne waliabiri kwa mashua mpaka Makedonia. Kisha wakatia nanga katika mji wa Neapoli. Kutoka hapo walitembeka kwa miguu mpaka Filipi ambao ulikuwa mji mkuu wa sehemu ile ya Makedonia. Watu wengi waliokaa Filipi walikuwa Warumi.

Kulikuwa na Wayahudi wachache sana waliokaa Filipi kwa hivyo hapakuwapo sinagogi ambapo wangekwenda kuabudia. Uliza mmoja wapo wa wanafunzi wako kusoma Matendo 16:13 kuona mahali ambapo Wayahudi waliabudia siku ya sabato. Watu wote waliocabudu waliitwa wanawake. Paulo aliwambia habari za kuja kwa Mwokozi, Yesu Kristo; na wanawake walisikiliza na kuamini. Walikuwa wamekwisha kumwamini Mungu, na walijua manabii walisema ya kwamba Mwokozi angekuja siku moja. Mmoja kati ya wanawake wale alitwa Lida. Alimwamini Kristo akabatizwa. Pia aliwakaribisha Paulo



na wenzake kwake nyumbani kukaa naye wakati walipokuwa Filipi.

Kila siku ambapo Paulo na Sila walipokwenda katika mahali pa maombi, kijakazi mmoja aliwafuata. Uliza: Je! kuna mmoja anayefahamu maana ya kijakazi? Waambie: Alikuwa amenunuliwa na watu wengine, na aliwapatia watu hao faida kwa kuagua. Mambo aliyoyasema mara nyingi yalikuwa kwele, kwa hivyo watu walimlipa pesa ili awaaguc. Wakati alipokuwa akiwafuata Paulo na kundi lake, aliendelea kupiga kelele, akisema, "Watu hawa ni watumishi wa Mungu aliye juu, wenyewe kuwahubiria nja ya wokovu." Ingawa maneno hayo yalikuwa kwele, yaliscemwa na upepo mchafu alyekuwa ndani ya kijakazi yule. Pepo huyo alikuwa akiwazua watu kumfuata Bwana. Aliwakaribisha Paulo na Sila sana kwa siku nyingi. Mwishowe Paulo alimwambia,

Kutoka Sidoni walisafiri katikati ya Kipro na pwani ya Foinike, kisha wakaelekea upande wa magharibi kupitia pwani ya Kilikia na Pamfilia mpaka wakafika Mira. Je! wanafunzi wanatafuta safari hii katika ramani zao? Katika Mira, Yulio aliwapandisha wafungwa wake katika merikebu iliyotoka Iskenderia kwenda Italia. Merikebu hii ilikuwa imebeba ngano kutoka Misri. Baada ya kuondoka Mira walisafiri karibu na Nido, na kutoka Nido, merikebu ilipita bahari ya upande wa mashariki ya Krete, ikafika Badari Nzuri. Krete ilikuwa kisiwa na Bandari Nzuri ilikuwa kusini ya kisiwa hiki.

Hatuji ni kwa muda gani merikebu ilikaa katika Bandari Nzuri, lakini "Wakati mwingi" ulikwisha kupita tangu Yulio na wafungwa wake kuondoka Kaisaria. Wakati huu ulikuwa wakati wa hatari sana wa mwaka kwa merikebu ndogo ya mbao kusafiri baharini.

Paulo alikuwa mfungwa wa ajabu. Fikiria mfungwa kuwaonya manahodha wa merikebu ya kwamba ingekuwa hatari kwao kuendelea na safari. Paulo alifanya hivyo. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 27:10. Nahodha wa merikebu hakukubaliana na Paulo. Labda Bwana alikuwa amezungunza na Paulo na kumwonya. Nahodha alijua kwamba Bandari Nzuri hapakuwa mahali pazuri pa kukaa wakati wa baridi. Alitaka kwenda Foinike. Walikata shauri kwamba

kama wangesafiri karibu na pwani hawangepata shida, tena safari haingewachukua muda mrefu.

Muda mfuji baada ya kuondoka katika Bandari Nzuri, dhoruba kali ilianza na kupiga-piga merikebu ile ndogo. Ilikuwa vigumu sana kwa mashika usukani kuongoza merikebu. Jambo aliofanya ni kuacha merikebu iendeshe na upepo. Kisiwa cha Kauda ni kama Kilometa 32 kusini magharibi ya Bandari Nzuri. Ni kisiwa kidogo. Waambie wanafunzi watafute kisiwa hiki katika ramani zao. Kwa kusafiri kandokando ya pwani, merikebu ile ilepuka upepo. Mawimbi yalikuwa juu sana na Merikebu ikaanza kurushwa huku na huko, hata wakaanza kutupa shehena baharini. Siku ya tatu walitupa vyombo vya meli.

Mawingu meusi yalifunika uso wa jua mehana na kufunika nyota usiku na kufanya safari kuwa ya hatari sana. Siku hizi manahodha wana vifaa vya kuwaonyesha mahali hasa walipo baharini. Katika siku zile za Paulo, na kwa miaka mingi sana baadaye, mabaharia walitegemea jua na nyota kuwaongoza. Wakati jua na nyota zilipofunika na mawingu, labda walisafiri katika mahali pa hatari pwani bila kujua mpaka waliposhindwa.

Baada ya kusafiri siku nyingi katika mawimbi makubwa, na bila jua wala nyota, walikata tamaa yao ya kuokoka. Hawakuwa na ufahamu hata kidogo wa mahali pale walipokuwa.

angetimiza ahadi zake kwake bila kujali hatari zilizomkabili na kuchelewa.

MAMBO YA KUKAZA

1. Mungu alitimiza ahadi yake ya kumtuma Paulo Rumi.
2. Malaika wa Bwana alimhakikishia Paulo ya kwamba hakuna mtu hata mmoja ambaye angeangamia baharini.
3. Alifuata ahadi ya Mungu, Paulo aliwasaidia abiria wenzake kujitayarisha kuondoka merikebuni.
4. Ingawa merikebu ilivunjika na kuangamia, watu walisalimika kama Mungu alivyoahidi.

KULIFUNDISHA SOMO


Wengi wetu hutembea wakiwa na fikira za picha zao wenyewe. Picha hizo ni za mambo tunayofikiria kuwa tunafanana nayo sasa, na picha za mambo tunayotumaini kuwa tutafanana nayo wakati tutakapokuwa wakubwa. Je! unajifikiria kuwa katika kazi fulani ya ajabu? Je! umepata kufikiria jinsi ya Mkristo unayotamani kuwa siku fulani?

Jiulize mwenyewe swali hili: "Nawezaje kuwa kama Mungu anavyonitaka?"

Mtume Paulo alikuwa na fikira ya picha yake ambayo haikutegemezwa kwa ahadi ya Mungu mwenyewe. Alikuwa akisafiri kwenda Rumi, mji uliokuwa makao makuu ya ulimwengu wa ustaarabu. Paulo aliendelea kuwa

"Nakuamuru kwa jina la Yesu Kristo, mtoke huyu. Akamtoka saa ile ile." (Matendo 16:18)

Mabwana za kijakazi yule hawangeweza kuwa na tumaini la kupata faida kwake baada ya p-popo kumtoka. Jambo hili liliwakasirisha sana. Waliwakamata Paulo na Sila wakawapeleka sokoni ambako watawala walikuwako. Waliwaambia watawala hawa ya kwamba Paulo na Sila walikuwa wakichafua sana mji wao kwa kuhubiri dini mpya. "Makutano wote wakaondoka wakawaendea, makadhi wakawavua nguo zao kwa nguvu, wakatoa amri wapigwe kwa bakora." (Matendo 16:23) Baada ya Paulo na Sila kupigwa walifungwa miguu kwa mikatale, wakatupwa gereza katika chumba cha ndani. Mikatale ni vipande vizito vya miti vilivyo na mashimo ya kuingiza miguu.



na taabu. Inaonekana kwamba mambo mengi yalijaribu kumzuia kupeleka ujumbe wa Kristo Rumi. Lakini yeye alimwamini Mungu. Mungu alikuwa amemwambia kwenda Rumi. Kwa hivyo Paulo alishawishika kabisa kwamba angeweza kutimiza ahadi hiyo ambayo Mungu alikuwa ameahidi.

Tunaanza safari ya kwenda Rumi. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 27:1. Kwa kifungu hiki, tunaona ya kwamba Paulo alikuwa bado mfungwa, na akida aliyewasimamia wafungwa alitwa Yulio. Tunadhani kwamba Luka pia alikuwapo katika safari hii kwa sababu neno "tuabiri" limetumiwa. Luka ndiye aliyehandika kitabu cha Matendo, na inawezekana kwamba alikuwapo pamoja na Paulo wakati wa kuhukumiwa na katika safari hii.

Biblia yetu inatwambia kwamba siku ya pili yake, merikebu ilisimama Sidoni. Yulio alionyesha fadhili zake kwa Paulo kwa kumruhusu kwenda kwa marafiki zake.

Paulo na Sila walikuwa wamekuja Filipi kwa sababu Mungu ndiye aliyewaita huko, lakini sasa walikuwa gereza. Ilipofika usiku wa manane, Paulo na Sila walianza kuomba na kumwambia Mungu nymbo za sifa. Wafungwa wengine waliwasikia wakiimba, wakashangaa kwa nini walikuwa na furaha. Walikuwa wamekwisha kupigwa, wakatupwa gereza, na sasa walikuwa wakimba.

Kulitokea kwa ghafla mtetemeko wa nchi na misingi ya gereza ikatikisika zaidi mno hata milango ikafunguka na vifungu vilivyokuwa mikononi na miguuni mwa wafungwa vililegezwa. Mlinzi wa gereza alipoona milango ya gereza ikiwa wazi, alidhania ya kuwa wafungwa wote walikimbia, akataka kujua mwenyewe. Nyakati zile, sheria ya Rumi iliamuru kwamba mfungwa akikimbia, basi mlinzi wa gereza atauawa kwa ajili yake. Paulo alimwona mlinzi yule akitaka kujiua, akapaaza sauti yake kwa nguvu. Mwambia mwanafunzi mmoja kusoma maneno ambayo Paulo alimwambia mlinzi yule wa gereza katika Matendo 16:28.

Mlinzi yule wa gereza alingia ndani ya gereza katika chumba kile ambacho Paulo na Sila walikuwamo, akawaangukia. Alisema, "Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?" Uliza: Paulo alimjibuje? Mwambia mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 16:31. Walimweleza mlinzi yule wa gereza maana ya kumwamini Bwana Yesu Kristo. Mlinzi na jamaa yake na

wote waliokuwamo nyumbani mwake, walisikia ujumbe wa Kristo, wakaaamini wote, wakabatizwa.

Minzi yule wa gereza alionyesha shukrani yake kwa kuosha mapigo ya Paulo na Sila. Pia aliwaandalia chakula, akawapa, wakala. Mbele, hakujali wanafunzi hawa kwamba waliunizwa na kwamba walikuwa na njaa, lakini sasa Kristo akawa moyoni mwake, aliwajalia na kuwatunza.

KAZI YA KUUFANYA

Andika herufi hii "X" katika kila mstari ulio kando ya maneno ya kwele.

1. Barnaba alifuatana na Paulo katika safari yake ya pili ya umisheni.

X 2. Timotheo alikuwa kijana aliyemwamini Mungu.

3. Paulo hakumchukua Timotheo.

X 4. Sila alifuatana na Paulo katika safari yake ya pili ya umisheni.

5. Paulo na Sila waliabiri kwa mashua kwenda kwa miji ambayo alikuwa bado haijapata kutembelea.

Piga mstari chini ya neno au maneno ya kwele katika sentensi zifuatazo:

1. (Siku moja) (Usiku) Paulo aliona maono, na katika maono hayo alimwona mtu aliyemwambia avuke aeenda Makedonia.

2. Watu (watalu) (wane) walikwenda pamoja na Paulo Makedonia.

3. (Petro) (Matibibu Luka) alikwenda pamoja na Paulo.

4. Wayahudi wa Filipi waliabudu

(ndani ya sinagogi) (kando ya mto).

5. (Lidia) (Mariamu) alikuwa mmojawapo wa wanawake wale waliobudu kando ya mto.

6. (Watalu) (Minzi wa gereza) alimwamini Bwana Yesu akawa Mkristo.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Nitamwambia Bwana maadamu ninaishi; nitamshangilia Mungu wangu nikiwa hai." Zaburi 104:33

Tutaishi mara moja tu hapa duniani, na tunapishi, inatupasa daima kumwambia Mungu nyimbo za sifa.

WAKATI WA KUFUNGA

Jel kwa nini Paulo na Sila walikuwa na furaha halisi? (Waruhusu wanafunzi kujadiliana jambo hili.)

Jel sisi pia tunaweza kuwa na furaha kama ile Paulo aliyokuwa nayo? Furaha halisi haitegemei mambo ya kidunia. Ni furaha inayopakana kwa kumjua Mungu na kujua kwamba anatawala maisha yetu. Hebu turudie kusema kifungu chetu cha kukumbuka. Tukumbuke kumsifu Mungu kila siku.

Waambie wanafunzi kufikiri kumya na kukata shauri kama wanastahili kuwa na furaha hiyo halisi inayopakana kwa kumjua Mungu wao binafsi, kama wanamruhusu Mungu kutawala maisha yao, kama wana tamaa ya kufanya jambo lo lote ambalo Mungu anawazambia kufanya. Funga kwa maombi.

kwa kujua kwamba dhambi zao zilisamehewa.

Hebu tusome pamoja kifungu chetu cha kukumbuka, Yakobo 5:20. Paulo alifanya nini ili kujaribu kuokoa roho katika mauvi? Aliwashi watu kumwamini Kristo. Alionyesha kwa matendo yake kwamba aliwajali.

Tutatumia dakika chache katika maombi ya kufikiri. Bila shaka utawajua watu wengi ambao hawajampokea Kristo kuwa Mwokozi wao. Fikiria mmojawapo wa watu hao. Labda ni rafiki yako. Jel

unajali ya kwamba rafiki huyu wako ni mwenye dhambi mbele za Mungu kwa sababu hajamtegemea Kristo kumsamehe dhambi zake? Ni kwa jinsi gani unaweza kuwa mwaminifu katika kuwasaidia marafiki zako kumjua Kristo? Ni kwa jinsi gani unaweza kuonyesha marafiki zako ya kwamba unawajali?

Waulize wanafunzi kadha kama wangependa kuomba. Wape wakati wa kutosha, kisha ufunge maombi hayo wewe mwenyewe.

Sura ya Kumi na Moja

KUHAKIKISHA AHADI ZA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Matendo

27

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Kila mwanafunzi darasani mwako anaweza kuwa mtoto wa Mungu mara tu anapomwamini Yesu kuwa Mwokozi wake. Kufanya hivyo humpa nafasi na haki ya kushiriki katika jamaa ya Mungu. Ushirika ambao wanafunzi wako wanao na Baba yao aliye mbinguni huongezeka wakati wanapomfuata Mungu ambaye ni Baba wa upendo, wa kutoa riziki, wa kuongoza, wa kusahisha, na wa kutia moyo.

Katika hali ya kila siku wanafunzi wako huonyesha kwamba wanamtambua Mungu kama Baba wakati wanapoi Neno lake na kutaka ahadi zake. Kila mwanafunzi anaweza kuona katika maisha yake ya kila siku kwamba ahadi zinaweza kuaminiwa na tena ni za kwele. Omba ili somo hili juu ya kuhakikisha ahadi za Mungu limsaidie kila mwanafunzi kuendelea kumtegemea Baba yake aliye mbinguni ambaye huimiza ahadi zake.

Fanya kusudi la somo hili kuwa la kuonyesha jinsi Paulo alivyoundelea kuwa na matumaini kwa Mungu

SHERIA YA KIRUMI

Hakuna mshitakiwa ye yote ahukumiwaye kabla ya kukutana na washtaki wake uso kwa uso na kupewa nafasi ya kujitea kuhusu mashtaka aliyofanyiwa.

Piga mstari chini ya sababu ya Festo kumtaka Agripa kumsikia Paulo.

1. Festo alitaka kumhukumu Paulo kufa.
2. Festo alitaka kujua jambo la kumwandikia Kaisari.
3. Festo alitaka kusikia habari za Yesu Kristo.

Tazama picha hiyo hapo chini. Watu hao waliopo pichani walikuwa watu muhimu sana wakati ule wa Paulo.



Jel! unafikiri Paulo alifurahi kupata nafasi ya kuzungumza nao? _____

Kwa nini, au kwa nini hakufurahi?

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Jueni ya kuwa yeye amrejezaye mwenye dhambi hata atoke katika njia ya upotevu, ataokoa roho na mauti, na kufunika wingi wa dhambi." Yakobo 5:20

Mwenye dhambi akitubu dhambi zake kwa Mungu kwa njia ya Kristo, roho yake itakolewa na atakuwa na uzima wa milele kama Kristo aliyoahidi. Dhambi zote, hata kama ni ngapi, zitasamehewa.

WAKATI WA KUFUNGA

Festo na Mfalme Agripa waliridhika kukaa bila kumjua Kristo, wakamdhihaki Paulo kwa tamaa yake ya kuzungumza habari za Bwana. Jel! ni kwa nini Paulo alihusika na watu hawa? (Wape wanafunzi wakati wajadiliane jambo hili.)

Hebu tusome pamoja Yohana 3:36. Maana ya kifungu hiki ni kwamba mtu anayemwamini Kristo kweli kama Mwokozi wake ana uzima wa milele. Mtu asiyemwamini Kristo hawezi kuwa na uzima wa milele, bali hasira ya Mungu inamkalia.

Kwa sababu Paulo alijua ya kwamba watu waliomwamini Kristo hawana uzima wa milele, mara kwa mara alitaka kuwasaidia. Alihusika nao hasa. Aliwataka kuwa na furaha

Sura ya Nne

PAULO AHUBIRI ATHENE

MASOMO YA BIBLIA: Matendo 17:16-34

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wanafunzi darasani mwako hujifunza kujifikiria mambo mengi, lakini wanahitaji kuongozwa na mtu mkubwa ili waweze kuwa na fikira na mawazo mema. Somo hili linatueleza habari jinsi Paulo alivyowafundisha watu wa Athene Injili ya Kristo. Wasaidie wanafunzi kuona mawazo mabaya ya watu wa Athene, na pia kuona jinsi Paulo alivyowaambia ukweli wa Mungu. Wasaidie wanafunzi kukata shauri kushiriki injili na wengine, na kuacha matokeo ya kushiriki kwao mikononi mwa Mungu.

Kusudi la somo hili ni kuonyesha ya kwamba kuwa watu wa dini peke yake hakutoshi. Ni lazima kumkiri Yesu Kristo kama Mwokozi wako.

MAMBO YA KUKAZA

1. Paulo aliwaona watu wa Athene kuwa wenye dini, lakini hawakumjua Mungu wa kweli aliye hai.
2. Watu wenye ujuzi walimpeleka Paulo Areopago kusikiliza mafundisho yake.
3. Katika kusema na watu hawa, Paulo alijaribu kuwaonyesha kwamba wazo lao la kuabudu miungu wengi lilikuwa kosa, na kwamba ilikuwa

lazima wamwamini Mungu wa kweli aliye hai ili waweze kupata wokovu.

4. Ni watu wachache tu kati ya wale waliomsikia Paulo ndio waliomwamini Yesu.

KULIFUNDISHA SOMO

Waulize wanafunzi wako swali hili: Jel! nitafanya nini watu wakikataa kusikiliza nikiwaambia habari za Kristo?

(Labda wewe kama mwalimu, umekwisha kujaribu kushiriki imani yako na mtu mwingine ambaye alikataa kusikiliza. Ikiwa umekwisha kuona jambo hili, uwaambie wanafunzi wako juu yake. Labda wao pia watakwambia jambo hili.

Tunakumbuka ya kwamba Paulo, mmisheni wetu, alikuwa amekwisha kutembelea miji mingi kushiriki Habari Njema ya Mungu. Katika mahali pengi, ni watu wachache tu ndio waliomsikiliza alipowaambia habari za Kristo, na wengine wakaamini. Tunajua ya kwamba watu wengine hawakumsikiliza, na kwamba Wayahudi wengine waliokasirika, waliwakamata Paulo na Sila na kuwaweka gerezani Filipi. Baada ya Paulo na Sila kufunguliwa gerezani, Timotheo alijunga nao. Wote watatu walikwenda Thesalonike na Beroia. Waambie wanafunzi kutafuta miji hii miwili katika ramani.

Watu wengi katika miji hii walisikiliza injili ya Kristo, wakamwamini kama Mwokozi. Pia kulikuwapo watu wengine ambao hawakutaka kusikiliza injili, watu hawa walimfanya Paulo kuondoka Beroa. Timotheo na Sila wakabaki Beroa.

Paulo alikwenda Athene, mji mkuu wa Uyunani. Wasaidie wanafunzi kupata mji huu katika ramani. Mwanbia mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 17:15-16. Hebu tujifanye kama kwamba tuko Athene pamoja na Paulo, na kwamba tunatembea naye mjini. Po pote tuendapo tunaona madhabahu na sanamu ambazo Wayunani wanatumia katika ibada yao. Majengo mazuri kuliko mengine yote mjini ni mahkalu ya miungu. Tunasimama na kuangalia miungu hao waliotengenezwa kwa dhahabu, kwa fedha, na kwa jiwu. Miungu hawa hawana uhai. Tunaweza kuwagusa. Hawawezi kujongea kwa maana wao ni sanamu tu zilizotengenezwa na wanadamu. Zinakaa ndani ya hekulu zilizojengewa.

Tunaposema na watu hawa wa Athene tunaona kwamba wanaamini ya kuwa miungu hawa wanatawala sehemu mbalimbali za ulimwengu. Wanatawambia ya kwamba "Neptune" anatawala bahari, maziwa na miti, "Jupiter" anatawala mbingu, na "Athena, mungu wa kike" anatawala mji wa Athene.

Kisha tunaona madhabahu iliyoandikwa, "KWA MUNGU

ASITETULIKANA." Watu wa Athene wanaogopa ya kuwa pengine hawamwabudu Mungu wa kweli, kwa hivyo wamejenga madhabahu hii kwa mungu wasiyemjua.

Paul anakasirika, watu hawa hawajui Mungu wa kweli aliyey hai. Paulo alikata shauri ya kwamba ni lazima kuwambia watu hawa habari za Mungu na Kristo. Wambie wanafunzi kusoma Matendo 17:17 wapate kuona jambo ambalo Paulo alifanya. Tutamfuata Paulo mpaka sokoni. Huko sokoni watu hawacadi kwa shughuli ya kuuza na kumunua bidhaa peke yake, wanakwenda pia kuzungunza juu ya shughuli nyengine kama siasa na ya dini. Paulo anasema na watu hawa. Wengine kati yao ni watu wenye ujuzi. Wana tamaa kusikia mawazo mabaya, kwa hivyo wananyamaza kinywa kutafutiza Paulo. Mwanbia mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 17:18, ili wanafunzi wote wapate kuona jinsi watu hawa walivyomfikiria Paulo na ujumbe wake.

Watu wengine waliposikia habari za Yesu na ufufu wake, walifikiri kwamba Paulo alijua habari za Mungu fulani mgumi kwao, na walitaka kusikia mengi kutoka kwake. Walimpelika Paulo mpaka Areopago, na wao walaketi juu ya mawe yaliyokuwa hapo. Paulo alitaka kuwaonyesha kwamba waligawa na kosa kubudu miungu hawa na sanamu nyengine. Pia alitaka kuwasaidia kumjua Mungu wa kweli na kusameheva dhambi zao.

kuelekea nuru na kuwafanya waache nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu.

Paulo alitii mwito wa Mwokozi katika maono. Kwanza, aliwahubiria watu wake kisha akawahubiria watu wa Mataifa.

Paulo alisema ya kwamba hakusema jambo lo lote tofauti isipokuwa yale yaliyomenwa na manabii. Je! ni ukweli upi muhimu ambao Paulo aliwambia watu wote? Mwanbie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 26:23.

Kwa sababu Festo alikuwa Mrumi, hakuweza kuelewa mengi ambayo Paulo aliyasema. Je! Festo alifikiri nini wakati Paulo alipokuwa akiitua ushabidi wake? Soma Matendo 26:24. Festo liwali alifikiri Paulo alikuwa na wazimu wakati Paulo aliposema juu ya ufufu wa Kristo katika wafu. Alifikiri ya kwamba Paulo alikuwa anasoma sana.

Ingawa Festo hakujua habari za manabii, Mfalme Agripa alikuwa anajua. Alikwisha kusikia unabii wa Kristo maishani mwake mwote. Paulo alimwuliza kama aliwamini manabii. Kisha Paulo alijibu swali hilo yeye mwenyewe kwa kusema, "Najua ya kuwa wawaamini." Mfalme Agripa alimwambia Paulo, "Kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo?" Paulo alimjibu, "Nanwomba Mungu kwamba, ikiwa kwa machache au ikiwa kwa mengi, si wewe tu ila na hao wote wanaonisikia leo wawe kama mimi, isipokuwa vifungo hivyo." (Matendo 26:29)

Wakati Paulo alipomaliza kusema, mfalme, liwali, Bernike na wakuu wengine, wote walitoka nje kusemezana juu ya kesi ile. Walikubaliana ya kwamba Paulo hakutenda neno lo lote lililostahili kifo wala kufungwa. Ingawa hakuwa na hatia, ile rufani aliyotaka kwa Kaisari haingeweza kubadilishwa.

Maombi ya Paulo yalikuwa yakijiibiwa na bwana. Alikuwa akienda Rumi, na alijua ya kwamba ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kwake kwenda Rumi.

KAZI YA KUFANYA

Mfalme Agripa na Bernike, dada yake, walikuja Kaisaria ambako mtume Paulo alikuwa mfungwa. Chora mvingo kwa herufi "K" iliyo kado ya sentensi iliyo ya kweli, na uchope mwingo kwa herufi "M" iliyo kando ya sentensi ambayo si kweli.

K M Mfalme Agripa na Bernike walikuja kumkaribisha Festo.


K M Festo liwali alimwambia mfalme ya kwamba Paulo alikuwa na hatia.

K M Viongozi wa Kiyahudi walitaka Paulo ahukumiwe.

Festo alimkumbusha Agripa sheria ya Kirumi. Kamilisha mambo aliyomwambia Agripa katika sentensi ifuatayo hapo chini:

siyo hatia. Nilimwuliza Paulo kama alitaka kwenda Yerusalemu kuhukumiwa huko, lakini yeye alitaka rufani kwa mfalme Kaisari Augusto."

Baada ya Agripa kumsikiliza Festo akimsimulia maneno juu ya Paulo, alimwambia Festo ya kwamba alitaka kumsikia Paulo yeye mwenyewe. Festo alimwahidi kwamba angemsikia Paulo keshowe. Festo alimtaka sana Agripa kusikia maneno ya Paulo. Hakuna na jambo lo lote kanuni la kumwandikia mfalme juu ya Paulo mfungwa wake. Halikuwa jambo la busara kumpeleka mfungwa kwa mfalme bila kumwandikia hatia yake. Festo liwali alitumaini ya kwamba kwa kumwuliza-uliza Paulo maswali, angepata jambo la kumwandikia mfalme.



Keshowe, Paulo alielewa mbele ya wakuu waheshimiwa - yaani, mbele ya mfalme, malkia liwali, wakuu wa vita, na watu wengine muhimu. Waulize vijana kama wanafikiri ya kwamba Paulo alifurahi kuzungumza na watu


hawa muhimu. Ngojewa ili wanafunzi watoe jibu.

Paulo alianza maneno yake kwa kumwambia Agripa ya kwamba alikuwa na furaha kujitetea yeye mwenyewe mbele ya mtu (yaani mbele ya mfalme Agripa mwenyewe) ambaye alijua desturi za Kiyahudi. Paulo alikuwa amekwisha kuwasimulia Feliki na Festo maneno hayo yake, lakini wao walikuwa Warumi na hawakufahamu vizuri dini ya Wayahudi. Mfalme Agripa alikuwa Myahudi kama yeye, tena alijua vyema sheria za Kiyahudi na desturi zao.

Paulo alieleza jinsi alipokuwa kijana aliwachukia Wakristo. Alieleza jinsi alivyofikiria kwamba alikuwa akifanya kazi njema kwa kuwatesa Wakristo na kujaribu kuwalazimisha kumlaani Kristo. Alifikiri kwa hakika ya kwamba kadiri angezidi kuwatesa waamini wa Yesu, ndiyo angezidi kupendeza Mungu, lakini fikira hii yake ilikuwa upuzi tu.

Paulo alimwambia Mfalme Agripa juu ya ugeuzi wake alipokuwa njiani kwenda Dameski. Waulize wanafunzi wakueleze habari za ugeuzi wa Paulo. Habari hizo zilikuwa katika somo la kwanza juu ya Paulo. Jaribu kuona jinsi wanavyoweza kuzikumbuka vyema.

Pia Paulo alimwandikia Mfalme Agripa ya kwamba Bwana alimwambia kufumbua macho ya Wayahudi na watu wa Mataifa waliokuwa vipofu katika macho ya kiroho, kuwageza waiache giza



Paulo alianzaje mahubiri yake? Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 17:22-23. Paulo alianza mahubiri yake kwa kuwasifu watu hawa. Alisema, "Katika mambo yote naona ya kuwa ninyi ni watu wa kutafakari sana mambo ya dini." (Matendo 17:22b) Uliza: Kwa nini unafikiri Paulo alimtaja mungu asiyejulikana? (Tumia wakati katika kuzungumza.)

Ingawa watu wa Athene waliabudu miungu wengi, hawakumjua Mungu pekee wa kweli, Mungu aliyewaumba na kuwatumia Mwanawe kuwaokoa katika dhambi zao. Paulo aliwaambia hakuja kuwaeleza habari za mungu mgeni, kama alivyotumainia, bali alikuja kuwaambia habari za Mungu ambaye walikuwa wakajaribu kumwabudu bila kumjua. Aliwaambia ya kwamba Mungu ambaye yeye alimwabudu ndiye Bwana wa mbingu

na nchi, na ndiye Mtawala wa vitu vyote.

Paulo aliwaambia watu hawa ya kwamba Mungu wa kweli na aliye hai hakai ndani ya mahekalu yaliyojengwa kwa mikono ya wanadamu, bali anakaa ndani ya roho ya kila mmoja wetu. Alisema Mungu "havi mbali na kila mmoja wetu." (Matendo 17:27.) Waambie wanafunzi wako kufungua Biblia zao katika Warumi 10:9-15.)

Uliza: Je! tunawajua watu wengine katika nchi hii wanaohitaji kumjua Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao?

Je! unaelewa ni kiasi gani unahitaji kumjua Yesu kama Bwana na Mwokozi wako?

KAZI YA KUFANYA

Soma sentensi zifuatazo kisha uweke alama hii (X) katika kila mstari ulio kando ya sentensi ya kweli.


X 1. Paulo aliudhika alipoona mji wote wa Athene ukijaa sanamu au miungu wa uongo.

X 2. Paulo alizungumza na Wayahudi ndani ya jengo la sinagogi ambalo Wayahudi walijenga kama mahali pao pa kuabudia.

X 3. Kila siku Paulo alizunguza habari za Yesu sokoni na wale aliokutana nao.

Je! ni maneno yapi mageni ambayo Paulo aliona madhabahu iliyoikuwa pale mjini? Andika

maneno hayo chini ya picha ya madhabahu.




KWA MUNGU ASIYE- JULIKANA

Soma katika Matendo 17:24-26 mambo ambayo Paulo aliwaambia watu wa Athene juu ya Mungu. Sasa chora mstari kutoka kwa kila sentensi hapo chini hadi kwa neno linalokamilisha.

Mungu aliumba
Mungu ni nchi
Bwana wa mbingu ulimwengu na
Mungu haka watu wote
ndani ya mikono ya
Mungu wanadamu
hatumikiwa kwa hekali
kutoka kwa mtu mmoja Mungu
alifanya taifa la

Soma matendo 17:32-34 unone jinsi watu mbalimbali walivyofikiria ujumbe wa Paulo. Chini ya kila picha andika namba ya kifungu cha Biblia kinaeleza habari yake.



Mpuzi huyu!
Nami awezaje
kufufuka katika
watu?

Kifungu cha 32:



Twaamini ya
kwamba alikufa
kwa ajili yetu.

Kifungu cha 34:



Tutasikiliza
tena katika
habari hiyo.

Kifungu cha 32:

Sura ya Kumi

KUMSHUHUDIA KRISTO

MASOMO YA BIBLIA: Matendo

25:13-27; Matendo 26:1-32

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Katika somo hili utataka vijana wako kuona mambo ambayo Paulo aliyaeona na kuwaza mambo Paulo aliwaza. Wakifanya hivyo ndipo watakuwa na tamaa ile kuu ya Paulo ya kuwataka wengine kujiunga na jamaa ya Mungu. Waongoze wanafunzi wako kuona ya kwamba Paulo alitumia kila nafasi kumshuhudia Kristo. Kusudi la somo hili ni kutia wanafunzi wako moyo kuwasaidia wengine kumpokea Kristo kama Mwokozi wao. Paulo, kwa uaminifu mkuu alitumia kila nafasi kushuhudia mambo ambayo Bwana Yesu aliyefufuka katika wafu alimfanyia, na kuwasili wengine kumpokea Yesu kama Mwokozi wao. Paulo aliwashuhudia watu wote - watu wa kawaida na wengine yeye. Katika somo hili tunajifunza jinsi aliyowashuhudia watu muhimu.

MAMBO YA KUKAZA

1. Paulo hakujitetea tu mbele ya Mfalme Agripa na wengine, bali aliwakaribisha pia kuwa Wakristo.
2. Inatupasa kushirikiana na Paulo ya kuwahubiria wengine wokovu wa Kristo.
3. Mungu alikuwa akimtayarisisha Paulo njia ya kwenda Rumi.

KULIFUNDISHA SOMO

Katika kuendelea na somo letu lililojipa, tutakumbuka ya kwamba Paulo alikuwa mfungwa bado katika Kaisaria. Aliitaka rufani kwa Kaisari mjini Rumi kuhukumu kesi yake.

Festo liwali alikuwa na mgeni mshamiwa. Je! ni nani aliyekuja Kaisaria kumtembelea Festo? Mwanafunzi anaweza kusoma Matendo 25:13 na kutupa jibu hili. Ndiyo, walikuwa Agripa mfalme wa Kiyahudi na Bernike dadaye. Kama mfalme katika Uyahudi (Palestina), Agripa alikuwa na mamala katika serikali ya Warumi kama Festo liwali aliyokuwa. Ilikuwa jambo la kawaida kwa watawala hawa wawili kuzungumza habari za serikali ya Warumi na shida zao.

Je! ni kesi ipi hasa ambayo Festo alimwambia mfalme Agripa? Ndiyo, alimwambia kesi ya Paulo aliyekuwa mfungwa wake. Je! Festo alimkumbusha Agripa jambo gani kuhusu sheria ya Warumi? Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 25:16.

Hapa kuna maneno ambayo Festo alimsimulia Agripa. "Muda mfupi baada ya mimi kuwa liwali, makuhani wakuu na wakuu wa Wayahudi waliniomba kumhukumu Paulo kufa. Na wakati wa hukumu nilistaajabu kuwasikia Wayahudi wakimshtaki Paulo kwa tofauti za kidini tu wala

1. Jemadari aliogopa kwamba Paulo angefanywaje? Angeraruliwa.

2. Wakati Paulo alipokuwa ngomeni ni nani aliyemtia moyo usiku? Bwana.

3. Wayahudi wale arobaini wenye hasira walipanga kufanya nini? Kumwua Paulo.

4. Ni nani aliyesikia mpango huo wao na kwenda kumwona Paulo? Mtoto wa dada ya Paulo.

5. Jemadari aliamua kumpeleka Paulo, Kaisaria. Je! alimpeleka kwa nani? Feliki liwali.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Hata twathubutu kusema, Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogopa; mwanadamu atanitenda nini?" Waraka kwa Waebrania 13:6

Katika hadithi ya Marie Monsen na ya Paulo, tunajifunza kwamba watu hawa walikuwa na imani kuu katika Bwana, na katika kuwasaidia na kuwalinda. Ikiwa wanafunzi wako wanaweza kuwa na imani hii katika Bwana, watakuwa na maisha ya furaha bila wasiwasi. Lakini hii si kusema kwamba hawatakuwa na shida. Maana yake hasa ni kwamba Mungu atawaongoza katika njia yo yote watakapomhitaji.

WAKATI WA KUFUNGA

Kama mwanafunzi akiuliza swali hili, "Je! naweza kuwa na hakika kwamba Mungu atakuwa karibu nami

wakati nitakapomhitaji?" Wewe utamjibuje? Somo hili juu ya Paulo ni swali zuri sana. Watie wanafunzi wako moyo kuomba kuwa na imani thabiti katika Mungu. Wakiwa na imani thabiti watajua kwamba Mungu yuko karibu nao daima. Waulize wanafunzi wako swali hili: Je! mnaweza kuwa na hakika kwamba Mungu atakuwa karibu nanyi wakati mtakapomhitaji? (Wape muda wa kujibu.)

Funga kwa maombi ili kila mmoja wao watakuwa na imani thabiti.

Klaudio Lisia kwa liwali mtukufu Feliki, Salamu! Mtu huyu alikamatwa na Wayahudi, wakawa karibu kumwua, ndipo nikaenda pamoja na kikosi cha askari nikamwoko, nilipopata habari ya kuwa yeye ni Mrumi. Nami nikitaka kulijua ile neno waliomshitakia, nikamtelemshea nikamweka mbele ya baraza; nikaona kwamba ameshitakiwa kwa ajili ya maswali ya sheria yao, wala hakushitakiwa neno lo lote la kustahili kuuawa wala kufungwa. Hata nilipowea habari kwamba patakuwa na yitimi juu ya mtu huyu, mara nikampeleka kwako, nikawaagiza wale waliomshitaki, wanene habari zake mbele yako. Wasalamu. Matendo 23:26-30

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Amin, amin, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani." Yohana 5:24

Katika kuwaeleza wanafunzi wako kifungu cha kukumbuka, unaweza kusema ya kwamba Yesu ndiye aliyewaambia watu maneno haya ya upendo wa Mungu. Aliwaambia ya kwamba kama wangepapokea maneno haya mioyoni mwao, na kumwamini Mungu, wangerithi uzima wa milele.

Sura ya Tano

USIOGOPE

MASOMO YA BIBLIA: Matendo 18:1-22

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Je! umepata kuogopa? Unafikiri wanafunzi walioko darasani mwako wanaogopa? Ndiyo, wanaogopa. Pengine wanaogopa giza au kuzungumza mbele ya darasa, au pengine wanaogopa ugonjwa au mauti. Vijana wengi wa rika lenu hawataki kusema kwamba wanaogopa kitu cho chote. Walikuwa katika umri huu, wanaogopa mambo mengi.

WAKATI WA KUFUNGA

Tumejifunza katika somo hili ya kwamba Paulo aliwaambia watu waioabudu miungu mingi habari za Mungu mmoja wa kweli. Wengine kati ya watu hao walianza kumwamini Mungu, wakajifunza kumpenda Kristo kama Mwokozi wao. Pengine baadhi ya wanafunzi wako hawamjui Yesu Kristo kuwa ndiye Mwokozi wao. Pengine hawaelewi jinsi ilivyo muhimu kufanya hivyo. Funga kwa maombi ili kwamba wanafunzi wako wote watamjua Kristo kuwa ndiye Bwana na Mwokozi wao.

Kwa kujifunza somo hili, utaona ya kwamba Paulo alikuwa na sababu ya kuogopa. Siku moja usiku katika maono, Bwana alisema na Paulo akamwambia asiogope kwa sababu angekuwa pamoja naye.

Kabla ya kufundisha somo hili, zungumza na wanafunzi wako juu ya woga. Ni jambo la muhimu sana kwa wanafunzi wako kujua ya kwamba Mungu yupo pamoja nao. Atawapa ushujaa wa kufanya mambo ambayo wanaogopa kufanya. Ni lazima wazungumze na Mungu juu ya woga

wao na kumwomba kuwasidia. Wakimwomba hivyo, atawasaidia. Labda wewe kama mwalimu, unaweza kujua woga wao. Ni lazima wajifunze kwamba hawapaswi kuishi kwa woga, bali wawe na ushujaa. Mungu atawapa ushujaa wanaotaka. Sisi sote tunapaswa kumwamini Bwana kutusaidia kushinda woga wetu. Wanafunzi wakiataka kuzungumza juu ya woga wao, uwaruhusu kufanya hivyo na uwasikilize. Pengine unaweza kuwasidia kuwa na nia ya kushinda woga wao kwa kumwamini Bwana. Kusudi letu leo ni kuonyesha kwamba Mungu atatusaidia wakati tunapoogopa.

MAMBO YA KUKAZA

1. Paulo alinubiri nyumbani mwa Yusto baada ya Wayahudi wasioamini waliokuwa sinagogini kukataa Injili.
2. Bwana alimwamuru Paulo katika maono kushuhudia kwa ushujaa, akaahidi kuwa pamoja naye.
3. Paulo alipondelea kuhubiri katika Korintho, Wayahudi walimkamata na kumpeleka mbele ya liwali wa Kirumi kuhukumwa.
4. Mungu alichagua kumlinda Paulo kudhuriwa.

KULIFUNDISHA SOMO


Katika somo lililopita tulimwacha Paulo Athene. Katika somo hili tutajifunza juu ya wakati wa Paulo kuwako katika Korintho. Wakati tunapojifunza somo hili, hebu

tufikirie nyakati ambazo Paulo angekuwa na sababu za kuogopa. Kisha tutatafuta jibu la swali hili: Naweza je kushinda woga wangu?

Jei Paulo alipata marafiki Korintho? Mwanbie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 18:2. Akila na Prisila, mke, waiikuwa wakikaa Rumi. Iliwabidi kuondoka huko kwa sababu Wayahudi wote waliamriwa kutoka Rumi. Kwa hivyo walikuja kukaa Korintho.

Wakati Paulo alipokwenda Korintho walikwenda nyumbani mwa marafiki zake wawili kukaa pamoja nao. Waiikuwa na kazi kama ya Paulo. Jei kazi hiyo ilikuwa nini? Mwanbie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 18:3.

Kila kijana wa Kiyahudi aliyetoka katika jamaa maskini au tajiri, alifundishwa kazi. Paulo alifundishwa ushonaji hema. Walishona hema kwa ngozi ya mbuzi.



waliokuwa na hasira nyingi. Walimrudisha Paulo ngomeni.

Siku ya pili yake, Bwana alisimama karibu na Paulo. Mwanbie mwanafunzi mmoja kusoma mambo ambayo Bwana alimwambia Paulo katika Matendo 23:11. Bwana alikuwa akimtia Paulo moyo kwa sababu pengine alijua kwamba Paulo alikuwa na wasiwasi juu ya mambo ambayo yangempata.

Kulipopambazuka, Wayahudi walifanya mapatano, wakajifunga kwa kiapo kwamba hawangekula kitu cho chote wala kunywa mpaka wamwue Paulo. Wayahudi hao waliocapiana waiikuwa arobaini. Walikwenda kwa wakuu na makuhani na wazee, wakawapasha habari juu ya kufifunga kwao kwa kiapo. Waliwaomba wakuu hao wa makuhani na wazee kuwasaidia katika mpango huu wao kwa kumwambia jemadari amlete tena Paulo mbele ya baraza. Walisema wangemwua Paulo kabla hajakaribia baraza.

Mtoto wa dada ya Paulo alisikia habari juu ya mpango huu akaenda ngomeni kumwarifu Paulo. Halatu Paulo alimwita askari mmoja akanwambia kumchukua mtoto yule kwa jemadari ili kumwarifu juu ya mpango ule wa Wayahudi arobaini. Baada ya mtoto yule kumwarifu jemadari juu ya mpango ule, jemadari alimwagiza asimwambie mtu ye yote kwamba alimwarifu juu ya mpango ule.

Jemadari aliona kwamba haikuwa salama kwa mfungwa wake (Paulo)

kubaki Yerusalemu. Alikata shauri kumpeleka Kaisaria kwa liwali Feliki. Alikata shauri kumwondoa Paulo usiku ule ule. Kwa ajili ya ulinzi na usalama, aliwaamuru askari mia mbili, na askari wapanda farasi sabini, na wenye mikuki mia mbili kumchukua Paulo na kumpeleka Kaisaria. Jemadari hakutaka jambo lo lote baya kumpata mfungwa huyu Paulo ambaye alikuwa raia wa Rumi. Pia, aliandika barua kwa liwali Feliki. Barua hii imeandikwa katika Matendo 23:25-30. Mwanbie mwanafunzi mmoja kusoma.

Askari wa miguu walimchukua Paulo mpaka kwa Antipatri usiku ule. Siku ya pili yake asubuhi walirudi zao ngomeni, na askari wale wapanda farasi wakamchukua Paulo na kumpeleka Kaisaria. Walimpa liwali barua ile waliopewa na jemadari, wakamweka Paulo mbele yake. Liwali alimwambia Paulo ya kwamba angesikia kesi yake wakati washtaki wangewasili kutoka Yerusalemu.

KAZI YA KUFANYA

Katika baraza kulikuwa na makundi mawili, Mafarisayo na Masadukayo. Makundi haya yaliofautiana katika imani yao. Paulo alikuwa Farisayo. Baada ya muda usio mrefu, makundi haya mawili waliingia katika mabishano makali juu ya Paulo. Mafarisayo walisema, "Hatuoni uovu wo wote katika mtu huyu." Jaza nafasi zilizoachwa katika sentensi zifuatazo:

Katika somo hili tutajifunza kwamba Paulo aliamini ahadi za kumlinda. Hakumwogopa mwanadamu.

Jemadari hakujiifunza sababu iliyowafanya Wayahudi wale wenye hasira kutaka Paulo auawe. Siku ya pili yake alimpeleka Paulo mbele ya baraza. Watu sabini wa baraza hilo walikuwa wazee ambao ndio waliokuwa wakuu wa Israeli. Baraza hili lilikuwa kama mahakama zetu za sasa. Lilikutana kuhukumu wale waliotanganya watu au wale waliotafundisha mambo kinyume cha sheria ya Kiyahudi. Katika wakati ule wa Paulo, kuhani mkuu ndiye aliyetawala baraza la Kiyahudi kama vile majaji wanavyotawala mahakama zetu za sasa.

Je! ni jambo lipi la kwanza ambalo Paulo aliliambia baraza? Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 23:1. Baada ya Paulo kusema maneno haya, kuhani mkuu alimwamuru mtu aliyekuwa akisimama karibu naye kumpiga mdomo. Labda kuhani mkuu alikuwa amekasirika sana na Paulo kwa sababu alijiona kuwa na hatia kwa sababu maisha yake hayakuwa mema na hakutubu dhambi zake kwa Mungu. Kisha Paulo alikasirika sana. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 23:3. Paulo alijua kwamba hakufanya lo lote baya la kumfanya kuadhibiwa.

Paulo alijua wazi kwamba hangehukumiwa na baraza lile kulingana na sheria. Alifikiria njia

nyingine ya kumfanya kushinda kesi yake. Aliona njia ambayo kwayo angeweza kuwafanya Mafarisayo kuwa upande wake. Baraza lile lilikuwa la Mafarisayo na Masadukayo, na makundi haya mawili hawakupatana sikuzote. Paulo alijivunia kuwa Farisayo kabla ya kukutana na Kristo. Alikata shauri kuleta mashindano kati ya Mafarisayo hawa na Masadukayo juu ya ufufuo wa wafu. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 23:8. Mafarisayo walisimama upande wa Paulo wakati alipoliambia baraza kwamba alikamatwa na kufungwa gerezeni kwa sababu ya kuamini kwake kwamba kuna ufufuo wa wafu.

Wakati Paulo aliposema ya kwamba aliamini ufufuo wa wafu, alikuwa na maana kwamba alikamatwa na kufungwa gerezeni kwa sababu ya kuwa Mkristo. Mojawapo ya kweli za maana ambazo Mkristo anaamini ni kwamba Kristo alifufuka katika wafu na sasa anakaa mbinguni. Sisi Wakristo tunajua ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu anayetupa uzima wa milele kwa maana yu hai.

Baada ya Paulo kusema kwamba aliamini ufufuo wa wafu, je! Mafarisayo walisema nini? Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 23:9. Kisha palitokea ugomvi mkubwa na jemadari akaamuru askari kushuka na kumwondoa Paulo. Yeye ndiye aliyekuwa na mamlaka juu ya Paulo na alioyogopa ya kwamba pengine Paulo angeraruliwa na watu

Je! unaweza kustaajabu kwa nini Paulo alitumia wakati katika kushona hema na hali kazi yake muhimu ilikuwa kuhubiri Injili? Paulo alikuwa na nia ya kujitegemea mwenyewe badala ya kutegemea makanisa. Tunaweza kuwa na hakika ya kwamba wakati Paulo alipokuwa akifanya kazi ya kushona hema, alitumia kila nafasi aliyokuwa nayo kuwaambia washonaji wenzake na wanunzi habari za Mwokozi wake.

Siku ya sabato ilipofika, Wayahudi wengi walikwenda sinagogini kumwabudu Mungu. Paulo pia alikwenda. Alitaka kuwaambia watu ya kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zao. Yeye mwenyewe alikuwa Myahudi na alitaka sana Wayahudi hawa wenzake kuokolewa. Paulo alikutana na Wayahudi hawa kila siku ya sabato, akiwafundisha maandiko ya Agano la Kale juu ya Mwokozi ambaye Mungu aliahidi kuwatumia. Aliwaeleza ya kwamba Yesu wa Nazareti ndiye aliyekuwa Mwokozi.

Je! ni marafiki gani wa Paulo waliojiunga naye wakati alipokuwa Korintho? Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 18:5.

Wayahudi hawa wa Korintho hawakupokea ujumbe wa Paulo kuwa wa kweli. Ingawa Sila na Timotheo walisema ujumbe huo ulikuwa wa kweli, ni Wayahudi wachache tu walioamini. Wale wengine walikuwa wajeuri sana kwa Paulo. Paulo aliwaambia ya kwamba ataachana nao. Alikwisha kujaribu

kuwaonyesha njia ya wokovu lakini hawakumwamini. Alisema angewapelekea watu wa Mataifa ujumbe wa Kristo.

Je! Paulo alifanya mikutano yake wapi wakati alipoondoka sinagogini? Alikwenda kwa nyumba iliyokuwa imepakana na sinagogi hiyo na ilikuwa nyumba ya mtu mmoja aliyetwa Yusto. Yusto alikuwa Myunani na alikuwa mwamini. Hata sasa Wayahudi wangepokea kusikia habari za Bwana Yesu kama wangetaka, kwa kuhudhuria mikutano ya Paulo nyumbani mwa Yusto.

Paulo alipoendelea kuhubiri Injili, Krispo, ambaye alikuwa alikuwa mkuu wa sinagogi, pamoja na nyumba yake yote, walimwamini Kristo na kumpokea kuwa Mwokozi wao. Wakorintho wengine wengi pia waliamini na kubatizwa.

Bwana alijua kwamba Paulo angehitaji ushujaa katika hatari ambazo zingemkabili wakati wa kuhubiri Injili. Paulo alikuwa mmojawapo wa mitume mashujaa zaidi kuliko wengine wote, lakini ingawa alikuwa shujaa, alikuwa na sababu nzuri ya kuogopa chuki na pingamizi ya Wayahudi hawa wenye hasira.

Usiku mmoja Bwana alisema na Paulo katika maono. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma ujumbe wa Mungu katika Matendo 18:9-10. Paulo alipata ushujaa mwingi katika maono yale ya Bwana hata akakaa Korintho akifundisha Neno la Mungu

kati ya watu kwa muda wa mwaka mmoja na nusu.

Katika mwaka huo mmoja na nusu ambao Paulo alikaa Korintho, Wayahudi walimkasirikia sana hata wakamkamata na kumpeleka mbele ya liwali wa Kirumi wa Uyunani. Walidai ya kwamba Paulo aliwawata watu kumwabudu Mungu kinyumbe cha sheria yao. Liwali alisema kama Paulo angalivunja sheria ya Kirumi angkubaliana nao na kusikiliza kesi hiyo, lakini kwa mambo ya sheria ya Kiyahudi, hatakubali kusikiliza kesi.

Haimaye baada ya hayo, Paulo aliondoka Korintho akabiri mpaka Efeso, na watu waliokuwa pamoja naye walikuwa Akila na Prisila, marafiki zake wa kushona hema. Paulo alihubiri sinagogini, Efeso kama ilivyokuwa desturi yake. Aliwaambia watu wa Efeso habari za Kristo.

Paulo aliwaacha marafiki zake wale (Akila na Prisila), akaendelea na safari yake mpaka Kasaria, na baadaye Yerusalemu ambapo alikwenda kwa kanisa la kwanza. Mwishowe alirejea Antiokia.

KAZI YA KUFANYA

Chora mstari chini ya jibu sawa la kila swali.

1. Je! Paulo alikaa pamoja na mume na mke yupi katika Korintho?

Anania na Safira

Akila na Prisila

2. Je! walifanya kazi gani?

Kushona hema
Kuwa samaki
Kulina

3. Paulo alikuwa amefundishwa kazi. Je! kazi hiyo ilikuwa nini?

Kulina
Kufuga kondoo
Kushona hema

4. Je! Paulo alihubiri wapi siku wa Sabato?

Sokoni
Sinagogini Njiani
5. Aliwahubiria watu gani.

Warumi
Watu wa Athene
Wayahudi

Kata maneno ambayo si kweli katika sentensi zifuatazo.

1. Wayahudi hawakuamini Injili ya Kristo, kwa hivyo, Paulo aliwaambia ya kuwa angkwenda kuwahubiria (~~Watumia~~) (Mataifa).

2. Paulo alilingia katika nyumba ya mtu mmoja aliyeiwa (Yusto) (~~Akila~~). Mtu huyu alikuwa wa Mataifa na alimwabudu Mungu. Nyumba yake ilipakana na (~~seke~~) (sinagogi).

3. Kristo, (~~kutani~~) (mkuu) wa sinagogi, pamoja na jamaa yake (~~hawakutwamini~~) (walimwamini) Kristo.

4. Watu wengine (wengi) (~~wachache~~) katika Korintho pia walimwamini Kristo.

Alikei katika chumba chake mle melini akingojia kuona jinsi Mungu angemimiza ahadi hizo zake. Mlango wa chumba hicho chake ulifunguka, kisha haramia mmoja akainingia ndani. Marie aliwaza kama kwamba Shetani mwenyewe ndiye aliyekuwa akisimama pale na kumkazia macho.

Haramia yule alimwuliza Marie kwa ukali kumpatia saa yake ya mkono. Marie alimweleza kwamba haikuwa desturi yake kutoa zawadi zenye thamani kama hiyo kwa watu asiowajua. Haramia alijaribu kumhonga kwa kumwambia ya kwamba angemlinda kama angempa ile saa yake ya mkono. Lakini mpaka sasa Marie alikataa.

Kwa ghafla haramia yule aliruka juu akiwa ameshika bastola yake mkononi na kumwekeza Marie kichwa na kupiga kelele akisema, "Nitakupiga risasi." Marie alimjibu kwa utulivu, "Hakuna silaha yo yote iliyotengenezwa na binadamu itakayofaa. Hii ni ahadi ya Bwana kwa watumishi wake."

Haramia yule, kwa mara ya pili tena alitisha kumpiga Marie risasi, na tena Marie akarudia kusema ahadi ile. Kwa ghafla pakaja haramia wa pili alilingia ndani akamtoa nje haramia yule wa kwanza. Haramia huyu wa pili hakutaka kumdhuru Marie.

Huu ulikuwa mwanzo wa kuona Mungu akifanya miujiza kwake. Marie alikata shauri kukaa mle chumbani mwake. Kwa siku tisa

alikula tu matunda, na biskuti na chokolei ambazo alikuwa nazo. Wale maharamia walitaka kumpa chakula walichokuwa wameiba. Lakini yeye aliwaambia, "La. Siwezi kula chakula mlichobba."

"Basi utakufa," maharamia walimwambia.

"Ndiyo, naweza kufa," aliwajibu, "lakini Baba yangu anaweza kunifanya kuwa hai."

Siku ya kumi kabla ya kupambazuka, alisikia mtu akigonga mlango. Mtu huyu alikuwa afisa wa pili na alikuwa na mai na mikate ya Kichina ambayo alimlelea. Na baadaye, alimlelea mayai kila siku asubuhi na mapema.

Marie alianza kushawishi mioyo ya maharamia wale wakati. Walikuja mlangoi pake kila siku na alisema nao akiwaambia habari za Bwana wake wa ajabu. Bwana aliendelea kumpa amani.

Wale maharamia waliambiana wao kwa wao. "Je! msichana huyu ana amani ya aina gani hi? Unaweza kuona usoni pake. Waangalie abiria wengine. Waonekana kuwa na wasiwasi na wadhaifu kila siku."

Baada ya siku ishirini na nne wale maharamia waliacha meli ile. Walimwacha mmisheni Marie bila kumdhuru. Marie alijifunza ukweli wa ahadi ile ya Mungu isemayo, "Bwana ndiye msaidizi wangu; sitaogopa cho chote mwanadamu atachonifanyia."

MUNGU AMLINDA PAULO

MASOMO YA BIBLIA: Matendo

22:30; Matendo 23:1-35

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Kuna wakati ambapo sisi huwaza miyoni mwetu kuwa tuko mbali sana na Mungu, au wakati ambapo tunawaza ya kwamba Mungu yuko mbali sana nasi. Wakati kama huo tumepoteza tumaini letu katika ulinzi wa Bwana kwetu. Tunajua sikuzote ya kwamba Mungu yuko karibu sana nasi tukimtafuta. Wazo hili la kuwa mbali na Mungu, kwa kawaida ni la muda tu, na kwa kuzungumza na Mungu hata kama ni kwa dakika chache tu tunapata tena mawazo yetu ya kawaida ya kwamba Mungu yuko karibu nasi daima. Katika kufundisha somo hili juu ya Paulo, omba ili wanafunzi wako watakuwa na matumaini mapya katika ulinzi wa Bwana, kwa kumwamini na kumtii.

Somo hili linafuatana na lile lililopita. Paulo alikuwa na nia ya kuteseka kwa ajili ya Kristo kwa sababu alimpenda Bwana wake. Kwa sababu Paulo alijua ya kwamba Bwana alikuwa karibu naye, hakuogopa watu. Waonyeshe wanafunzi ya kwamba Paulo hakuogopa mambo ambayo watu wangemfanyia kwa sababu alimwamini Mungu kuwa msaidizi wake. Kusudi la somo hili ni kuonyesha kwamba Mungu atatulinda ikiwa tutamkiri.

MAMBO YA KUKAZA

1. Paulo alikuwa na akili katika kushughulika na watu waliomshtaki kwa baraza la Kiyahudi.
2. Bwana alimtia Paulo moyo.
3. Bwana atakuwa msaidizi wetu kama maisha yetu yataonyesha kwamba kumpendeza yeye ni kuzuri zaidi kuliko kuwapendeza watu.

KULIFUNDISHA SOMO

Kabla ya kusimulia hadithi ya Paulo, wasimulie wanafunzi hadithi hii ya kweli ya Mwamerika mmoja mmisheni wa China.

Abiria waliokuwa na woga walinong'onezana wao kwa wao, "Meli yetu imetekwa nyara na maharamia Wachina." Ilikuwa yapata siku nyingi tangu meli yao kuanza safari. Abiria hawa walidhania kwamba wangepatwa na jambo baya sana.

Marie Monsen, mmisheni huko China, pia aliogopa kwanza. Kisha alikumbuka ahadi fulani za Mungu zinazosema: "Usiogope maana niko pamoja nawe; usifadhaike maana mimi ndimi Mungu wako; nitakushika kwa mkono wangu wa kuume wa wema wangu." "Bwana ndiye msaidizi wangu; sitaogopa cho chote mwanadamu atakachonifanyia."

5. Mungu alisema na Paulo katika maono ~~(akamwambia alikuwa hatari kwa hivyo ilimpasa kuondoka)~~ (akamwambia akae na kuwahubiria watu, wala asioogope).

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Kwa maana mimi, Bwana, Mungu wako, nitakushika mkono wako wa kuume, nikikuambia, Usiogope; mimi nitakusaidia."

Isaya 41:13

Mungu alitoa ahadi hii yake siku za nabii Isaya, na anatoa ahadi hii siku hizi. Tukimwamini yeye, atatusaidia. Tuna shukrani kubwa kwa kujua ya kwamba Mungu aliye hai ndiye Mungu wetu

WAKATI WA KUFUNGA

Maisha ya Paulo yalikuwa hatari kwa sababu Wayahudi ambao hawakumwamini Kristo walikasirika naye sana. Kama Paulo hangaliamini ahadi ya Mungu ambayo Mungu alimwahidi kumsaidia, angaliondoka Korintho. Paulo alimwamini Mungu na Mungu akamsaidia. Waulize wanafunzi wako kama wanafikiri kwamba ahadi ya Mungu inawahusu wao pia. Ndiyo, ahadi hiyo ni kwetu sisi sote tunaoamini. Hebu tuseme tena kifungu cha kukumbuka. Ahadi ya Biblia kama hiyo ya kifungu cha kukumbuka hutusaidia kushinda woga. Hebu tumshukuru Bwana kwa ahadi yake kwamba atatusaidia. Tukate shauri kumwendea haraka wakati tunapojaribiwa kuwa woga.

Funga kwa maombi.

Sura ya Sita

KUMPENDEZA MUNGU BADALA YA MWANADAMU

MASOMO YA BIBLIA: Matendo

19:23-41

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Mara nyingi vijana hukabiliwa na shida ya kufanya jambo ambalo ni kosa, na wasipofanya, huchukiwa na marafiki zao. Tunapoendelea kukua, tunatambua ya kwamba urafiki wa namna hii hautupasi kutaka. Katika

somo hili letu juu ya Paulo, Paulo anatambua jinsi anavyowafanya watu wengi kupoteza faida katika shughuli zao kwa sababu ya mahubiri yake. Anajua ya kwamba wafanya biashara hawa hawampendi, lakini anaona ni heri kumpendeza Kristo kuliko kuwapendeza watu hawa.

Ni muhimu sana wanafunzi kujifunza kwamba ni bora

kumpendeza Kristo kuliko kuwependeza watu, kama mambo ambayo watu hao wanataka wafanye si mazuri. Kwa hivyo, mara kwa mara vijana wanamtaka kila mtu kuwependa, lakini si vizuri kama kupendwa huko kwao kutaweka katika hali ya kutenda kosa. Kusudi la somo la leo ni kuonyesha kwamba ni vizuri kutenda kama Kristo angali'daka tufanye hata kama kufanya hivyo kutatufanya kuwa na maadui wengi. Omba ili wanafunzi wako wawe na tamaa halisi ya kumpendeza Kristo bila kujali mawazo ya wengine.

MAMBO YA KUKAZA


1. Toko moja la kazi ya Paulo katika Efeso lilikuwa kwamba uuzaji vhekalu ya sanamu ulipungua.
2. Wafanya biashara (yaani, walia fedha) waliwataharukisha watu mjini kote.
3. Inawapasa Wakristo wakati mwingine kuchagua kama wanataka upendeleo wa nani - wa wanadamu au wa Kristo.

KULIFUNDISHA SOMO

Wakristo wengi wana tamaa mbalimbali. Hutafuta kumtumika Kristo na wakati huo huo wanatafuta mambo ya kidunia. Mtume Paulo alijizua kuwa na tamaa mbalimbali kama hizo. Alijioa sana sana kwa Kristo hata akajichukua mwenyewe kama mtumwa wa Kristo. Alikataa kupokea mapenzi ya wanadamu

kushindana na kusudi lake la kupata kibali cha Kristo.

Paulo alisimama Efeso alipokuwa njiani kwenda nyumbani wakati wa safari yake ya pili ya umisheni. Alikuwa amewaacha Priscila na Akila, marafiki zake wa kutengeneza hema katika mji huo. Na wakati aliporudi Efeso katika safari yake ya tatu ya umiseni, alikaa kwa miaka miwili akifanya kazi nao na kushuhudia Bwana. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 19:8-9. Tunaona ya kwamba Paulo alingia tena sinagogini kama alivyofanya Korintho. Alingia katika darasa la mtu mmoja aliyetwa Tirano. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 19:10-11. Mungu alifanya miujiza mingi sana kuwa huduma ya Paulo. Watu waliokuwa wakifanya ugannga waliiteta vitabu vyao pamoja na kuvichoma. Vitabu hivi vilikuwa na thamani ya fedha hamsini elfu, lakini waganga hao walijua kwamba Kristo hakupenda mambo hayo ya kuagaa.



tutajifunza mambo ambayo Paulo aliwaambia viongozi wale.

KAZI YA KUFANYA

Paulo aliingia hekaluni Yerusalemu. Alitaka kuwaonyesha Wayahudi kwamba alishika sheria za Mungu. Wakati Wayahudi wengine wasioamini walipomwona Paulo ndani ya hekalu, waliana kuwataharukisha watu juu yake. Weka herufi hii "X" kando ya mambo ambayo Wayahudi walishitaki Paulo kufanya.

X Kufundisha mambo kinyume cha watu.

Kufundisha mambo yanayo-pinga dhambi.

X Kufundisha mambo kinyume cha sheria.

X Kufundisha mambo kinyume cha hekalu.

X Kumwingiza Myunani ndani ya hekalu lao takatifu.

Jaza nafasi zilizoachwa katika sentensi zifuatazo kwa majibu ya kweli.

1. Paulo aliongea lugha gani na jemadari? Kiyyunani
2. Paulo aliongea lugha gani na Wayahudi? Kiebrania
3. Ni jina lipi Paulo alilotaja ambalo liliwakasirisha sana Wayahudi? Watu wa mataifa.

Chora mwingine kwa maneno ya kweli katika sentensi zifuatazo.

1. Jemadari aliwaamuru askari wake

kumlisha kupigana kumpiga Paulo.

2. Paulo alisema ya kwamba yeye alikuwa Mwafrika mtu mwema raia wa Rumi.

3. Paulo hakupigwa lakini aliwekwa gerezeni alipewa kitanda laini aliambiwa kusoma sheria.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Maana mmepeva kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, ila na kuteswa kwa ajili yake." Wafilipi 1:29

Katika kifungu hiki Paulo anawaambia Wafilipi ya kwamba wanapaswa kuteseka kwa ajili ya Kristo. Paulo aliteseka bila huzuni kwa ajili ya Kristo. Inatupasa sisi kuwa tayari kuteseka kwa Kristo ikiwa ni lazima.

WAKATI WA KUFUNGA

Paulo hakunung'unika juu ya mateso yaliyomjia maishani mwake kwa sababu alikuwa mtiifu kwa Kristo. Alijua kwamba kwa kutokuwa mtiifu kwa Yesu ambaye alikuwa kwa ajili yake kungemdhuru zaidi mmo.

Wakati mwingine tunaweza kuwa na nafasi za kuthibitisha utii wetu kwa Kristo. Yatupasa kuwa kama Paulo, na kuwa na nia ya kuteseka kwa ajili ya Bwana na Mwokozi wetu.

wote wa mji kukasirika naye. Alimwekea Paulo ulinzi mkali asipate kutoroka. Kisha jemadari aliwauliza watu ya kuwa Paulo alikuwa nani na alifanya nini. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma jibu ambalo jemadari alijibiwa na watu wale katika Matendo 21:34. Ilikuwa vigumu kwa jemadari kupata jibu la kweli kutoka kwa watu, kwa hivyo aliwaamuru askari kumkamata Paulo na kumfunga kwa minyororo na kumpeleka ngomeni ambako angekaa salama. Walipofika katika daraja kuingia ngomeni, iliwabidi askari kumbeba Paulo kwa sababu ya umati ule mkubwa wa watu wenye hasira waliopiga kelele wakisema, "Mwondoe huyu." Maana yake hasa ni kwamba walitaka askari kumwua Paulo.

Walipofika tayari kuingia ngomeni, Paulo alisema na jemadari kwa lugha ya Kiyunani. Jemadari alifikiri ya kwamba Paulo alikuwa Mmisiri yule ambaye kabla ya siku zile aliwafitinisha watu. Paulo alimwambia ya kwamba yeye alikuwa Myahudi kutoka Tarso. Kisha alimwomba jemadari kumruhusu kusema na watu wale. Jemadari alipokubali, Paulo alisimama madarajani kisha akasema na watu wale kwa lugha ya Kiebrania. Walinyamaza na kumsikiliza Paulo akiwaambia habari kuhusu ugeuzi wake. Waliyasikiliza maneno ambayo alikuwa akisema na kupendeza nao mpaka wakati aliposema kwamba Mungu alimtuma kuwahubiria watu wa Mataifa. Neno hili liliwakasirisha

sana wakaanza kupaza sauti zao wakisema auawe. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma jinsi watu wale waliyoonyesha hasira zao katika Matendo 22:23. Jemadari ambaye hakuelewa maneno ambayo Paulo aliyasema kwa lugha ya Kiebrania, alidhania kwamba Paulo alifanya kosa kubwa sana kwa maana watu walimkasirikia sana. Alikata shauri kuamuru Paulo kupigwa ili ajue sababu. Wakati askari walipokuwa wakimfunga Paulo na kumweka tayari kupigwa, Paulo alimwuliza jemadari swali. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma kifungu cha 25 cha Matendo 22. Kulingana na sheria za kirumi, hakuna raia yeye yote wa Rumi ambaye angeweza kufungwa wala kuadhibiwa kwa njia yoyote mpaka anapohukumiwa na kupatikana na hatia. Jemadari alimfikiria Paulo kuwa ni Myahudi tu na hakudhania kwamba angeweza kuwa raia wa Rumi.

Paulo aliepuka kupigwa, lakini alikuwa bado mfungwa. Jemadari alikuwa hajajua sababu ya Wayahudi kumtaka Paulo kuuawa. Hangeweza kumfungua mpaka wakati ambapo angefanya uchunguzi na kujua habari zake. Pia alifikiri kwamba Paulo alikuwa salama sana gerezani kuliko vile angalikuwa nje ambako Wayahudi wangemfikia na pengine kumwua.

Siku ya Pili yake, jemadari aliwaita viongozi wote wa dini ya Kiyahudi, akampa Paulo nafasi ya kujitetea mbele yao. Katika somo litakalofuata

Mji wa Efeso ndipo palipokuwa makao ya mungu mke Artemi. Watu kutoka nchi nyingi walikuja kumwabadu. Sanamu ya Artemi haikuwa nzuri kama sanamu nyingine za Wayunani; lakini watu waliamini kwamba sanamu hiyo ya jiwe ilianguka kutoka mbinguni. Waliweka ndani ya hekalu zuri lililojengwa kwa mawe meupe. Karibu kila mtu aliyetembelea mji wa Efeso alinunua sanamu ndogo ya Artemi au vihekalu vyake. Sanamu hizi ambazo zilitengenezwa kwa udongo, kwa miti, au kwa vyuma, watu walizichukua na kusafiri nazo kama hirizi ya kuwaletaka bahati njema. Hata nyingine ziliwekwa nyumbani kama miungu wa nyumbani.

Mafundi waliotengeneza sanamu hizi na kuziua, pamoja na vihekalu, walipata faida nyingi. Paulo aliona moyoni mwake ya kwamba kama alihubiri kweli Neno la Mungu kwa uaminifu, ilimpasa kuwaambia watu ya kwamba ilikuwa kosa kumwabadu Artemi. Bila shaka alijua kwamba jambo hilo lingelela shida baina yake na mafundi wale waliotengeneza sanamu hizo za Artemi na kuziua. Kwanza ilimpasa (yeye Paulo) kujibu swali hili moyoni mwake: "Je! niwapendeze nani, wanadamu au Kristo?" Alijua ya kwamba watu kama wangejifunza kumpenda Kristo na kumwabadu, wangekoma kununua sanamu za Artemi. Paulo alijibu swali lake? Alikusudia kumpendeza Kristo hata kama angekuwa na uadui na mafundi wake waliotengeneza sanamu.

Mungu alibariki mahubiri ya Paulo. Watu wengi waliacha imani yao ya uwongo na kumwamini Mungu wa kweli aliye hai. Wakristo hawa, kwa kweli walimpenda Paulo, wakawa marafiki zake.

Paulo alikata shauri kukaa Efeso mpaka baada ya karamu ya Pentekoste kwisha. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma 1 Wakorintho 16:8-9. Siku hii ilitokea katika mwisho wa mwezi wa Mei. Na huu ndio mwezi ambao watu wengi walikuja Efeso kumwabadu Artemi. Watu walifika kutoka kila sehemu za jimbo hilo kufurahia mchezo na sherehe iliyofanywa kwa heshima ya mungu mke wao. Bila shaka, Paulo alikuwa akitazamia wakati huu wa sherehe kwa sababu aliwaambia watu hawa habari za Mwokozi aliyekufa ili kuwaokoa katika dhambi zao.

Je! watu wale waliompokea Bwana Yesu kama Mwokozi wao wangeendelea kumwabadu Artemi? La, hawangeendelea kwa maana sasa wangekuwa na mwokozi aliye hai maishani mwao na hawangekuwa na hitaji lo lote la hirizi ya bahati njema. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 19:26.

Mtu mmoja aliyetwa Demetrio alikuwa mmojawapo wa mafundi wale waliotengeneza sanamu za kuwauzia watu. Aliona ya kwamba watu walikuwa hawanunui sanamu kama zamani. Hakuwa akipata faida nyingi kama zamani. Mafundisho ya Paulo yalikuwa yakiangusha biashara

ya mafundi wote waliotengeneza sanamu katika Efeso.

Demetrio alitia mkutano wa mafundi wote wa sanamu. Aliwakumbusha kwamba walitajirika sana kutokana na biashara ile ya kutengeneza sanamu na kuziiza. Pia aliwaarifu ya kuwa mafundisho ya Paulo yalikuwa yakiwazua watu kunuua sanamu katika Efeso na katika Asia yote. Alisema ya kwamba hawakuwa katika hatari ya kupoteza biashara yao peke yake, bali hata hekalu la Artemi lilikuwa katika hatari ya kuhesabiwa si kitu. Heshima ya mungu mke wao aliye mkuu ilikuwa hatari. Demetrio aliwafanya watu hao wengine kukasirika sana juu ya jambo hilo. Walianza kupiga kelele, wakisema, "Artemi wa Efeso ni mkuu."

Watu wengi hukuwanyika mara moja wakati lisilo la kawaida linapofanyika. Baada ya muda mfupi watu huzidi kuongezeka. Jambo kama hili ndilo lililofanyika Efeso. Baada ya muda mfupi, Waefeso wote walikuwa wakipiga kelele pamoja na mafundi wale wa kufua fedha, na kusema, "Artemi wa Efeso ni mkuu." Hata baadhi ya watu waliokiri upendo wao kwa Kristo walijiunga na watu wale.

Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 19:29 kuona ni shida ipi iliyokuwa ikioka. Je! Paulo aliyekuwa chanzo cha shida hiyo alikuwa wapi? Mara tu aliposikia kelele hizo alitaka kwenda

katika mahali pale pa mehezo ambapo walivapokea marafiki zake wawili. Lakini wanafunzi pamoja na baadhi ya watu wa Asia walimsihi asinde. Walijua kama Paulo angekwenda pale, basi ghasia zingezidi kuendelea.

Mkutano ule ulikuwa umechafuka sana hata wengine hawakujua sababu ya kukusanyika kwao pale. Juhudi zilifanywa kuwatuliza watu lakini waliendelea tu kupiga kelele, "Artemi wa Efeso ni mkuu." Mwishowe, karani wa mji aliwatuliza watu.

Karani huyu wa mji alianza kusema na watu kwa njia ya werevu ambayo wangependa kuelewa. Aliwaambia ya kwamba kila mtu alijua Waefeso walimwabudu Artemi mungu mke aliye mkuu, kwa hivyo hapakuwa na sababu ya kuwa na wasiwasi. Aliwaambia kwamba Paulo na wenzake hawakufanya kosa lo lote. Hawakuiba vitu vya hekalu wala kumtukana mungu mke wao, Artemi. Aliongeza kusema kwamba ikiwa Demetrio alikuwa na neno juu ya mtu ye yote, neno hili lilipaswa kupeleka barazani kuhukumiwa. Aliwaambia watu kuondoka na kwenda zao kwa amani kama siyo wangepingia taabuni kwa kuanzisha ghasia.

Paulo alichagua kumpendeza Kristo kuliko kumpendeza mwanadamu. Mungu alimsaidia katika hali hii. Baada ya ghasia kwisha, Paulo aliwaita wanafunzi wake, akazungumza nao, kisha akaondoka kwenda Makedonia.

imani katika Kristo kama Mwokozi. Wayahudi wale walikuwa wamezifanya sheria hizo kutawala maisha yao kwa miaka mingi sana na ilikuwa vigumu sana kwao kubadili fikira zao.

Ilikuwa muhimu kwa Wakristo Wayahudi Yerusalemu kumwamini Paulo kwa hivyo wazee walimtolea pendekezo juu ya jambo la kufanya. Walimwambia Paulo kwamba palikuwapo watu wanne ambao waliofungwa nadhiri kumtumikia Bwana. Watu hawa walipanga kuingia hekaluni na kuoga humo na kunyoa vichwa yao kama ishara ya utakaso wao. Wazee wale walimdokeza Paulo akaingia pamoja na watu wale wanne na kujitakasa. Jambo hili lingewapendeza Wakristo Wayahudi ya kwamba Paulo alikuwa akitii sheria ya Musa. Paulo alifanya kama walivyodokeza kwa sababu alitii kwele sheria za Musa sikuzote. Ilikuwa muhimu kwa Paulo kuwa hekaluni kwa siku saba kuondoa nadhiri ile ambayo yeye na watu wale wanne Wayahudi waliweka. Kabla ya siku hizi saba kumalizika, Wayahudi wengine wasioamini kutoka Asia walimwona Paulo hekaluni. Walijua ya kwamba Paulo alimleta mtu mmoja wa Mataifa Yerusalemu kutoka Efeso kwa sababu walikwisha kuwona pamoja mjini mle. Ilikuwa uwongo, lakini wao walisema kwamba Paulo alimwingiza mtu huyu wa Mataifa hekaluni.

Wayahudi walikuwa na sheria kali sana iliyowakatiza mtu ye yote wa Mataifa kuingia katika mahali pao pa

ibada. Walifikiri wao ndio waliokuwa wote pekee wa Mungu, na kwamba mahali pao pa ibada palipaswa kutumiwa na wao wenyewe.

Wayahudi wale kutoka Asia walijua kwamba wangepachagua watu kwa kuwaambia ya kwamba Paulo alimwingiza mtu wa Mataifa hekaluni. Wayahudi wale walisema ati Paulo alikuwa akifundisha kinyume cha sheria ya Wayahudi na ya hekalu. Pia walisema ati Paulo alitia hekalu unajisi kwa kumwingiza mtu wa Mataifa ndani.

Je! habari hii ilikuwa kwele? La. Lakini watu hawa hawakujali kungoja na kupata ukweli ndani yake. Walianini tu mambo ambayo Wayahudi wale kutoka Asia walisema, kwa hivyo walimkamata Paulo, wakamburita, wakamtoa ndani ya hekalu, kisha wakafunga milango. Walikuwa na nia ya kumwua Paulo na hawakutaka kutia hekalu lao unajisi kwa kumwua akwa ndani ya hekalu.

Mmoja wa askari walinzi alimpasha jemadari habari ya kwamba mji wote ulikuwa umechafuka. Jemadari aliwachukua askari haraka wakaenda mjini ambako kulikuwa ghasia. Watu walipowaza jemadari na askari wake wakijajia mbojo, waliacha kumpiga Paulo. Baada ya jemadari kumwoko Paulo, aliamuru afungwe kwa minyororo. Jemadari hakujua kwamba Paulo hakuwa na hatia. Alithania kuwa Paulo alitenda kosa kubwa sana ambalo lilwafanya watu

KUTESEKA KWA AJILI YA KRISTO

MASOMO YA BIBLIA: Matendo

21:18-22:29

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wokovu kwa imani katika Yesu Kristo unatolewa bure kwa wenye dhambi, lakini kuwa Mkristo mwanafunzi tunahitaji kwamba tuwe na nia ya kuacha mambo yote kuhusu hali yetu na vitu vyote tulivyo navyo. Paulo alitangaza nia yake ya kuteseka kwa ajili ya Yesu. Katika somo hili tunamwona akijaribiwa. Ilimbidi kufanya uchaguo mguumu sana. Je! angeveza kuwa mwaminifu kwa Yesu bila kujali mambo aliyotendewa na wengine? Kusudi la somo hili ni kuonyesha kwamba ni lazima kuwa mwaminifu kwa Yesu kila siku na kila saa.

Paulo alipokea maonyo ya haraka ya kumzuia kwenda Yerusalemu, lakini maonyo hayo hayakumzuia kwenda. Alipofika Yerusalemu alikwenda nyumbani mwa Yakobo akatoa habari njema kuhusu kazi ambayo Mungu alifanya katika Mataifa kwa huduma yake. Viongozi na Wakristo wa Yerusalemu walifurahi kujua kwamba Mungu alimpatia Paulo ushindi mkuu katika kazi yake ya umisheni.

Tutaona katika somo hili kwamba iliwalazimisha viongozi kumpasha Paulo habari ya kuhuzunisha.

MAMBO YA KUKAZA

1. Paulo alikwenda hekaluni kuwaonyesha Wayahudi kwamba aliamini kutii sheria za Mungu.
2. Paulo alitaka Wakristo Wayahudi kutambua ya kwamba watu wa Mataifa pia walikuwa watu wa Mungu na walipaswa kujua habari za Kristo.
3. Paulo hakunung'unika juu ya mateso yake, bali aliendelea kumshuhudia Kristo.

KULIFUNDISHA SOMO


Viongozi Wakristo ambao walikwisha kumsikia Paulo akieleza habari kuhusu kazi yake ya umisheni, walitaka Wakristo wengine Wayahudi kuelewa maneno ya Paulo na kumwamini. Iliwabidi kumwambia Paulo habari ya kuhuzunisha kwamba Wakristo wengi Wayahudi katika Yerusalemu hawakumwamini. Wakristo hao Wayahudi walikuwa wakimshtaki Paulo kwa kuwafundisha Wayahudi katika nchi nyingine kutotii sheria za Musa. Lakini Paulo hakuwa akiwafundisha Wayahudi wale kutotii sheria za Musa, bali alikuwa akifundisha kwamba imani katika Kristo ndilo lililokuwa jambo muhimu. Baadhi ya sheria ambazo Wayahudi walifikiria kuwa nzuri, Paulo aliwaambia kwamba hazikuwa nzuri kwa sababu hazikuhusiana na

KAZI YA KUFANYA

Jaza nafasi zilizoachwa katika sentensi zifuatazo.

1. Katika somo hili tunamwona Paulo katika mji wa Efeso.
2. Kwanza Paulo alihubiri katika sinagogi.
3. Paulo aliondoka sinagogini akahubiri katika darasa la Tirano.
4. Demetrio aliyekuwa mfua fedha maarufu katika Efeso alitengeneza sanamu za Artemi na vihekalu na kujipatia faida pesa nyingi.

Picha hiyo hapo chini inaonyesha hekalu, pesa, na mikono. Chora mstari kutoka kwa kila swali hadi kwa mojawapo ya vitu hivyo pichani ambacho ndicho jibu la swali hilo.



1. Je, Ni kitu kipi katika picha kinachoonyesha kwamba wafua fedha walipata kwa kufanya sanamu?
2. Je! Paulo alisema kwamba Mungu hawezi kufanywa kwa nini?
3. Je! watu wa Efeso wangehesabu nini kuwa si kitu kama wangeendelea kumsikiliza Paulo?

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Nimemweka Bwana mbele yangu daima, kwa kuwa yako kuumeni kwangu, sitaondoshwa." Zaburi 16:8

Mwandishi wa Zaburi aliyeandika kifungu hiki cha kukumbuka, alisema

kwamba alimweka Bwana mbele yake daima. Kwa kuwa na Bwana karibu hangeweza kuwa na wasiwasi wakati alipoazimu kufanya jambo ambalo lilimfanya kutopendwa na watu

WAKATI WA KUFUNGA

Katika kufunga itakuwa vizuri kueleza juu ya Roho Mtakatifu aliye ndani yetu sisi kama Wakristo. Mungu alimtuma Mwanawe ulimwenguni kuwa Mwokozi wetu. Mwanawe Yesu Kristo, aliwafundisha watu upendo wake. Kristo alipojua ya kwamba wakati wake wa kuondoka ulifika, aliwaambia watu kwamba hangewaacha peke yao; bali angewatumia Roho Mtakatifu kukaa nao daima. Roho Mtakatifu alimpa Paulo nguvu na hekima ya kufanya mambo yaliyompendeza Mungu wala siyo ya kumpendeza mwanadamu.

Waulize wanafunzi: Je! mnaweza kufikiria wakati ambapo unatubidi kuchagua kumpendeza Kristo au kuwapendaza watu? Wasaidie wanafunzi kutambua kwamba wanapopatana na watu vizuri, wakati huo karibu wote wanampendaza Kristo. Wakati mwingine inatubidi kutojali kupendwa na watu ili tuweze kuwa watifu kwa Kristo. Wakati kama huo unapotufikia, Mkristo wa k'veli anaweza kumtegemea Roho Mtakatifu kumtia nguvu ili aonyeshe utii wake wa kwanza kwa mwokozi wake.

Funga kwa maombi ya kwamba mtaweza kuwa waaminifu kwa Kristo wakati wote.

PAUL AENDA YERUSALEMU

MASOMO YA BIBLIA: Matendo
20:13-38; 21:1-19

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Katika sehemu zote za ulimwengu, daima kuna watu ambao hujaribu kutuza kufanya jambo tunalifikiria kuwa haki. Tukijua ya kwamba jambo tunalofanya ni la haki, tuendeleo kufanya katika njia hiyo hata kama wengine wanajaribu kutongoza kufanya katika njia nyingine.

Katika somo hili tunamwona Paulo akiwa na nia ya kwenda Yerusalemu, lakini marafiki zake wanaona hatari itakayompa akienda huko. Wanajaribu kumshawishi asiende. Marafiki hawa wanafanya mambo wanayofikiri kuwa haki kwa Paulo, na inampa Paulo ugonu wa kukataa mashauri yao; ingawa anajua kwamba anafanya jambo la haki.

Wakati unapojiandaa kufundisha, fikiria wanafunzi wako na jinsi somo hili juu ya Paulo linaweza kuwa na mvuto kwa maisha yao. Wako katika umri ambao wanaweza kuwa chini ya mvuto mbaya na pia mzuri.

Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wanafunzi wako kuwa imara kutenda haki hata kama wakambiwa kufanya jambo lingine.

Waonyeshe wanafunzi ya kwamba Paulo alikataa kuacha mambo

aliyoaamini kuwa ndiyo mapenzi ya Bwana kwake.

MAMBO YA KUKAZA

1. Paulo alikataa mawazo yake mwenyewe yaliyomshawishi kutofuata mapenzi ya Mungu.
2. Paulo alikataa kushawishiwa na marafiki zake kutofuata mapenzi ya Mungu.
3. Sisi pia inatupasa kuwa na nia ya kwenda kumshuhudia Bwana mahali po pote.

KULIFUNDISHA SOMO

Tume kuwa tukisafiri na Paulo katika safari yake ya tatu ya umisheni. Sasa anafanya mipango ya kurudi Yerusalemu.

Baada ya ghasia iliyotokea Efeso, Paulo alipita Makedonia na kutembelea makanisa pale. Kisha aliendelea na safari mpaka Uyunani. Waambie wanafunzi kutafuta Efeso katika ramani, na kufuata njia itokayo Efeso kwenda Makedonia na Uyunani. Labda aliabiri kutoka Efeso mpaka Makedonia. Kisha alitembea kwa miguu kupitia nchi hiyo ya Makedonia mpaka Uyunani. Paulo alikaa Uyunani kwa miezi mitatu. Alipanga kuabiri kwenda Troa, kisha kutembelea kupitia mji alipotaka kutembelea na kwenda Yerusalemu. Mwambie mwanafunzi



KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Kisha nikaisikia sauti ya Bwana, akisema, Nintume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi." Isaya 6:8

Kifungu hiki cha kukumbuka kinajieleza chenyewe. Yatupasa sisi sote kumsikiliza Bwana na kumtii. Labda anataka wewe au mwanafunzi wako ye yote kuwapelekea wengine neno lake. Wakati huu sasa ambapo unajifunza kufundisha darasa lako, unamtii Mungu na unawapelekea wanafunzi wako neno lake.

WAKATI WA KUFUNGA

Waulize wanafunzi wako maswali haya: Je! basikeli ingekuwa na msada gani kama ingetumiwa kwa muda tu na kuharibika? Saa (ya mkono) ingekuwa na msada gani kama mtu anayeivaa hawezi kuitegemea? Askari angekuwa na usiadizi gani kama hawezi kumtii afisa wake wakati wote? Je! Paulo angalikuwa na msada gani kama angalimtii Bwana kwa wakati fulani tu?

Funga kwa maombi.

angekabiliwa na hatari ya kufungwa gerezeni. Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma majibu ya Paulo katika Matendo 21:13. Hata mwishowe marafiki hawa waliona kwamba hawakuwa na jambo la kusema wala kufanya ili kubadili nia ya Paulo. Waliacha kumsihi asiende wakamwomba wakisema, "Mapenzi ya Bwana yatendeke."

Paulo alifunga safari kwenda Yerusalemu bila kujali maonyo yale, akijua wazi kwamba alikabiliwa na mateso na taabu. Ingawa marafiki zake hawakumtaka kwenda, walikwenda pamoja naye. Hii ilikuwa mara ya tano Paulo kutembelea Yerusalemu tangu alipokuwa Mkristo. Katika mji huu, Wakristo wengine waaminifu walipenda sana Paulo kuwatembelea. Wakati alipowasili huko walimpokea na furaha.

Siku ya pili baada ya Paulo kuwasili Yerusalemu, yeye na marafiki zake walikwenda kumwona Yakobo ambaye alikuwa kiongozi wa kanisa la Yerusalemu. Viongozi na wazee walikuja kusikia habari kuhusu huduma ya Paulo. Paulo aliwaambia mambo yote kuhusu kazi ambayo Bwana alitenda katika Mataifa kwa huduma yake. Alivaeleza miji yote ambayo alitembelea na makanisa mapya waliyoanzishwa.

Tangu Paulo kuwa Mkristo, alimtii Bwana wakati wote. Aliwaza moyoni kwamba Bwana alimtaka kurejea

Yerusalemu, na ingawa marafiki zake waliompenda walijaribu kumzuia kuingia hatarini, Paulo alikuwa akimsikiza Mungu badala ya kuwasikiliza wao.

KAZI YA KUFANYA

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kuandika majibu ya kweli katika nafasi zilizoacha.

1. Paulo alikuwa amepanga kwenda Uyunani. Alibadilisha nia yake kwa sababu Wayahudi walipanga kumwua.
2. Waamini wa Tiro walimwonya Paulo ya kwamba asiende Yerusalemu.

3. Wakati wa Paulo kuondoka Tiro ulipofika, Wakristo wote walim-sindikiza mpaka pwani.

4. Kabla Paulo kuondoka Tiro, walipiga magoti pwani, wakaomba.

5. Katika Kaisaria, Paulo na marafiki zake walikaa nyumbani mwa Filipo.

Katika Kaisaria, marafiki za Paulo walimsihi asiende Yerusalemu. Lakini Paulo aliwaambia kwamba alikuwa tayari kuuawa kwa ajili ya Bwana. Marafiki zake hawakuweza kumbadili nia. Andika maneno ambayo walimwambia.

mmoja kusoma Matendo 20:3 mpate kuona sababu iliyomfanya Paulo kubadili mipango yake ya kuabiri. Alitembea kwa miguu kupitia Makedonia tena mpaka Filipo ambako alingia mashua na kuabiri hadi Troa.

Paulo na marafiki zake, Luka na Timotheo, walikaa Troa kwa muda wa siku saba. Alikuwa na haraka kurudi Yerusalemu kuadhimisha Karamu ya Pentekoste kwa hivyo hakuwa na wakati wa kwenda Efeso tena. Aliwauliza wazee wa kanisa la Efeso kukutana naye Milato. Wasaidie wanafunzi kutafuta miji ya Efeso na Milato katika ramani wapate kuona jinsi miji hii miwili ilivyo karibu.

Katika Milato ndipo Paulo alipowapa wazee wale maneno ya mwisho. Aliwaambia pengine hawangeweza kumwona uso tena. Aliwaambia ya kwamba sasa uongozi wa makanisa ungekuwa chini yao. Pia aliwaambia kwamba alikwisha kuonywa asirejee Yerusalemu, na kwamba akirejee angekabiliwa na mateso na taabu. Pia aliyajibuje maonyo haya? Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 20:24. Paulo alikusudia kurejea Yerusalemu kwa sababu aliwaza moyoni mwake ya kwamba Bwana ndiye aliyemtaka kurejea huko.

Baada ya Paulo kuwaaga wazee wale wa Efeso, merikebu ambayo yeye pamoja na marafiki zake walisafiria ilikwenda hadi kisiwa cha Kosi. Siku ya pili yake walifika Rodo.

Kutoka Rodo waliendelea na safari mpaka Patara. Kutoka Patara walisafiri mpaka Foinike karibu na pwani ya Kipro, kisha wakashuka Tiro. Waambie wanafunzi kufuata safari hii katika ramani yao.

Merikebu waliyokuwa nayo ndani ilishusha shehena yake hapa Tiro na ikakaa kwa muda wa siku saba. Paulo aliwakuta Wakristo marafiki katika mji huu. Marafiki hawa walipoambiwa na Paulo ya kwamba alikuwa safarini kwenda Yerusalemu, walimwonya asiende. Walimwambia angekabiliwa na hatari kama akienda huko. Lakini Paulo aliwaambia hana budi kwenda kwa maana aliona ni Bwana ndiye aliyemtaka aende Yerusalemu. Marafiki hao walimsindikiza hadi pwani, kisha wote wakupiga magoti wakaomba.



Kutoka Tiro, Paulo na marafiki zake walisafiri mpaka Kaisaria na wakakaa nyumbani mwa Filipo kwa siku chache. Hapa tena Paulo alionywa asiende Yerusalemu kwa maana

Ulimwengu katika
Siku za Paulo

